# MWUJIZA WA AHMAD

Na

Hadhrat Mirza Ghulam Ahmad[as] wa Qadian
Masihi Mau'udi na Imam Mahdi

ISLAM INTERNATIONAL PUBLICATIONS LTD

# Mwujiza wa Ahmad

Tafsiri ya Kiswahili ya: I'jaz Ahmadi (Kiurdu)

I'jaz Ahmadi (Swahili Translation)

**Mwandishi:**
Hadhrat Mirza Ghulam Ahmad[as] wa Qadian

**Mfasiri:**
Sheikh Muzaffar Ahmad Durrani

Chapa ya Kwanza kwa Sura ya Makala (Kiurdu): 1902
Chapa ya Kwanza (Kiswahili): 2024

© Islam International Publications Ltd.

**Kwa Maelezo Zaidi:**

**Tanzania:**
Jumuiya ya Waislamu Waahmadiyya, Tanzania
Mtaa wa Bibi Titi Mohamed S.L.P. 376, Dar es Salaam.
Simu: +255222110473 Fax: +255222121744

**Kenya:**
E.A. Ahmadiyya Muslim Mission
P.O. Box 40554 Nairobi Kenya Simu: +254222111031

Kimechapwa na Ahmadiyya Printing Press
Dar es Salaam, Tanzania / Nairobi, Kenya

**ISBN:** 978-1-84880-779-2
10 9 8 7 6 5 4 3 2 1

# NENO LA MWENEZI

Twawaletea wasomaji wa Kiswahili tafsiri ya kitabu cha Mwanzilishi wa Jumuiya ya Waislamu Waahmadiyya kiitwacho Mwujiza wa Ahmad – *I'jaz Ahmadi* – ambacho kwa hakika ndio mwujiza hasa. Kitabu chenyewe ni Nyongeza ya kitabu cha *Nuzuulul-Masih*.

Katika kijiji kimoja cha India kinachoitwa *Mudd*, Wilaya ya Amritsar, ndugu mmoja Mian Muhammad Ya'kub alipojiunga na Jumuiya ya Waislamu Waahmadiyya, wenyeji wa kijiji hicho walifyeruka sana na kumsusia. Kisha ikaamuliwa ufanywe mjadala tarehe 29, 30 Oktoba 1902 kijijini, baina ya wataalamu wa Waahmadiyya na Waislamu wengine. Seyidna Ahmad[as] akawatuma Maulawii Seyid Muhammad Sarwar Shah na Maulawii Abdullah Mkashmiri; Masuni wakamteua Maulawii Thana'ullah wa Amritsar kwa mjadala. Waliohudhuria kusikiliza mjadala walikuwa wapatao mia saba, lakini Waahmadiyya walikuwa wanne tu.

Hadhrat Maulawii Seyid Muhammad Sarwar Shah akamwuliza Maulawii Thana'ullah, mbona hukuandika jibu la *I'jazul Masih* ilhali ulidai kuwa unaweza kuandika kwa urahisi sana. Maulawii Thana'ullah alikuwa hana la kusema. Akasema tu kwamba yuko tayari kufanya *mubahala* na Seyidna Ahmad[as] na akadai kuwa bishara zote za Seyidna Ahmad[as] zilibatilika. Yeye

hakuhakikisha kabisa madai yake, bali akatumia tu mdomo mchafu sana kupita hata maadui wakali sana wa Jumuiya ya Waahmadiyya na wahudhuriao wakamshangilia kwa sababu ya chuki waliyokuwa nayo nyoyoni mwao dhidi ya Waahmadiyya.

Seyidna Ahmad[as] alipoletewa taarifa ya mjadala huo, akafikiria sana njia itakayoweza kupambanua ukweli mbali na uwongo. Akamwomba Mwenyezi Mungu na akaamua kutunga kasida kwa Kiarabu fasaha ambamo ataeleza habari za mjadala wa Mudd.

Seyidna Ahmad[as] akaanza kutunga kasida 8 Novemba 1902 na kumaliza 12 Novemba, katika siku tano, kwa msaada maalumu wa Mwenyezi Mungu. Na akatangaza kwamba kama Maulawii Thanau'llah na masheikh wenzake wakiweza kuijibu kasida hii kwa kutunga kasida, kila mmoja peke yake au kwa kujumuika wote pamoja, ndani ya siku tano, nitawapa zawadi ya rupia elfu kumi. Pia akaandika insha fupi kwa Kiurdu ambayo nayo wakapaswa kujibu.

Seyidna Ahmad[as] akaandika kwamba hao wakiweza kuandika kasida na jibu la insha ya Kiurdu, si tu watapata rupia elfu kumi, bali nitathibitika kuwa mwongo katika madai yangu, na wafuasi wangu wote watapaswa kutengana nami. Lakini akatangaza kuwa

Mola wangu Ameishapokea dua yangu, basi hakuna atakayemudu kuandika kasida na jawabu la insha ya Kiurdu. Akasema: Mungu Amewapumbaza akili zao, Amevunjilia mbali kalamu zao.

Ndani ya kitabu hiki mtaweza kusoma kasida hiyo yenye beti 533, pamoja na tafsiri kwa Kiswahili.

Kasida ya Seyidna Ahmad[as] ipo kwenye *Bahari ya Tawiil* (بحر طويل) na imetiliwa irabu kulingana na arudhi – njia isiyotumika katika nathari, lakini ni ya kawaida sana katika shairi. Basi mtakuta pengine badala ya *fat'h*, *dhamm* na *kasr*, herufi fulani imetiliwa *sukuun*; msishangae, washairi wa Kiarabu wanaielewa kabisa kanuni hii.

Wanajopo wetu kwa kujibidiisha fika wamejaliwa kutayarisha tafsiri hii, kuidurusu na kuitengeneza fomati. Mwenyezi Mungu Awapatie malipo bora. Amin

Munir-ud-Din Shams
Wakilut Tasnif wa Ziada
London 19 Novemba 2023

الحمد للہ والمنۃ کہ ضمیمہ نزول المسیح جس کے ساتھ

## دس ہزار روپیہ کا اشتہار ہے

حسب وعدہ مولوی ثناء اللہ صاحب امرتسری کے
محض پانچ دن میں ابتداء نومبر ۱۹۰۲ء سے
طیار ہو کر اسکا نام

# اعجاز احمدی

رکھا گیا

اور اس رسالہ میں پیر مہر علیشاہ صاحب و مولوی اصغر علی صاحب
و مولوی علی حائری صاحب شیعہ وغیرہ بھی مخاطب ہیں جنکا نام
رسالہ میں مفصل درج ہے (تاریخ طبع ۱۵ دسمبر ۱۹۰۲ء)

بمقام قادیان باہتمام حکیم فضل الدین صاحب مطبع ضیاء الاسلام میں طبع ہوا

مملوکہ ماسٹر نور الٰہی ہومیو پیتھ دارالامان قادیان

تعداد اشاعت ۲۵۰۰

Jalada la chapa ya kwanza

Je, Allah Hamtoshei mtumishi Wake? Je, Allah Hamtoshei mtumishi Wake?
Je, Allah Hamtoshei mtumishi Wake?

Je, Allah Hamtoshei mtumishi Wake? Je, Allah Hamtoshei mtumishi Wake? Je, Allah Hamtoshei mtumishi Wake? Je, Allah Hamtoshei mtumishi Wake?

Sifa zote njema ni za Allah na hisani yake kwamba Nyongeza ya Nuzuulul Masih sawa na ombi la Maulawii Thana'ullah wa Amritsar, ambayo pamoja nayo limeambatanishwa

**Tangazo la Zawadi ya Rupia Elfu Kumi,**

ikitayarishwa tarehe 8 Novemba 1902 ndani ya siku tano tu ikaitwa

# Mwujiza wa Ahmad

Na ndani ya kitabu hiki Pir Mehr Ali Shah, Maulawii Asghar Ali, Mshia Maulawii Ali Ha'irii na wengineo wameshughulikiwa ambao majina yao yametajwa humu. (Tarehe ya kuchapishwa: 15 Novemba 1902)

Kimepigwa chapa Qadian, chini ya usimamizi wa Hakiim Fadhlud-Din, ndani ya Matbaa Dhiaul-Islam, iliyomilikiwa na Master Nur Ilahi, tabibu wa Homeopathi.

Je, Allah Hamtoshei mtumishi Wake? Je, Allah Hamtoshei mtumishi Wake? Je, Allah Hamtoshei mtumishi Wake? Je, Allah Hamtoshei mtumishi Wake?

Je, Allah Hamtoshei mtumishi Wake? Je, Allah Hamtoshei mtumishi Wake?
Je, Allah Hamtoshei mtumishi Wake?

Nakala 3500

بِسۡمِ اللّٰهِ الرَّحۡمٰنِ الرَّحِیۡمِ [1]

نَحۡمَدُہٗ وَ نُصَلِّیۡ عَلٰی رَسُوۡلِہِ الۡکَرِیۡمِ [2]

# NYONGEZA YA KITABU ‘KUSHUKA KWA MASIHI’

Iliandikwa 6 Shaabani 1320 Hijra, siku ya Jumamosi, iliyo 8 Novemba 1902, ambayo pamoja nayo kuna tangazo la zawadi ya rupia elfu kumi.

رَبَّنَا افۡتَحۡ بَیۡنَنَا وَ بَیۡنَ قَوۡمِنَا بِالۡحَقِّ وَ اَنۡتَ خَیۡرُ الۡفٰتِحِیۡنَ [3]

Ee Mola wetu, hukumu baina yetu na baina ya kaumu yetu kwa haki, nawe ndiwe Mbora wa wanaohukumu.

Enyi wasomaji, Mungu Awaongozeni. Ibainike kwenu kwamba haja ilisikika kuandika makala hii kwamba kijijini Mudd, wilaya ya Amritsar, marafiki zangu wawili wenye ikhlasi walikwenda katika mjadala kwa kusisitizwa na Munshi Muhammad Yusuf. Kwa upande wetu Maulawii Muhammad Sarwar akawekwa kujadili na kundi la pili walimwita Maulawii Thana’ullah kutoka Amritsar. Kama Maulawii Thana’ullah asingetumia hiana na uongo katika

---

[1] Kwa jina la Mwenyezi Mungu, Mwingi wa rehema, Mwingi wa ukarimu.

[2] Twamhimidia Yeye na kumsalia Mtume wake Mkarimu.

[3] Al-A‘raaf 7:90

☆ Kwa kuwa nilitakiwa kwenda Batala, 7 Novemba 1902, kwa hiyo makala hii ilichelewa kuandikwa. Mwandishi

majadiliano, isingehitajika kuandika makala hii. Lakini, kwa kuwa Bwana Maulawii aliyetajwa akaona ni faradhi yake kukadhibisha bishara zangu na kuongopa, kwa hiyo Mungu Akanielekeza kuandika makala hii, ili adhalilike kila aongopaye. Enyi waadilifu, haijafichika kwa wasomaji wa kitabu chetu *Nuzuulul-Masihi* zilimoandikwa ishara za kimbingu mia na hamsini kwa ushahidi wa mamia ya mashahidi. Haikufichika kwamba ishara kamilifu na takatifu zinaendelea kunyesha kama mvua; na kama mashahidi wote wa bishara hizo kutimia wajumuishwe, nafikiri watakuwa zaidi ya hata laki sitini. Lakini, ni sikitiko kwamba chuki na upendo wa dunia ni maradhi ya kulaaniwa ambayo kwayo mtu haoni huku anaona, na hasikii huku anasikia, na haelewei huku anaelewa. Naapa kwa Mungu Ambaye uhai wangu umo mkononi Mwake kwamba ishara zilizodhihirishwa kwa ajili yangu na kutokea kuhakikisha ukweli wangu, kama mashahidi wao wasimamishwe mahali pamoja, basi hatakuwa mfalme yeyote duniani mwenye wanajeshi wake zaidi kuliko mashahidi hao. Hata hivyo dhambi za namna namna zaendelea kutendeka ardhini kiasi hiki kwamba watu wanakadhibisha ishara hizi pia.

Mbingu imeshuhudia kwa ajili yangu na ardhi pia, lakini watu wengi wa dunia hawakunikubali. Mimi ndimi yule ambaye katika wakati wake ngamia wameachwa na

bishara ya aya takatifu وَاِذَا الۡعِشَارُ عُطِّلَتۡ[4] imetimia, na bishara ya Hadithi وَ لَيُتْرَكَنَّ الْقِلَاصُ فَلَا يُسْعٰى عَلَيْهَا ikaonyesha mng'ao wake kamili kiasi hiki kwamba wahariri wa magazeti na majarida wa Arabuni na wa Ajemi pia wakapaza sauti katika matoleo yao kwamba reli inayotayarishwa baina ya Madina na Makka ni dhihirisho la bishara ile iliyotolewa kwa maneno haya katika Kurani na Hadithi, iliyo alama ya wakati wa Masihi Mau'udi. Kadhalika katika Vitabu vyote vya Mungu ilihabarishwa kwamba katika wakati wa Masihi Mau'udi tauni itaenea na hija itazuiliwa na nyota ذُوالسِّنِيْن (*dhussinii*) itatokea. Na mwanzoni mwa Elfu ya Saba, Mau'udi yule atadhihiri aliyepangwa kutokea upande wa mashariki ya Damasko na kwamba atajidhihirisha mwanzoni mwa karne ambapo msalaba utakuwa umepata ushindi mkubwa sana. Basi, leo mambo hayo yote yameshatimia, na ili kunisaidia Mungu Ameonyesha ishara kubwa kwa mkono wangu. Kifo cha Atham kilikuwa ni ishara kubwa iliyodhihirika sawa na bishara. Miaka kumi na miwili hapo kabla katika ***Baraahine Ahmadiyya*** pia iliashiriwa kwenye hii na Hadithi moja pia ilipasha habari ya tukio hili, lakini wakorofi wakaidhihaki na hawakuikubali. Na muda wa bishara hii ulikuwa na sharti; na bishara haikutolewa kwa sababu yu Mkristo, bali kama vile katika kitabu

[4] Na ngamia watakapoachwa. At-Takwiir 81:5

kinachoeleza mjadala, waliouita Wakristo '*Vita Takatifu*', imeandikwa sababu ya kutolewa bishara ni hii tu kwamba katika kitabu chake *Andruna Baibal* alimwita Mtume Mtukufu[saw] jina dajali. Basi, wakati wa kutoa bishara, yeye aliambiwa mbele ya watu wapatao sabini kwamba sababu ya bishara hii ndiyo hii tu kwamba ulimwita Nabii wetu[saw] dajali. Basi, kama hutarejea na neno hili, utahilikishwa katika miezi kumi na mitano. Hapo Atham katika kikao hicho hicho akarejea na akasema najikinga kwa Mungu, sijasema neno kama hilo kwa Mtume[saw] na akanyanyua mikono miwili na katoa ulimi kutoka kinywani na akitetemeka akakanusha kwa ulimi wake, na mashahidi wa tukio hilo si tu Waislamu, bali Wakristo zaidi ya arobaini pia ndio mashahidi. Je, hiyo si kurejea kwake? Na je kuogopa kwake, na katika muda wa bishara kuacha kabisa majadiliano aliyokuwa akifanya sikuzote nami na marehemu Sheikh Ghulam Hasan chifu mkuu wa Amritsar pia na Mian Ghulam Nabii nduguye marehemu Mian Asadullah wakili wa Amritsar pia. Je hii siyo dalili kwamba lazima aliogopa. Na je kuondoka Amritsar na kuishi kukaa kimya katika mazingira ya kigeni na kulia sana siyo dalili kwamba moyo wake ulitishika na kutetemeka. Na je licha ya kuahidiwa rupia elfu nne kutoapa ilihali ikathibitishwa kwamba inajuzu kuapa katika dini ya Kikristo, bali Bwana Yesu mwenyewe pia aliapa na vile vile Paulo. Je hii siyo dalili kwamba

akashikwa na hofu? Basi, je bado haijathibitika kurejea kwake katika kauli ya kuita dajali? Na nani aweza kuthibitisha kwamba baada yake katika muda wa bishara alimwita Mtume[saw] dajali? Kisha juu ya hii kama ilivyokuwa katika bishara yangu kwamba mwongo atakufa katika uhai wa mkweli, je hakufa katika uhai wangu? Kama bishara haikutimia, basi niambieni Atham yupo wapi? Umri wake ulikuwa sawa na umri wangu, yaani karibu na miaka 64. Kama mna shaka, basi tazameni karatasi zake za pensheni katika afisi ya serikali kwamba lini na katika umri gani akapata pensheni. Ikiwa bishara haikuwa sahihi, kwa nini alikufa kabla yangu. Laana ya Mungu iwe juu ya wasemao uongo. Mtu anapoacha haya, basi aropoke atakavyo, nani anamzuia.

Angalieni, kuhusu Lekhram bishara iliyotolewa, ilielezwa humo waziwazi kwamba katika miaka sita atahilikishwa kwa kuuawa siku itakayokuwa imeungana na siku ya Idi, ikatimia kimachomacho hata kwamba Fateh Ali Shah, Deputy Collector, na kadhalika, waheshimiwa wapatao elfu nne wakitayarisha kumbukumbu wakaandika kwamba bishara hii imetimia barabara, ilihali watu hao walikuwa miongoni mwa kundi la wapinzani, lakini hata hivyo masheikh hao wa jina wasiomcha Mungu hawakubali. Upo ushuhuda mwingi ulioandikwa na ndugu zao wahehimiwa, bali katika kumbukumbu hiyo

wapo Mabaniani wengi pia, lakini chuki ni kitu kinachowapofusha binadamu. Bishara hizi ndizo ambazo mtu mkweli akizisikia machozi yake yatatiririka, lakini hata hivyo watu hao husema bishara yoyote haikutimia. Hawakumbuki kwamba hatimaye sisi pia tutakufa siku moja. Ishara walizoonyeshewa hao kama wangeonyeshewa watu wa Nuhu wasingegharikі; na kama kaumu ya Luti wangepata habari zake wasingenyeshewa mawe. Lakini, watu hao wanaona jua lakini husema upo usiku; hao wamewazidi hata Wayahudi. Kukadhibisha ishara za Mungu si jambo hafifu, mwisho wake haukuwa mwema katika zama zozote; basi je sasa utakuwa mwema? Lakini, katika zama hizi ukanaji Mungu umezagaa na mioyo imekuwa migumu na haiogopi. Niwafananishe hao na nani? Watu hao wanafanana na kipofu anayekanusha uwepo wa jua na hatambui upofu wake. Watu hao ni kama Wayahudi na Wakristo wasioona mamia ya misaada na miujiza ya Mungu iliyodhihiri kwa mkono wa Mtume Mtukufu[saw], na hutaja-taja vita ya Uhud na habari ya Hudaibia, na hiyo ndiyo hali ya Wayahudi kuhusu Hadhrat Masihi[as] pia.

Siku hizi kitabu cha Myahudi mmoja kimechapishwa kilichopo kwangu wakati huu, kana kwamba ni kitabu cha Maulawii Muhammad Husain au Maulawii Thana'ullah. Anaandika katika kitabu chake kwamba mtu

huyo, yaani Isa[as], hakuonyesha hata muujiza mmoja wala bishara yake yoyote haikutimia. Akasema, nitapewa kiti cha enzi cha Daudi. Alipataje? Akasema, wanafunzi kumi na wawili watapata viti kumi na viwili huko Peponi. Walipataje viti hao kumi na wawili? Yuda Iskariote akichukua rupia thelathini akatengana naye na akaondolewa katika wanafunzi, na Petro akamlaani mara tatu, je akastahiki kupata kiti? Isitoshe, akasema kwamba watu wa zama hizi hawatakufa mpaka nitarudi; wapi akarudi? Kisha, huyo Myahudi anaandika kwamba yatosha kuhakikisha yeye kuwa mwongo kwamba katika kitabu cha Malaki tulipashwa habari kuwa Masihi mkweli mwenye kuja katika Wayahudi hatakuja kamwe mpaka Nabii Eliya arudi tena duniani. Sasa, wapi Eliya akashuka kutoka mbinguni? Kisha, katika sehemu hii anapiga kelele sana na anawasihi watu kwamba angalieni, katika kitabu cha Nabii Malaki bishara yenyewe ilikuwa ni hii kwamba Eliya mwenyewe atakuja tena duniani, lakini mtu huyo anamwita Yohana (anayetambulika kwa jina la Yahya baina ya Waislamu) kuwa Eliya, kana kwamba anamwita mithili yake; lakini Mungu Hakutupatia habari ya mithili, bali alisema waziwazi kwamba Eliya mwenyewe atakuja tena. Na hata tukiulizwa siku ya Kiama, tutaweka kitabu hiki hiki mbele ya Mungu kwamba wapi Uliandika mithili ya Eliya atatumwa kabla ya Masihi Mau‘udi. Na baada ya

kuandika hayo anamtukana sana Hadhrat Masihi. Kitabu kipo, akione atakaye.

Semeni sasa, moyo wa Myahudi huyo na Maulawii Muhammad Husain na Maulawii Thana'ullah unafanana au la? Kuhusu bishara yangu fulani kuwa kinyume wanasema uongo sana ilihali bishara yangu hata moja haikubatilika, bali bishara zote zimetimia waziwazi. Bishara zenye sharti zimetimia sawa na sharti na zitatimia; na bishara zisizokuwa na sharti kama vile bishara kuhusu Lekhram, zikatimia zilivyokuwa. Hii ni hakika hasa ya bishara zangu. Lakini kuhusu bishara za Hadhrat Isa[as], upinzani alioleta huyo Myahudi mtaalamu, ni mkali sana, bali ni mkali kiasi hiki kwamba hata sisi pia hatujui jibu lake. Na kama akiweza kujibu upinzani huo Maulawii Thana'ullah au Maulawii Muhammad Husain au yeyote miongoni mwa mapadri, basi tutampa rupia mia moja taslimu kama zawadi. Kaitwa Mungu, na hali ndiyo hii ya bishara! Hata sisi pia twaajabika juu yake. Bishara kama hizo hata haziwezi kutanguliwa ili idhaniwa kwamba zilitanguliwa. Naam, bishara kuhusu onyo kama vile bishara kuhusu Atham au bishara kuhusu mkwe wa Ahmad Beg ni bishara ambazo zinaweza kuahirishwa pia sawa na Kurani na Torati; na kuahirishwa kwao hakulazimu kuwa zilikuwa batili. Kwani Mungu Anayo hiari ya kuzuia onyo lake kama ilivyo itikadi ya Waislamu na Wakristo, kwa sababu bishara ya Nabii Yunus

iliyokuwa kuhusu adhabu haikukuwa na sharti yoyote ya toba, hata hivyo ikafutika, na hakuna Mwislamu au Mkristo awezaye kusema kwamba Yunus[as] alikuwa mwongo. Someni kitabu cha Yona Nabii na *Durri Manthur*.

Sasa ni ajabu sana kwamba wapinzani wangu wananiletea upinzani ambao kwao wanalazimika hata kuachana na Islam. Kama wangekuwa na takwa moyoni mwao, wasingeleta upinzani kama huo ambao Manabii wengi zaidi wanashirikiana katika huo. Kisha inastaajabisha kwamba maelfu ya bishara zilizotimia dhahiri shahiri hawazitupii macho. Na kama bishara moja wasipoweza kuelewa kwa ujinga wao, basi huitaja mara kwa mara. Je huu ni uaminifu? Kama wakitafuta haki, basi njia ya kuamua ilikuwa rahisi kwamba wenyewe wangekuja Qadian na ningewapa matumizi pia ya kuja na kurudi na nimewakaribisha kama wageni ndipo wangepata kujituliza kwa moyo mkunjufu. Kupinga kwa kukaa mbali, bila kupata uhakika kamili, ni kwa sababu ya ujinga na chuki. Safari moja wajinga wa namna hii wapatao mia tano wakatengana na Hadhrat Masihi, kwani bishara za mtu huyo hazijatimia. Na kwa kweli, sababu ya Yuda Iskariote kuritadi ilikuwa hii kwamba silaha zilinunuliwa hadharani lakini yote yakawa bure, wala bishara kurithi kiti cha enzi cha Daudi haikutimia, hatimaye Yuda akichoka akaritadi. Masihi naye hakupata kujua kwamba huyo ataacha imani

na akamwahidia kiti cha Peponi bila sababu yoyote. Kadhalika baadhi ya wapinzani wakaleta upinzani juu ya safari ya Hudaibia kwamba bishara hii haikutimia. Na safari ndefu ilionyesha kwamba fikara ya Mtume Mtukufu[saw] ilielekea kwenye hii kwamba wataidhinishwa kuizunguka Kaaba kama ilivyotabiriwa. Hapo baadhi ya wenye bahati mbaya wakaritadi; na Hadhrat Umar[ra] akapata majaribio kwa siku chache na hatimaye kwa kusamehewa kosa hili akatenda matendo mengi mema kama ilivyo dhahiri kutokana na kauli yake. Mifano hii ipo kwa wenye bahati mbaya, hata hivyo wapinzani wajinga wenye bahati mbaya wa wakati huu wanaikimbilia bahati mbaya, na bahati mbaya inawashinda, hawajizuii. Wamezusha upinzani wa aina aina. Mathalani, wasema kwamba kabla ya kudai kuwa Masihi Mau'udi nimekiri katika *Baraahine Ahmadiyya* ujio wa Hadhrat Isa[as]. Enyi wajinga, kwa nini mnaharibu ahera yenu. Katika ikrari hiyo imeandikwa wapi kwamba ninaeleza hii kwa wahyi wa Mungu, na lini nimedai kwamba mimi ni mjuzi wa ghaibu. Nilikuwa na itikadi hii hii iliyo itikadi yenu mpaka Mungu Akanielekeza kwenye hii na kunifahamisha mara kwa mara kwamba u Masihi Mau'udi, na Isa[as] ameshafariki. Kwa sababu hiyo, kwa moyo mweupe, niliandika katika *Baraahin* kuhusu ujio wa Hadhrat Masihi[as]. Lakini, Mungu Aliponifungulia uhakika wenyewe basi nikaachana na itikadi hiyo. Sikuacha itikadi

ile ya kawaida isipokuwa kwa sababu ya yakini kamili iliyozingira moyo wangu na kunijaza nuru, ilihali katika *Baraahin* hiyo hiyo nikaitwa Isa na nikafanywa kuwa Khatamul Khulafaa na ikasemwa kunihusu kwamba wewe ndiwe utakayevunja msalaba, na nikaambiwa kwamba habari yako imo katika Kurani na katika Hadithi na wewe ndiwe unayehusikana na aya hii: هُوَ الَّذِیۡۤ اَرۡسَلَ رَسُوۡلَہٗ بِالۡہُدٰی وَ دِیۡنِ الۡحَقِّ لِیُظۡہِرَہٗ عَلَی الدِّیۡنِ کُلِّہٖ[5]

Lakini, ufunuo huu ulioandikwa waziwazi katika *Baraahine Ahmadiyya,* hekima ya Mungu iliuficha nisiuone, na kwa sababu hii licha ya kuitwa Masihi Mau'udi waziwazi ndani ya *Baraahine Ahmadiyya* kwa sababu ya mghafala uliotiliwa moyoni mwangu nikaandika itikadi ya ujio wa mara ya pili wa Hadhrat Isa[as] katika *Baraahine Ahmadiyya*. Basi, huu ni ushahidi juu ya moyo wangu mweupe sana na mghafala wangu kwamba ingawa ufunuo wa Mungu ulioandikwa katika *Baraahine Ahmadiyya* ulinifanya Masihi Mau'udi, lakini nikaandika itikadi hii ya kawaida katika *Baraahin*. Mimi mwenyewe naajabika kwamba licha ya ufunuo wazi ulionifanya Masihi Mau'udi kivipi nikaandika itikadi ya kawaida katika kitabu hicho.

[5] Yeye ndiye Aliyemtuma Mtume Wake kwa mwongozo na kwa dini ya haki ili kuifanya izishinde dini zote. As-Saff 61:10

Kisha kwa miaka kumi na miwili – muda ulio mrefu – nikaendelea kughafilika kwamba Mungu kwa kusisitiza sana Ameniita Masihi Mau‘udi katika *Baraahin* lakini nikaendelea kukaa imara juu ya itikadi ya kawaida ya ujio wa mara ya pili wa Hadhrat Isa[as]. Miaka kumi na miwili ilipopita ndipo wakati ukawadia kwamba nifahamishwe uhakika wenyewe, hapo funuo zikaanza kufululiza kwamba wewe ndiwe Masihi Mau‘udi.

Basi, Wahyi wa Mungu ulipofikia kileleni kuhusu habari hii na nikaamrishwa فَاصۡدَعۡ بِمَا تُؤۡمَرُ , yaani unayoamrishwa uwafikishie watu kwa uwazi, na nikapewa ishara nyingi na nikatiliwa moyoni mwangu yakini kama mchana ndipo nikawafikishia watu ujumbe huu. Mpango huu wa Mungu ulikuwa ni dalili ya ukweli wangu na ilikuwa alama ya ikhlasi yangu na kutokujisingizia. Kama kazi hii ingekuwa ya mwanadamu na mzizi wake ungekuwa hila ya kibinadamu, basi ningedai wakati ule wa *Baraahine Ahmadiyya* kwamba mimi ni Masihi Mau‘udi, lakini Mungu Akageuza fikara yangu, sikuweza kufahamu ufunuo wa *Baraahin* kwamba unanifanya Masihi Mau‘udi. Hii ilikuwa ikhlasi yangu ambayo ni dalili kubwa juu ya ukweli wangu. La sivyo, wapinzani wangu waniambie kwamba licha ya kufanywa Masihi Mau‘udi katika *Baraahine Ahmadiyya*, kwa nini sikutangaza dai hili kwa miaka kumi na miwili na kwa nini nikaandika katika

*Baraahin* kinyume cha ufunuo wa Mungu. Je hii iliyofanyika haipaswi kutafakariwa? Je hii siyo hiana kwamba wanataja ibara hii ya *Baraahine Ahmadiyya* nilimoeleza sawa na itikadi rasmi ya watu wote ujaji wa mara ya pili wa Masihi, lakini hawataji kwamba katika *Baraahine Ahmadiyya* hiyo kuna dai la kuwa Masihi Mau'udi pia. Hii ni hoja nyepesi Aliyoniwekea Mungu mapema ndani ya *Baraahine Ahmadiyya*. Hata adui pia anaweza kushuhudia kwamba wakati wa kuandika *Baraahine Ahmadiyya* sikuwa na habari kwamba mimi ndiye Masihi Mau'udi, ndiyo maana sikudai hivi wakati huo. Basi, kuhusu funuo zinazoniita Masihi Mau'udi katika zama za kutotambua kwangu zinawezaje kuwa na shaka kwamba ni uzushi wa mtu! Kwani, kama zingekuwa ni uzushi wangu basi ningejifaidisha nazo kutoka katika *Baraahin* hiyo na kutoa madai yangu, na ingeyumkinaje kwamba ningeandika katika *Baraahin* hiyo hiyo kwamba Isa[as] atarudi tena duniai. Na kujumuika kwa mambo haya mawili yanayopinzana katika kitabu kimoja na kutodai kwangu kuwa Masihi Mau'udi kunalazimisha hakimu mwadilifu kwa kudhihirisha rai hii kwamba kwa hakika moyo wangu ulighafilikia wahyi huu wa Mungu uliopo katika *Baraahine Ahmadiyya* juu ya kuwa kwangu Masihi Mau'udi, kwa hiyo nikajumuisha mambo haya yanayopingana katika *Baraahin.*

Kama katika *Baraahine Ahmadiyya* ingekuwa kwamba Isa[as] yule yule atarudi tena duniani na isingekuwa habari yoyote kuhusu kuwa kwangu Masihi Mau'udi, hapo mwenye papara angeweza kujifaidisha kidogo kwa maneno hayo na angeweza kusema kwamba miaka kumi na miwili baada ya *Baraahine Ahmadiyya* kwa nini ikaachwa itikadi hiyo ya zamani. Ingawa kusema hivyo pia ingekuwa bure, kwani Manabii na wapokeaji wahyi huwa wadhamini wa ukweli wa wahyi tu; hawawezi kulaumiwa kwa maelezo yao kuwa ghalati na kinyume cha matukio; kwani, hayo ndiyo rai yao, si Neno la Mungu. Hata hivyo, watu wa kawaida waliweza kudanganywa, lakini sasa upinzani wa kipuuzi kama huo hauna nafasi wa kutiwa maanani, kwani katika *Baraahine Ahmadiyya* hiyo miaka kumi na miwili kabla ya kutoa madai nikaitwa sehemu nyingi Masihi Mau'udi, na kwa mwenye akili hii ni dalili bayana sana juu ya ukweli wangu.

Ilmuradi, katika *Baraahine Ahmadiyya* kutajwa kwa ujio wa mara ya pili wa Hadhrat Masihi[as] kuliweza kumdanganya mwenye akili ndogo kama isingekuwa imeelezwa chochote juu ya kuwa kwangu Masihi Mau'udi katika *Baraahine Ahmadiyya*, lakini kutajwa huko ilikuwa wazi kiasi hiki kwamba Masheikh wa Ludhiana, Muhammad, Abdul Aziz na Abdullah walileta kipingamizi katika zama hizo hizo kwamba mtu huyu

anajiita Isa na bishara zote zimhusuzo Isa anazinasibisha zote kwake; na jibu lake likatolewa na Maulawii Muhammad Husain katika maoni yake kwamba kipingamizi hiki ni bure kwani katika *Baraahin* hiyo hiyo imo ikrari pia ya ujio wa mara ya pili wa Hadhrat Isa[as].

Basi nashukuru juu ya mipango ya Mungu kwamba kwa njia nyepesi sana Alitayarisha mapema njia ya kuniondolea lawama katika *Baraahin*. Kama katika *Baraahine Ahmadiyya* isingetajwa kwa njia yoyote ujio wa mara ya pili wa Hadhrat Isa[as] na ingetajwa tu kuwa kwangu Masihi Mau'udi, hapo makelele yaliyopigwa baada miaka kadhaa na kutayarishwa fatwa za kukufurisha, makelele hayo yangepigwa wakati ule ule. Na kama katika *Baraahin* ungetajwa ujio wa mara ya pili wa Hadhrat Masihi[as] na zisingeandikwa humo funuo za kuwa kwangu Masihi Mau'udi, basi wapumbavu wangepata hoja kwamba katika *Baraahin* ulikubaliwa ujio wa mara ya pili wa Hadhrat Isa[as], basi kwa nini baada ya miaka kumi na miwili ukakanushwa ujio huo. Lakini, kwa upande mmoja kuniita kuwa Masihi Mau'udi katika *Baraahin* sawa na wahyi wa Mungu na kwa upande mwingine kinyume chake kutajwa kwa kalamu yangu kama itikadi ya kawaida ya ujio wa mara ya pili wa Masihi, ni jambo ambalo mwenye akili anaweza kuelewa kwalo kwamba huu ni mpango maalumu wa Mungu. Ilmuradi,

mpango wa Mungu ukaniacha kukosea kwamba nikataja katika kitabu hicho ujio wa mara ya pili wa Isa[as] ambamo ikatajwa kuwa kwangu Masihi Mau'udi, ukabainisha moyo wangu mweupe na kutozusha. Waila ilikuwa shaka gani kwamba funuo zile zote zilizoandikwa katika ***Baraahine Ahmadiyya*** zinazonifanya Masihi Mau'udi, zingechukuliwa kuwa uzushi; na akili ya kawaida haitakubali kwamba dai la kuwa Masihi Mau'udi lililotajwa baada ya miaka kumi na miwili likapangwa mapema muda kiasi hicho. Ilmuradi, katika kitabu hicho, ambamo imetajwa kuwa kwangu Masihi Mau'udi, mumo humo kutajwa pia ujio wa mara ya pili wa Hadhrat Isa[as], ni ushahidi mzima juu ya moyo wangu mweupe na kutozusha.

Ni sikitiko kwamba wapinzani wamepotewa na akili kiasi hiki kwamba wanashika sehemu moja ya kila jambo na kuacha ya pili. Wamtajapo Mkristo Atham hawataji kabisa sharti wala hawatamki kwa ulimi kufa kwake sawa na bishara na kuingia kaburini kulikobashiriwa mapema, na mambo yathibitishayo kwamba Atham akaacha kumwita Mtume Mtukufu[saw] dajali, hawataji kabisa matukio hayo. Hawathubutu hata kuashiria kwenye mambo hayo, wanamezea yote. Na wanapotaja mkwewe Ahmad Beg, kamwe hawawaambii watu kwamba sehemu moja ya bishara hii imeshatimia katika muda uliowekwa, yaani Ahmad Beg akafa ndani ya muda, na sehemu ya pili

inapaswa kusubiriwa. Pia hawasemi kwamba bishara ilikuwa kuhusu onyo na yenye sharti kama ufunuo تُوْبِيْ تُوْبِيْ فَإِنَّ الْبَلَاءَ عَلَىٰ عَقِبِكِ hudhihirisha uliochapwa mara kadha. Na ni dhahiri kwamba baada ya kifo kama hicho cha Ahmad Beg, kutishika ni jambo la asili. Basi kwa sababu ya hofu yao hiyo sehemu ya pili ikaahirika kutimia kama ilivyo suna ya Mugnu katika bishara za onyo. Lakini, wapinzani hao waovu hawataji kamwe mambo haya pia; na sawa na tabia ya Wayahudi, kwa kupotosha habari ilivyo wanaieleza namna ambayo kwayo watie wasiwasi katika mioyo ya majahili, bali watu hao wakawazidi hata Wayahudi. Kwani, watu hao huzusha kuhusu kila jambo kama vile Maulawii Thana'ullah akafanya hivyo katika mjadala wa huko *Mudd* na akidanganya akasema, angalieni mtu huyo katika bishara yake fulani akaandika kwamba mwana atazaliwa, lakini binti akazaliwa na baada yake mwana akazaliwa na akafa, na bishara ikabatilika.

Sasa, mtu awaulize hao kwamba ikiwa hamna hiana na uongo katika kauli yenu basi toeni ule ufunuo uliochapishwa Alimohabarisha Mungu kwamba lazima safari hii mvulana atazaliwa, au kwamba mwana atakayezaliwa baada ya binti ndiye mwana aliyeahidiwa sio mwingine. Hata kama tukifikiria kwamba labda mvulana huyu ndiye aliyeahidiwa, basi fikara yetu ni kitu gani usipokuwa wahyi dhahiri wa Mungu. Mtume

Mtukufu[saw] alifikiria kwamba atahamia Yamama, lakini fikara ile haikutokea sahihi na hatimaye akahamia Madina. Na kama ilikuwa ndani ya bishara kwamba lazima kwa himila ya kwanza tu atazaliwa mvulana huyo, basi maneno hayo yalitakiwa kuwepo katika wahyi wa Mungu, lakini je yeyote aweza kuonyesha kwamba kulikuwa na neno lolote kama hilo katika wahyi. Angalieni, kuhusu Mtume Mtukufu[saw], manabii wengi wa Kiisraeli walitoa bishara kwamba atazaliwa, lakini baada ya ujio wa manabii wengi mwisho wa wote Mtume Mtukufu[saw] akatumwa. Sasa, je mtu aweza kupinga kwamba bishara za manabii hao zilibatilika, kwani Mtume Mtukufu[saw] alizaliwa baada ya kupita miaka elfu mbili kamili baada ya Musa[as], ilihali sawa na bishara ya Torati, Wayahudi wakafikiri kwamba Nabii yule atazaliwa karibuni; lakini haikutokea hivyo, bali katikati wakaja Manabii kadha. Basi, upinzani kama huo huleta mjinga au mtu habithi wa hali ya juu asiye na hofu ya Mungu.

Maulawii Thana'ullah alitoa mambo hayo katika mjadala wa huko Mudd. Kwa sababu ya mambo hayo kila mcha Mungu anaweza kuelewa kwamba hali ya masheikh hao imefikia wapi. Kwa harara ya chuki hawazingatii njia ya unabii na kigezo kile kilichowekwa kwa kuwatambua Manabii, na kila upinzani wao unakuwa ni uongo mtupu na njama ya kishetani. Kama hao ni wakweli, basi kwa

kufika Qadian wathibitishe bishara yoyote kuwa batili. Na kwa kila bishara itatolewa zawadi ya rupia mia moja, na zaidi ya hii itatolewa nauli ya kuja na kurudi. Lakini kwa utafiti huu njia ya unabii iwe kigezo cha ukweli na uongo. Nasema kwa yakini kwamba kama miujiza yangu na bishara si sahihi kwao, basi watalazimika kukataa Manabii wote[as] na hatimaye watafia katika kufuru.

Ni sikitiko kwamba watu hao hawamwogopi Mungu. Wanayo marundo ya uchafu mfukoni mwao. Wanawafuata Wakristo na Wayahudi. Wakristo walikuwa wakisema, kama kwa Mtume Mtukufu[saw] ilikuwepo bishara ya ushindi katika Kurani Tukufu, kwa nini alipigana vita na kwa nini akawaua maadui kwa hila na mipango. Leo watu hao wanaleta upinzani wa aina hii. Mathalan, husema kwamba kwa ajili ya binti wa Ahmad Beg, kwa nini ilifanywa bidii kuwatuliza mioyo yao kwa njia mbalimbali, na kwa nini Ahmad Beg akaandikiwa barua kama hizo. Lakini ni sikitiko kwamba hao wawili, yaani Wakristo na hao Wayahudi wapya, hawaelewi kwamba kujibidiisha kwa kutimiza bishara haikuharamishwa. Mtu ambaye Mungu Anampasha habari kwamba mgonjwa fulani atapona, huyo hajakataliwa kwamba atumie dawa pia, kwani labda amekadiriwa kupona kwa kutumia dawa. Ilmuradi, kujaribu hivyo hakukukataliwa sawa na itikadi ya Wakristo na Wayahudi, wala katika Islam. Katika

mjadala huo wa Mudd, Maulawii Thana'ullah alileta upinzani huu pia kwamba haikutimia bishara iliyotolewa kuhusu dhila ya Muhammad Husain, Ja'far Zatalli na rafiki yake mwingine. Kama watu hao wasingeleta upinzani wa namna hii basi wangeshabihianaje na Wayahudi. Kwangu mimi ilikuwa lazima upinzani kama huo ungeletwa. Ee bwana katika muda wa kusikilizwa kesi hiyo maandishi ya Maulawii Muhammad Husain yalipokamatwa yaliyokuwa kinyume cha fatwa ya kukufurisha, je kwa kuangalia daraja ya utaalamu wake yeye hakudhalilika na kufedheheka? Yaani, kunikabili akaandika katika *Isha'atus-Sunnah* kwamba kumkana Mahdi Mau'udi ni kufuru, na akapiga kelele kwamba huyu mtu anapinga itikadi iliyokubaliwa ya Islam, na haki ni hii hii kwamba Mahdi Mau'udi atadhihiri na Masihi atashuka kutoka mbinguni. Kisha kwa kuifurahisha serikali akakanusha ujio wa Mahdi. Kijitabu chake kile kikakamatwa na dhidi yake ikatolewa pia fatwa ya kufuru ya ndugu zake. Sasa semeni, kwa kitendo hiki cha unafiki amepata heshima au dhila? Dhila siyo hii tu kwamba mtu apigwe viatu kichwani hadharani, bali mtu anayedai kuwa Maulawii na mcha Mungu, kama mwenendo wake wa unafiki ukithibitika, basi hakuna dhila kubwa zaidi kuliko hii kwa ajili yake. Hakuna dhalili zaidi kuliko

mnafiki, [6] إِنَّ الْمُنٰفِقِيْنَ فِي الدَّرْكِ الْاَسْفَلِ مِنَ النَّارِ . Ni kupata doa jeusi baya namna gani kueleza mbele ya watu kwamba ujio wa Mahdi ni haki na kumkana ni kufuru, na kwamba vita vitapiganwa sana, lakini kwa kuifurahisha serikali kusema kwamba hii yote ni uongo. Kama yeye bado hajadhalilika, basi tutalazimika kukiri kwamba heshima zenu ni imara zaidi hata kuliko jengo la zege kiasi hiki kwamba maovu ya aina yoyote hayazitilii tofauti yoyote. Kuhusu heshima ya Ja'far Zatalii, watu hao hawana uzito wowote, hao wote ni kivuli cha Maulawii Muhammad Husain, kwani yu wakili wao; dhila ya wakili wao ilipothibitika, je dhila yao bado imebaki. Kivuli daima hufuata asili yake; mti wenyewe ulipoanguka, kivuli kitawezaje kubaki! Kama mtu bado anashuku, basi kauli zote mbili za Maulaii Muhammad Husain ninazo. Kauli moja kwa kuwafurahisha watu na kauli ya pili kwa kuifurahisha serikali, azione mwenyewe kwa macho yake; kisha mwenyewe aamue kwa uadilifu kwamba akiitwa Maulawii na kuwa wakili wa wamwaminio Mungu Mmoja ametenda kazi hii ya unafiki. Je hii ndiyo sababu ya heshima au dhila?

[6] Bila shaka wanafiki wako katika daraja ya chini ya Moto. An-Nisaa 4:146

Tumeshaona Wayahudi katika zama hizi, nasi tumeamini kwamba aya غَيْرِ الْمَغْضُوْبِ عَلَيْهِمْ[7] iliashiria kwenye hii hii kwamba katika umati huu pia Wayahudi walioghadhibikiwa lazima watazaliwa, basi wameshazaliwa na bishara ya Mtume Mtukufu[saw] imeshatimia. Lakini je umati huu una bahati mbaya kiasi hiki kwamba katika takdiri yao iliandikwa kuwa Wayahudi tu! Hatuwezi kunasibisha kamwe amali hii kwa Mungu Karimu kwamba kwa kuwa Wayahudi waliolaaniwa uwe umati huu, na Masihi aje kutoka katika wana wa Israeli. Kwa jambo hili umati huu unafedheheka, na haupaswi kuitwa kuwa umati uliorehemiwa. Basi, kama inavyofahamika, umati huu kuwa Wayahudi kutokana na aya غَيْرِ الْمَغْضُوْبِ عَلَيْهِمْ hutaka kwamba Masihi aliyefika kwa kukabili Wayahudi walioghadhabikiwa, mfano wake pia aje kutoka katika umati huu huu. Kwenye hii hii, aya اِهْدِنَا الصِّرَاطَ الْمُسْتَقِيْمَ صِرَاطَ الَّذِيْنَ اَنْعَمْتَ عَلَيْهِمْ[8] inaashiria. Ni sikitiko kwamba Hadithi ile pia imetimia katika zama hizi iliyosema kwamba maulamaa wa zama za Masihi watakuwa waovu zaidi kuliko wote watakaokuwa wanakaa ardhini. Na tuwasikitikieje Wayahudi wa awali, hao walikuwa wakitoa Kitabu cha Mungu walipopinga ingawa hawakuelewa maana yake, lakini watu hawa wanaleta mambo yaliyozushwa. Na Wayahudi walikuwa na vipingamizi imara kuhusu hali ya Hadhrat Masihi[as] na

[7] Al-Faatiha 1:7

[8] Al-Faatiha 1:6-7

bishara zake kiasi hiki kwamba hata sisi pia tunaona vigumu kujibu, isipokuwa tu tuseme lazima Isa[as] alikuwa Nabii kwani Kurani inamwita Nabii. Na hakuna dalili yoyote inayoweza kuthibitisha unabii wake, bali hoja kadhaa zipo juu ya kubatilisha unabii wake. Hii ndiyo hisani ya Kurani juu yake kwamba imemwandika yeye pia ndani ya orodha ya Manabii. Ndiyo maana tumemwamini kwamba yu Nabii mkweli na mtukufu na ameepukana na tuhuma alizotiliwa yeye na mama yake. Yathibitika kutokana na Kurani Tukufu kwamba alituhumiwa kwa mambo mawili makubwa.

(1) Mosi, kuzaliwa kwake kumelaaniwa, Mungu Apishe mbali; yaani alizaliwa nje ya ndoa.

(2) Ya pili, kifo chake pia kimelaaniwa, kwani alikufa kwa kuwambwa msalabani. Na imeandikwa katika Torati kwamba mwanaharamu ni maluuni, hataingia kamwe Peponi wala hatanyanyuliwa kwa Mungu. Na kadhalika hii pia iliandikwa kwamba atundikwaye mtini, yaani atakayekufa msalabani, yeye pia amelaaniwa, naye pia hatanyanyuliwa kwa Mungu. Shutuma hizi mbili zilikuwa kali sana. Katika Kurani Tukufu, Mwenyezi Mungu Amejibu shutuma hizi mbili katika sehemu ile ile moja nayo ni hii: وَبِكُفْرِهِمْ وَقَوْلِهِمْ عَلٰى مَرْيَمَ بُهْتَانًا عَظِيْمًا وَّقَوْلِهِمْ اِنَّا قَتَلْنَا الْمَسِيْحَ عِيْسَى ابْنَ مَرْيَمَ رَسُوْلَ اللّٰهِ ۚ وَمَا قَتَلُوْهُ وَمَا صَلَبُوْهُ وَلٰكِنْ شُبِّهَ لَهُمْ[9] (juzuu 6, Sura An-Nisaa). Katika aya

[9] An-Nisaa 4:157-158

hii mna jibu la shutuma zote mbili. Na muhtasari wa aya ni hii kwamba Isa[as] hakuzaliwa kwa njia ya haramu wala hakufia msalabani, bali ikafahamika kwa kudanganyika kwamba ameshakufa. Hivyo yu mkubaliwa wa Mungu na ameshanyanyuliwa kwa Mungu kama Manabii wengine. Sasa, wako wapi masheikh wanaoufikisha mbinguni mwili wa Hadhrat Isa[as]? Hapa ugomvi wote ulikuwa kuhusu roho, usiohusikana na mwili.

Ilmuradi, Kurani Tukufu imemwita Hadhrat Masihi[as] kuwa mkweli. Lakini, twalazimika kusema kwa sikitiko kwamba Wayahudi wanavyo vipingamizi vikali kuhusu bishara zake ambavyo hatuwezi kuviondoa kwa njia yoyote. Kwa kutegemea Kurani tu tumeshamwamini na tumemkubali kwa moyo wa kweli, na bila hiyo hatuna dalili yoyote juu ya unabii wake. Wakristo wanalilia Uungu wake, lakini hapa hata Unabii wake hauwezi kuthibitika. Hae, tumpelekee nani huzuni hii kwamba bishara tatu za Bwana Yesu zikathibitika kuwa uongo waziwazi, na leo yupo nani ardhini awezaye kutatua tatizo hili. Ole wao, wanaufanya ukweli kuwa uongo. Ni fadhili kubwa juu ya Nabii wetu[saw]; mtu yule hataaibika mbele ya watu amfuataye kikweli Nabii huyu mpendwa. Niwaambie nini majahili hao na nitilieje upendo wa ukweli mioyoni mwao wanaozunguka kama waigaji, na kazi yao ni mzaha na dhihaka, na kufanya masihara ni

mwenendo wao. Mamia ya ishara zinang'aa kama jua, lakini kwao haijadhihiri ishara yoyote mpaka sasa. Nimesikia, bali nimeona maandishi ya Maulawii Thana'ullah wa Amritsar yaliyosainiwa naye anamoomba kwamba nataka kwa moyo uamuzi wa aina hii kwamba makundi mawili, yaani mimi na yeye, tuombe kwamba aliye mwongo kati yetu wawili afe katika uahi wa mkweli, na pia akadhihirisha matakwa yake kuandika kitabu mfano wa *I'jazul Masih*, chenye ufasaha na balagha ile ya *I'jazul Masih* na chenye makusudio hayo yake. Kama Maulawii Thana'ullah amedhihirisha matakwa haya kwa moyo, si kwa unafiki, basi kuna nini iliyo bora kuliko hii. Na atafanya hisani kubwa kwa umati huu katika zama hizi za mafarakano kwamba akiwa shujaa atafanya uamuzi kwa njia hizi mbili kati ya haki na batili. Hili ni pendekezo lake zuri; sasa ni afadhali akae imara juu yake.

Kama kadhabu mmoja aondoke duniani na watu wengine wapate kuongoka, basi afanyaye shindano kama hilo atapata malipo ya Nabii. Lakini kwa mubahala ya mauti kwa upande wetu hatuwezi kuita kwani mapatano na serikali yanatuzuia kutoa changamoto ya namna hii. Naam, Maulawii Thana'ullah na wapinzani wengine hawakukataliwa kutulazimisha kujibu changamoto kama hiyo; awe Maulawii Thana'ullah au Maulawii mwingine aliye miongoni mwa wajulikanao na awe ameheshimika

katika jama'at yake, ambaye watu waheshimiwa kwa uchache hamsini watoe ushahidi wa kuthibitisha kwenye kipeperushi cha tangazo lake. Na kwa vile Maulawii Thana'ullah sawa na maandishi yake, yupo tayari kwa changamoto kama hiyo, basi hatuna kipingamizi chochote kwamba atoe changamoto ya namna hii, bali ana ruhusa kwa upande wetu, kwani changamoto yake pekee inatosha kwa uamuzi. Lakini, litakuwa sharti kwamba kifo chochote kisitokee kwa kuuawa, bali kiwe kutokana na maradhi tu kwa mfano kwa tauni au kwa kipindupindu au kwa maradhi mengine yoyote ili kifo cha namna hii kisisababishe tashwishi kwa watawala, nasi tutaendelea kuomba pia kwamba makundi yote mawili wasalimike na kifo cha namna hii; mwongo apate kifo kile tu kinachotokea kwa maradhi; na kundi la pili pia litalazimika kushikamana na kanuni hiyo. Na ikumbukwe kwamba bishara yetu kuhusu mauaji ilikuwa bishara mahususi iliyohusu Lekhram, humo Mungu Akadhihirisha kwamba atakufa kwa kuuawa na ikatangazwa hivyo. Nami nafikiri, siri ya yeye kuuawa ilikuwa ni kuwa akamtukana vikali Nabii wetu[saw] na Manabii wote, na Mungu Akaona matusi yake yamefikia kileleni na katika kutusi hakumwacha Nabii yeyote. Hatimaye 'kisu' cha ulimi wake kikawa kisu hasa na kumwangukia. Na hii ilikuwa ishara kubwa mno; na ikatendeka dhambi hii kubwa ardhini kwamba bishara zinga'razo kama hizo zikakataliwa na watu waipendao dunia.

Hivyo, kama Maulawii Thana'ullah yupo tayari kwa changamoto ya aina hii, basi barua ya kimaandishi pekee haitatosha, bali anapaswa kutoa tangazo lililochapwa lielezalo kwamba mtu huyu (hapa aandike jina langu waziwazi) namwona yu kadhabu, dajali na kafiri na anayedai kuwa Masihi Mau'udi, mwenye kupokea ufunuo na wahyi, nami nina yakini kwamba yu mwongo katika madai haya. Na Ee Mungu, nakuomba kwamba kama itikadi yangu hii si sahihi na kama mtu huyu kwa kweli ni Masihi Mau'udi, na kwa kweli Isa[as] ameshafariki, basi nifishe kabla ya kifo cha mtu huyu. Na kama mimi ni mkweli katika itikadi hii na mtu huyu kwa hakika ni dajali, asiye na imani, kafiri na muritadi, na Hadhrat Masihi[as] yupo mzima mbinguni atakayekuja wakati fulani usiojulikana, basi mhilikishe mtu huyu ili fitina na mafarakano yafutike na Islam isipate madhara kutoka kwa dajali mmoja, mpotoshaji, na aongozaye vibaya. Amin tena Amin.

Hapo kabla, mubahala wa aina hii ameishafanya Maulawii Ghulam Dastgir Kasuri pia kwenye uk. 27 wa kitabu chake *Fat'he Rahmani* na siku chache tu baada yake katika uhai wangu akaingia kaburini, na akathibitisha ukweli wangu kwa kufa kwake. Lakini, Maulawii Thana'ullah akitaka, basi ajaribu mwenyewe, anahusikanaje na

Ghulam Dastgir, kwani yeye mwenyewe anadhihirisha utayari pia kwa ajili hii.

Changamoto hii iliyo kwa kweli ni mubahala, italazimika kuiandika neno kwa neno namna niliyotaja hapo juu, pasipo kupunguza wala kuongeza hata neno moja. Na kama yakitakiwa mabadiliko yoyote maalumu, basi yataamuliwa kwa kupitia barua za binafsi. Kisha tangazo hili la mubahala latakiwa kutiliwa saini, kwa akali, za waheshimiwa hamsini, na yatakiwa angalau nakala mia saba za tangazo hili zienezwe nchini, na nakala ishirini za tangazo nipostiwe kwa rejista.

Sina haja kumtupia changamoto ya *mubahala* au nifanye mubahala dhidi yake. Mubahala wake aliodhihirisha utayari wake unatosha kwa ukweli wangu. Kwani, Mwenyezi Mungu tangu zama za *Baraahine Ahmadiyya*, ambacho miaka ishirini na mitatu imeshapita tangu kichapishwe, Amedumisha ishara hii kwa ajili yangu. Nakiri kwamba nikishindwa katika ushindani huu, basi Jumuiya yangu wanaozidi laki moja hivi sasa wanapaswa wote waachane nami kwa kuchoka, kwani Mungu Akinithibitisha kuwa mwongo Amenihilikisha basi sitaki uongozi na uimamu katika hali ya kuwa mwongo, bali katika hali hii nitakuwa mbaya zaidi kuliko Myahudi na kuwa mahali pa aibu na ari kwa kila mtu.

Na mtu atakayeondoa fitina kwa changamoto kama hii, sharti athibitike kuwa mkweli, jina lake litabaki duniani kwa heshima kubwa. Na mtu atakayekuwa dajali, laghai na mzushi, kwa kifo chake dunia itapata raha sawa na usemi huu mashuhuri 'Taka katoweka, dunia katakasika'. Niandike nini zaidi ya hayo. Na ikiwa jambo fulani la lazima nimelisahau unalolihitaji uadilifu, basi niarifiwe nitalikubali kwa furaha sharti lisiwe la upuuzi na lisiwe na mnuko wa hila na ulaghai, na liwe kwa sababu ya takwa, sio kama ujanja wa watu wa kidunia. Na Mwenyezi Mungu Hujua kwamba nataka haki idhihirike kwa njia yoyote iwayo. Ingawa naona ishara za Mungu kama mtu analiona jua, nami naamini wahyi huu wa Mungu kama niaminivyo Kurani Tukufu, lakini nataka hoja ikamilike juu ya mkanaji kwa kila jiha. Ee Allah, unaona shughuli zetu, Unajua yaliyomo mioyoni mwetu, na kwa macho Yako makali siri zetu hazifichikani, basi uamue baina yetu na wapinzani wetu; na aliye mkweli machoni pako usimwangamize, kwani kwa kumwangamiza mkweli, watu wengi wataangamia. Ee Mungu wangu Mweza, sogea karibu Ukajikalie kiti chako cha adili na kumaliza mabishano haya ya kila siku. Ndimi zetu zi mbele ya watu, na uhakika wa mioyo yetu upo wazi kwako. Nisemeje na moyo wangu ukubalije kwamba utaingiza mkweli kaburini kwa dhila. Wenye maisha ya maovu watashindaje! Naapa kwa Dhati yako kwamba hutafanya

hivyo kamwe. Na kadiri Maulawii Thana'ullah aliyonifedhehesha kwa shutuma kinyume cha hakika na kwa viapo vya uwongo katika mkutano wa kijijini Mudd, malalamiko yangu yote ni mbele ya Mwenyezi Mungu, nami sihuzuniki kukadhibishwa huku. Kwani, wanapomwita Hadhrat Isa[as] pia kadhabu, basi kama wakiniita mimi pia kadhabu, tuwasikitikieje! Kwani, wasema kwamba Mungu alipomwuliza je wewe ulisema niamininini mimi na mama yangu kwa Mungu, Isa akaongopa, yaani akatoa jibu lililokuwa uongo mtupu. Kwani, akasema kwamba mpaka nilipokuwa kati ya umati wangu nilikuwa shahidi juu yao na uliponifisha ukawa mchungaji wao; sijui wakafanya nini nyuma yangu. Na ni dhahiri kwamba nani anaweza kuwa kadhabu mkubwa kuliko yule atakayesema uongo mbele ya Mungu Atakapoketi siku ya Kiama kwenye Kiti cha uadilifu! Je utakuwa uongo mbaya zaidi kuliko huu kwamba mtu atakayekuja mara ya pili duniani kabla ya Kiama na atakaa duniani miaka arobaini na atapigana na Wakristo na kuvunja misalaba na kuua nguruwe na kuwasilimisha Manasara wote, yeye mtu huyo huyo siku ya Kiama atasema, akikanusha matukio haya yote, kwamba sina habari ikatendeka nini nyuma yangu. Na hivyo ataongopa mbele ya Mungu na atadhihirisha kwamba sina habari ya hali ya Wakristo na ya dini yao tangu wakati ule uliponifisha. Angalieni, huu ni uongo mchafu namna gani

tena mbele ya Mungu; basi je Hadhrat Masihi[as] anakuwa kadhabu au la? Fungueni Kurani Tukufu na someni aya فَلَمَّا تَوَفَّيْتَنِىْ kisha semeni, je mmemchukulia Isa[as] kuwa kadhabu au la!

Lakini, tuisikitikieje hii, kwani kwenu Mungu pia ni mwongo. Mwenyezi Mungu Akaeleza bayana kifo cha Isa[as] katika aya فَلَمَّا تَوَفَّيْتَنِىْ[10], na kwa uwazi Akaeleza udhuru huu wa Hadhrat Isa[as] kwamba baada ya kifo chake watu hao wamepotea. Basi, Mungu Anafahamisha kwamba ikiwa Hadhrat Isa[as] hajafa, basi Wakristo pia mpaka sasa hawajapotea, kwani kushikamana kwa Wakristo na njia iliyonyooka ikaambatanishwa na uhai wake tu. Na alama ya upotevu wa Wakristo ikawekwa kuwa ni kifo cha Hadhrat Isa[as]. Sasa semeni, katika hali hii, kwenu Mungu Awezaje kuwa mkweli ambaye kauli yake haikukubaliwa.

Na kadhalika katika aya وَ مَا مُحَمَّدٌ اِلَّا رَسُوْلٌ ۚ قَدْ خَلَتْ مِنْ قَبْلِهِ الرُّسُلُ[11] Mungu Alidhihirisha kifo cha Manabii wote kwa neno moja lihusikanalo na kifo cha Manabii wote, na kwa Hadhrat Isa[as] halikutumika neno lolote mahususi. Mungu Apishe mbali, kwenu hii pia ni uongo wa Mungu. Aya hii ndiyo ambayo kwa kuisoma Hadhrat Abu Bakr[ra]

---

[10] Al-Maaida 5:118

[11] Aali 'Imraan 3:145

alithibitisha kifo cha Mtume Mtukufu[saw]. Mantiki hii ya Abu Bakr[ra] pia ilikuwa ni ya ajabu kwamba licha ya Isa[as] kukaa mzima mbinguni, anasoma aya hii mbele ya watu; anawapa utuvu wa aina gani? Je hajui kwamba Isa[as] yupo mzima mbinguni na atakuja tena na atakaa duniani kwa miaka arobaini. Isa[as] ana umri ule mrefu na Mbora wa Manabii[saw] ana umri huu mdogo. [12] تِلْكَ إِذًا قِسْمَةٌ ضِيزَىٰ

Na Masahaba pia walikuwa watu wa ufahamu wa ajabu ambao wakisikia tu aya hii wakanyamaa, na hakuna aliyemjibu Abu Bakr[ra] kwamba mheshimiwa, unasoma aya hii ya aina gani inayotuongezea majuto; Isa[as] yupo mzima mbinguni na atakuja tena, lakini Nabii[saw] wetu mpendwa ameachana nasi kwa kudumu. Kama Isa[as] yupo nje ya kanuni hii ya Mungu na ni mwenye kupata umri wa mika elfu nyingi na atakuja tena, kwani nini basi Nabii[saw] wetu hakujaliwa neema hii? Na ukweli ndio huu kwamba Abu Bakr[ra] na Masahaba wote waliokuwepo wakati huo na hakuna hata mmoja asiyekuwepo miongoni mwao, wakaelewa maana hii hii ya aya hii kwamba Manabii wote wameshafariki. Na inaonekana kwamba mmoja au wawili kati ya Masahaba wasiokuwa na ujuzi sana wakisikia kauli za Wakristo waishio pembezoni mwao walikuwa na dhana hii kwamba Isa[as] yupo mzima mbinguni, kama vile Abu Hurairara aliyekuwa na uelewa mdogo na hakuwa na

[12] Huo tena ni mgawanyo mbaya sana. An-Najm 53:23

ujuzi sana. Lakini Abu Bakr[ra] ambaye Mungu Akamjalia elimu ya Kurani, aliposoma aya hii, ndipo Masahaba wote wakathibitikiwa kifo cha Manabii wote na wakafurahia sana aya hii, na huzuni yao waliyopata moyoni kwa kifo cha Mtume[saw] mpendwa ikaondoka na wakawa wanaendelea kusoma aya hii katika mitaa ya Madina. Kuhusu tukio hilo, Hassaan bin Thabitra akatunga beti hizi za kueleza huzuni alipofariki Mtume Mtukufu[saw]. Beti zenyewe ni hizi:

كُنْتَ السَّوَادَ لِنَاظِرِيْ فَعَمِيْ عَلَيْكَ النَّاظِرُ
مَنْ شَاءَ بَعْدَكَ فَلْيَمُتْ فَعَلَيْكَ كُنْتُ اُحَاذِرُ

Yaani, ewe Nabii[saw] ulikuwa mboni ya macho yangu nimepofuka kwa kuondoka kwako. Sasa afe yeyote awe Isa[as] au Musa[as], nilihofia kifo chako tu, yaani kwa kifo chako tumeyakini kwamba Manabii wengine wote wameshafariki, hatuwajali. **Mshororo**:

عجب تھا عشق اس دل میں، محبت ہو تو ایسی ہو

Upendo wa ajabu ulikuwemo moyoni humu; kama iwe huba, basi na iwe kama hii.

Kisha mnamkadhibisha Mwenyezi Mungu hivi kwamba Mungu Anasema baada ya tukio la msalaba tukawapa Isa[as] na mamake kimbilio mlimani palipopita maji safi, yaani chemchemi zilitiririka, penye starehe sana na palikuwa ni mfano wa  Pepo, jinsi  Anavyosema Mungu

وَ اٰوَيۡنٰهُمَاۤ اِلٰى رَبۡوَةٍ ذَاتِ قَرَارٍ وَّ مَعِيۡنٍ[13]. Yaani, baada ya tukio la msalaba lililokuwa mkasa mkubwa, Tulimpa Isa na mamaye kimbilio pale palipoinuka sana penye starehe fika na maji matamu, tangu, yaani nchi ya Kashmir. Sasa, ikiwa mnajua Kiarabu kidogo basi mnaweza kuelewa kwamba neno اٰوٰى hutumika wakati wa kutolewa kimbilio kwa kuokoa katika msiba fulani. Usemi huu umetumika katika Kurani Tukufu nzima na katika kauli za Waarabu na katika Hadithi. Na yathibitika kwa Neno la Mwenyezi Mungu kwamba Hadhrat Isa[as] alipatwa na msiba wa msalaba tu katika maisha yake yote. Na huthibitika kutokana na Hadithi kwamba Mariamu akapatwa na huzuni kali katika maisha yake yote kwa tukio hili tu. Basi, aya hii inatangaza kwa sauti kubwa kwamba baada ya tukio la msalaba Mwenyezi Mungu Akimwokoa Hadhrat Isa[as] katika maafa hayo Akamfikisha kwenye nchi nyingine kutoka nchi hii yenye kuudhi, palipotiririka chemchemi za maji safi na sehemu hiyo ilikuwa imeinuka. Sasa lipo swali kwamba je huko mbinguni pia kuna mlima wenye chemchemi ambapo Mwenyezi Mungu Akamkalisha Hadhrat Masihi[as]. Na kwa kuchunguza historia ya maisha ya Hadhrat Masihi toeni mfano wowtoe kwamba baada ya shida yoyote Mwenyezi Mungu Akapeleka katika nchi yenye starehe, iliyo mfano

[13] Al-Mu'minuun 23:51

wa Pepo na ndio mlima mrefu zaidi duniani kwenda juu na zinapotiririka chemchemi. Basi, sawa na mawazo yenu, Mungu Apishe mbali, Mungu Anaonekana mwongo waziwazi kwamba Anataja mlima baada ya tukio la msalaba Alipomkalisha Isa[as] na mamake, nanyi bila sababu mnampandisha mbinguni tena bure kabisa. Ebu, semeni kwamba akiwa Nabii kwa nini amekaa pasipo kutimiza jukumu lake kwa muda mrefu? Kisha nyinyi na Maulawii Thana'ullah mkikanusha aya hii mnamfikishia mbingu ya pili na hamwezi kujibu swali hili kwamba kwa nini mtu mzima akaenda kukaa pamoja na roho za wafu. Watu hao wameshaiaga dunia hii na wameshafika ahera; je yeye naye pia ameshafika ahera?

Na huu pia ni uongo dhidi ya Mungu kana kwamba Hakuelewa matilaba ya Wayahudi na Akaifanya methali hii '*Swali tofauti na jawabu potofu*' iafikiane Naye. Wayahudi walisema, roho ya Masihi haikupaa kwa Mungu, na Mungu Akawajibu kwamba nimemnyanyua mzima kwa mwili kwenye mbingu ya pili, na Nitamfisha wakati fulani. Ni jibu gani hili! Swali lilikuwa kwamba baada ya kufa Isa[as] hakunyanyuliwa na – Mungu Apishe mbali – yeye amelaaniwa. Jibu la swali hili lilikuwa hili kwamba bado Isa[as] hajafa, atakapofariki nitanyanyua

kwangu roho yake.[14] Jibu hili potofu lililotolewa halihusikani hata kidogo na jambo lililobishaniwa. Kadhalika kumhusu Mtume Mtukufu[saw] mna dhana aliongopa kwa kusema kwamba nimemwona Isa[as] katika roho za wafu walioishaenda nje ya dunia hii. Mtu mwenye mwili amekaaje pamoja na roho, na bila kufa amefikaje huko ahera? Imani hii ni ya kushangaza kwamba Mungu Ameshuhudia kwa kauli yake kwamba Isa[as] ameshafariki, ushahidi huo hawakukubali. Kisha, Mtume Mtukufu[saw] kwa feli yake, yaani kwa kuona, akashuhudia kwamba nimeshamwona katika roho za wafu; ushahidi huo nao unakataliwa, kisha kudai Islam na kugamba kuwa *Ahle Hadithi*! Katika usiku wa Mi'raji, Mtume Mtukufu[saw] hakuongea na Isa[as]; lakini akaongea na Musa[as] na imo katika Kurani Tukufu kwamba usiwe na shaka katika kuonana na Musa[as]. Basi, huu ni uongo wa aina gani waliotuhumiwa nao wote wawili, Mungu na Mtume[saw].

---

[14] Wayahudi hawakuwa na habari ya kuzimia kwa Hadhrat Masihi[as]. Shaka hii hii ndiyo waliyotiliwa. Kwa vile walidhani kwamba Isa[as] ameshakufa msalabani, kwa hiyo hawakukubali kunyanyuliwa kwake kiroho, na hawajakubali mpaka sasa. Kwao jambo la kubishaniwa lilikuwa kunyanyuliwa kiroho tu, kwani kwao kunyanyuliwa kimwili sio msingi wa wokovu. Mwandishi

Kisha wanasema, ipo kuhusu Isa[as] kwamba اِنَّهٗ لَعِلۡمٌ لِّلسَّاعَةِ[15] . Watu wenye elimu hii ya Kurani, yapasa kujitahadharisha nao, kwani 'نیم ملا خطرہ ایمان' [Sheikh nusunusu ni hatari kwa imani]. Enyi watu, je Mtume Mtukufu[saw] siye عِلۡمٌ لِلسَّاعَةِ[16] aliyesema بُعِثْتُ اَنَا وَ السَّاعَةُ كَهَاتَيْنِ ; na Mungu Akasema: اِقْتَرَبَتِ السَّاعَةُ وَ انْشَقَّ الْقَمَرُ[17] . Huu ni ujinga unukao sana kwamba wanafikiri maana ya neno 'Saa' hapo ni Kiama. Sasa fahamuni kutoka kwangu kwamba hapo maana ya 'Saa' ni adhabu ile iliyowashukia Wayahudi baada ya Hadhrat Isa[as] kwa mkono wa Tito wa Roma, na Mwenyezi Mungu Mwenyewe katika Sura Banii Israaiil ya Kurani Tukufu Ametoa habari ya 'Saa' hii. Maelezo ya aya hii hii yapo katika aya hii: مَثَلًا لِّبَنِیۡۤ اِسۡرَآءِیۡلَ[18] . Yaani, katika zama za Isa[as], Wayahudi wakapewa mfano ya Kiama kwa njia ya adhabu kali; na hiyo ikawa 'Saa' kwao. Sawa na usemi wa Kurani 'Saa' ni adhabu. Basi, ikahabarishwa kwamba 'Saa' hii itawashukia Wayahudi kwa sababu ya kumkana Hadhrat Isa[as]. Na ishara hiyo ikatokea, na 'Saa' ile ikawashukia Wayahudi. Na vilevile katika zama zile tauni kali pia ikawasibu, na kwa hakika tukio hilo lilikuwa Kiama kwao

---

[15] Lakini kwa yakini yeye ni elimu ya Saa ile. Az-Zukhruf 43:62

[16] Nimetumwa mimi na 'Saa' kama hivi viwili – na akaashiria kwenye kidole cha kati na cha Shahada. Mwenezi.

[17] Saa imekaribia na mwezi umepasuka. Al-Qamar 54:2

[18] Methali kwa wana wa Israeli. Az-Zukhruf 43:60

ambapo malaki ya Wayahudi wakaangamia, na maelfu wakafa kwa tauni na waliobaki wakatawanyika wakidhalilika sana. Kiama Kikuu (قِيَامَة كُبْرٰى) kitakuwa Kiama kwa watu wote, lakini hiki kilikuwa Kiama kwa Wayahudi hasa. Karina nyingine juu yake imo katika Kurani Tukufu kwamba Mwenyezi Mungu Anasema kwamba وَ اِنَّهٗ لَعِلْمٌ لِّلسَّاعَةِ فَلَا تَمْتَرُنَّ بِهَا[19] Yaani, Enyi Wayahudi, kwa Isa[as] mtatambua Kiama ni kitu gani, mithili Yake mtapewa, yaani مَثَلًا لِّبَنِيْٓ اِسْرَآءِيْلَ[20], Kiama kile kitawafikieni, msiwe na shaka ndani yake. Ni dhahiri kwamba Kiama hasa ambacho bado hakijatokea, kuhusu hicho haikufaa kuwa Mungu Angesema msiwe na shaka juu ya Kiama hicho nanyi mtakiona. Wayahudi wote wa zama zile wameshakufa na Kiama kijacho hawakukiona. Je Mungu Alisema uongo? Naam, Kiama cha Tito wakakiona. Basi, Kiama hicho ni Kiama kile walichoona Wayahudi kwa mkono wa Tito wa Roma katika zama za Hadhrat Masihi[as], kisha kwa sura ya tauni wakakiona. Ahadi hii ya zamani ya adhabu iliendelea ndani ya Vitabu vya Mungu inayotajwa sehemu mbalimbali katika Biblia. Kwa ajili yake katika Kurani Tukufu aya maalumu ilishuka. Ahadi hiyo imo katika Kurani Tukufu na katika vitabu vya kale na kwa hiyo hiyo Wayahudi

[19] Lakini kwa yakini yeye ni elimu ya Saa ile. Kwa hiyo msiifanyie shaka. Az-Zukhruf 43:62

[20] Methali kwa wana wa Israeli. Az-Zukhruf 43:60

walitanabahishwa, waila nani anakiogopa Kiama kilicho mbali. Je masheikh wa zama hizi wanakiogopa Kiama kile; la hasha! Na kama nilivyoeleza sasa hivi, neno hili la 'Saa' halihusikani na Kiama tu wala Kurani haikuliambatanisha na Kiama pekee. Ni sikitiko kwamba masheikh wenye ujuzi kidogo ambao mwisho wao ni mbaya kwa ujahili wao wanatoa tafsiri ambayo kwayo maana halisi inapotea. Wayahudi walikuwa na hofu gani ya Kiama cha mwisho, lakini bishara ya adhabu ya karibu bila shaka ilikuwa inaathiri mioyo yao.

Ni sikitiko kwamba masheikh wa kawaida wanaojikalia chumbani mwa msikiti tu mtazamo wao ni finyu wasijue 'Saa' hiyo iliahidiwa katika Vitabu vya zamani, iliyowashukia Wayahudi katika enzi ya Tito. Na Kurani Tukufu inasema waziwazi kwamba wakalaaniwa kwa ulimi wa Isa[as]; na kueleza tukio la adhabu kali kwa neno la 'Saa' sio usemi wa Kurani Tukufu tu, bali usemi huo umo katika Vitabu vya zamani vya kimbingu na unakithiri humo. Basi, haijulikani masheikh hao wa kawaida wamesikia kutoka wapi na kwa nani kwamba neno 'Saa' daima hutumika kwa Kima tu. Ni sikitiko kwamba watu hao wamekuwa kama mahayawani. Kwa kila hatua wanadhalilika kwa makosa yao, hata hivyo hawaachani na makosa. Je upo mpaka pia wa makosa! Watu hao hawaelewi kabisa matakwa ya Kurani. Wakampandisha

Hadhrat Isa[as] mzima mbinguni kwa mwili lakini lawama iliyokuwa ya Wayahudi hawakuijibu kabisa. Hii Aliyosema Mungu kwamba Wayahudi walisema إِنَّا قَتَلْنَا الْمَسِيحَ عِيسَى ابْنَ مَرْيَمَ[21] , na Akajibu kwamba hapana, bali Tukamnyanyua, hii ilikuwa ni jibu la jambo gani? Je, la kuuawa tu?

Basi, sikilizeni, kwa kupiga makelele kwamba tumeshamfisha Isa msalabani, Wayahudi hao walimaanisha kwamba yu mlaaniwa, na roho yake haikunyanyuliwa kwa Mungu jinsi roho ya Musa[as] na Adamu[as] ilivyonyanyuliwa. Basi, jibu la Mungu lilitakiwa kuwa 'Hapana, kwa hakika roho yake ilinyanyuliwa. Kunyanyua mwili mbinguni au kutonyanyua halikuwa ni jambo la kubishaniwa. Kwa hiyo – Mungu Apishe mbali – ufahamu huu wa Mungu ni wa ajabu kwamba iliyokataliwa ni kunyanuliwa roho kwa Mungu, lakini Mungu Anajibu ukinzani huu kwamba Nimemkalisha Isa[as] akiwa hai kwa mwili wake kwenye mbingu ya pili. Ni jibu la ajabu, na bado imebakia kufa na kuchukuliwa roho! Mungu Ajua roho itanyanyuliwa au hapana – jambo lenyewe lililobishaniwa.

Kadhalika watu hao wenye akili ndogo, wakikisia moyoni mwao kubatilika kwa baadhi ya bishara zangu wanasema hii pia kwamba kama baadhi ya bishara zimebatilika au kuna kosa la kufafanua maana ya ufunuo, basi madai ya

---

[21] An-Nisaa 4:158

Umasihi yategemeweje, labda haya pia ni ghalati. Jibu lake la kwanza ni hili kwamba لَعْنَةُ اللهِ عَلَى الْكَاذِبِيْنَ[22] . Na Maulawii Thana'ullah alisema hii tu wakati wa mjadala wa kijijini Mudd kwamba bishara zote zimebatilika. Kwa hiyo twawakaribisha na kusema kwa jina la Mungu kwamba waje Qadian kwa kutafiti na wapeleleze bishara zote. Nasi twaahidi kwa kuapa kwamba kwa kila bishara itakayothibitika uongo sawa na njia ya unabii tutawakabidhi rupia mia moja, waila 'nishani' maalumu ya laani itadumu kubaki shingoni mwao. Tutawalipia matumizi pia ya kuja na kurudi. Na bishara zote zitatakiwa kupelelezwa ili ubishi wowote usibaki kwa siku zijazo. Na kwa sharti hili tu rupia zitatolewa na kuthibitisha kutakuwa ni jukumu letu.

Ikumbukwe, katika kijitabu *Nuzuulul Masihi* nimeandika bishara mia na hamsini; yaani hizo zikithibitika kubatilika, basi Maulawii Thana'ullah atachukua rupia elfu kumi na tano na atasalimika na kuomba-omba mlangoni pa watu; bali tutamwambia bishara zingine pia pamoja na uthibitisho, na sawa na ahadi hiyo tutaendelea kumpa rupia mia kwa kila bishara. Hivi sasa idadi ya Jumuiya yangu ni zaidi ya laki moja. Basi, kama kwa ajili ya Maulawii huyo nikichukua rupia moja moja kutoka kwa kila mwanajumuiya, zitakuwa rupia laki moja, zote

[22] Laana ya Mungu iwe juu ya waongo.

atapatiwa ilhali yuahangaikia kila mlango kwa Anna mbili mbili. Na imeshuka ghadhabu ya Mungu, na anategemea sanda za wafu au hela za kutoa mawaidha. Kupata rupia laki moja ni kama Pepo kwake lakini asipozingatia niliyoeleza, asije Qadian kwa utafiti huu sawa na masharti yaliyotajwa ambamo yamo masharti mawili – kuthibitisha ukweli au kukadhibisha, basi yalaaniwe majivuno aliyofanya kijijini Mudd ndani ya mjadala na akasema uongo kwa ukavu wa macho. Mwenyezi Mungu Anasema لَا تَقْفُ مَا لَيْسَ لَكَ بِهٖ عِلْمٌ[23] . Lakini, bila elimu na utafiti kamili akakadhibisha hadharani; je, huu ni uaminifu? Mtu yule ni mbaya zaidi kuliko mbwa anayebweka bila sababu, na maisha yale yamelaaniwa yanayopita kwa upujufu.

Na baadhi ya watu wanadhani kwamba kwa kuelewa visivyo ufunuo fulani, amani inatoweka na shaka inaingia kwamba pengine Nabii au Mtume au *Muhaddathi* amedanganyika kuhusu madai yake pia. Dhana hii ni potofu kabisa. Na watu walio wazimu kidogo hunena hivyo. Na ikiwa wanayo itikadi hiyo, basi wanapaswa kuachana na unabii wa Manabii wote, kwani hakuna Nabii asiyekosea wakati fulani kuelewa ufunuo. Mathalan, Hadhrat Masihi[as] aliyefanywa Mungu, bishara zake nyingi zina makosa; kwa mfano, kudai kwamba nitapewa kiti cha ufalme cha Daudi. Akadai hivyo kwa sababu ya

---

[23] Wala usifuate usiyo na elimu nayo. Banii Israaiil 17:37

kutegemea ufunuo aliofunuliwa kwa kifupi akadhani kwamba nitakuwa mfalme. Alikuwa katika kizazi cha Daudi, na kwa kusema alikuwa mwana mfalme. Kutokana na sentensi hii inaonekana alitamani sana kiti cha kifalme na ufalme; na Wayahudi nao pia walikuwa wakisubiri azaliwe kati yao atakayeanzisha ufalme wao tena na kuwaokoa katika utawala wa Warumi.

Basi, kwa hakika dai kama hili kwamba ufalme wa Daudi utaletwa tena lilikuwa ni matakwa hasa ya Wayahudi; na mwanzoni kwa kufurahia jambo hili Wayahudi wengi walijumuika naye. Lakini, baadaye kwa sababu ya mambo kadha Wayahudi wakaelewa kwamba mtu huyu hana bahati kama hii, basi wakajitenga naye. Na baadhi ya wakorofi wakapeleka taarifa hii kwa Gavana wa serikali ya Kirumi pia kwamba mtu huyu anadai kiti cha enzi cha Daudi, ndipo haraka sana Hadhrat Masihi akageuka na akasema, ufalme wangu ni wa kimbingu si wa kidunia. Lakini, Wayahudi bado wanapinga kwamba ikiwa ufalme ulikuwa wa kimbingu, kwa nini akawaamuru wanafunzi wake, uzeni nguo zenu mkanunue silaha. Basi, hakuna shaka kwamba Hadhrat Masihi akakosea kuelewa ufunuo, yumkini huu uwe wasiwasi wa kishetani, ambao baadaye akaachana nao, kwani Manabii hawaachwi kubaki katika makosa. Na nimeandika 'wasiwasi ya kishetani', sawa na maneno ya Injili tu, kwani inathibitika kutokana na Injili

kwamba mara moja moja Masihi alikuwa akipata funuo za kishetani pia,[24] lakini alikuwa akitupilia mbali funuo zile na Mwenyezi Mungu Alikuwa Akimlinda na kuguswa na shetani, na sifa zake hizi zimeandikwa katika Hadithi za Islam na daima akasalimika, kamwe hakufuata shetani.

Myahudi fulani mkorofi anaandika katika kitabu chake kwamba safari moja Masihi akapatwa na mapenzi ya mwanamke mgeni, lakini kauli ya adui haitegemewi.[25] Yeye alikuwa mkubaliwa na mpendwa wa Mungu; ni mahabithi wanaomtuhumu. Naam, kwa kuelewa ufunuo visivyo alitamani kiti cha enzi cha Daudi, lakini hayakutimia matamanio yake; na sawa na methali maarufu بن مانگے موتی ملیں، مانگے ملے نہ بھیک [Utazipata lulu pasi kuomba, na kwa kuomba hata sadaka utakosa kupata], alikosa kiti cha enzi cha Daudi. Lakini yule Mteule[saw] wa Mungu, Mkuu wa Mitume aliyejitenga na ufalme wa kidunia na kusema اَلْفَقْرُ فَخْرِیْ , yaani umaskini ni fahari yangu, Mungu Akamjalia ufalme. Akasema, daima nataka kukaa na njaa siku moja na keshoye kula, lakini Mungu Akamlinda na njaa na umaskini. Hii ni fadhili mahususi.

---

[24] Tanbihi: Mapadri watatu Wajerumani wamefasiri hivyo maongezi ya shetani yaliyotajwa katika Injili. Mwandishi

[25] Tanbihi: Wakristo pia wanapayuka hivyo dhidi ya Mtume Mtukufu[saw] na safari moja Hadhrat Musa[as] pia akatuhumiwa hivyo. Mwandishi

*Ijtihadi* nyingi za Hadhrat Masihi zilithibitika batili; labda sababu yake ilikuwa kwamba mwanzoni matakwa yake hayakuweza kutimia. Ilmuradi, mambo hayo hayakuleta hitilafu katika Unabii. Nabii huwa na mamia ya nuru pamoja naye ambazo kwazo anatambulikana na ukweli wa madai yake hudhihirika. Basi, kama *ijtihadi* yake fulani si sawa, hii haileti tofauti ndani ya madai yenyewe. Mathalani, macho yakimfikiria mtu kuwa fahali, hatuwezi kusema kwamba hakuna faida ya kuwepo macho, au kuona kwake hakutegemewi. Basi, kwa Nabii mfano wa madai na mafundisho yake ni kama macho yavionavyo vitu vilivyo karibu, na hayakosei. Na mfano wa kukosea katika baadhi ya mambo ya *ijtihadi* ni kama macho yavionavyo vitu vya mbali, basi baadhi ya wakati yanakosea kuvitambua. Ndiyo sababu twaweza kusema kwamba kwa kuwa fikara aliyokuwa nayo Hadhrat Isa[as] kwa wema wa Wayahudi, yeye akafikiria kupata ufalme wake. Kwa hiyo, sawa na aya tukufu إِلَّآ إِذَا تَمَنَّىٰٓ أَلْقَى ٱلشَّيْطَٰنُ فِىٓ أُمْنِيَّتِهِۦ[26] shetani akamdanganya na akamtilia moyoni tamaa ya kiti cha enzi cha Daudi. Lakini, kwa kuwa alikuwa mkaribishwa na mpendwa wa Mungu, kwa hiyo wasiwasi wa kishetani haukuweza kubaki na haraka akaelewa kwamba ufalme wangu ni wa kimbingu si wa ardhi.

---

[26] Ila anapotamani, Shetani anatia (fitina) katika tamanio lake. Al-Hajj 22:53

Ilmuradi, *ijtihadi* hii ya Hadhrat Masihi ikawa batili. Wahyi wenyewe ulikuwa sahihi, lakini akakosea kuufahamu. Ni sikitiko kwamba makosa mengi yaliyomo katika *ijtihadi* ya Hadhrat Isa[as], mfano wake haupatikani katika Nabii mwingine yeyote. Labda hili pia ni sharti kwa Uungu wake, lakini je twaweza kusema kwamba kwa *ijtihadi* zake nyingi batili na bishara batili Utume wake umekuwa wenye mashaka? La, hasha. Ukweli wenyewe ni kwamba yakini inayotiliwa moyoni mwa nabii kuhusu unabii wake, hoja zile zinang'ara kama jua, na zinafululiza kujumuika kiasi hiki kwamba jambo lile linakuwa bayana pasipo kuhitaji hoja. Kisha, kama katika baadhi ya vipengele vingine litokee kosa la *ijtihadi*, hilo haliidhuru yakini, kama vile vitu viletwavyo karibu na mtu na vikisogezwa karibu na macho, basi macho ya mtu hayakosei kuvitambua, na yanaamua kwa yakini kwamba hiki ni kitu fulani, na kiwango chake ni kiasi kadha, na uamuzi huu unakuwa sahihi; na ushahidi wa kuona huku unakubaliwa mahakamani. Lakini kama kitu kisiletwe karibu na, kwa mfano, mtu aulizwe kutoka umbali wa nusu maili au robo maili kwamba kitu kile cheupe ni kitu gani, basi yumkini mtu mwenye mavazi meupe adhaniwe kuwa farasi mweupe, au kwa kumwona farasi mweupe amdhanie mtu. Basi, hivyo ndivyo Manabii na Mitume huonyeshwa kuhusu madai yao na kuhusu mafundisho yao kutoka karibu sana na huonyeshwa kwa mfululizo kiasi hiki hata

kwamba haibaki humo shaka yoyote. Lakini, baadhi ya vipengele vya mambo ambavyo havina makusudio ya muhimu, jicho linaviona katika kashfi kutoka mbali pasipo kufululiza kuona, kwa hiyo wakati mwingine jicho linadanganyika pia kuvitambua. Basi Hadhrat Isa[as] alipodanganyika katika bishara zake akadanganyika kwa sababu hii. Lakini, katika madai ya Unabii hakudanganyika, kwani Unabii wenyewe huo akaonyeshwa kutoka karibu na akaonyeshwa mara kwa mara.

Maulawii Thana'ullah amedanganyika pia kwamba anamtolea kila mtu Hadithi zinazopinzana, hivyo ndivyo akapata kudanganyika mzee wake Maulawii Muhammad Husain. Popote inapotajwa uhai au kifo cha Hadhrat Masihi[as] mara huleta rundo la Hadithi kwamba tazameni Sahihi Bukhari, Sahihi Muslim, Jam'i Tirmidhii, Sunan Ibni Majah, Sunan Abi Daud, Sunan Nasa'i, Musnad Imam Ahmad, Tabarni, Mu 'jam Kabir, Naim Ibn Hammad, Mustadrak Haakim, Sahihi Ibn Khuzaima, Nawaadirul Usuul Tirmidhii, Abu Daud Tialsi, Ahmad, Musnadul Firdaus, Ibn 'Asaakir, Kitabul Wafaa cha Ibn Jauzii, Sharhus-Sunnah Baghawii, Ibn Jariir, Baihaki, Akhbarul Mahdi, Musnad Abi Ya'la na vitabu vingine vya Hadithi, kwamba humo mmeandikwa kwamba Isa[as] atashuka, ingawa haijaamuliwa katika Baitul Makdis au katika Damaskas au katika Afiik au katika jeshi la

Waislamu. Hii ni 'tisho' linalotolewa siku hizi. Na la kushangaza zaidi ni kwamba baadhi ya vitabu kati ya hivyo vimeadimika kiasi hiki kwamba hata babu zao pia hawakupata kuviona, lakini wanataja majina yao ili ifahamike kwamba hao ndio masheikh wakubwa wanaojua vitabu vingi hivyo. Ni sikitiko kwamba watu hao ni mahaini; tunaona aibu kwa kuwataja Wayahudi, kwani ndani ya Islam wako Wayahudi wa namna hii.

Siku chache zimepita, Maulawii Muhammad Husain akiipelekea serikali ya Kiingereza kitabu fulani juu ya Mahdi akaifurahisha ambamo imeandikwa kwamba Hadithi yoyote kuhusu Mahdi haikuthibitika kuwa sahihi, na akapata ardhi kama zawadi, haijulikani kwa huduma ipi; lakini huduma yenyewe ni hii tu kwamba amefutilia mbali habari ya uwepo wa Mahdi. Sasa semeni, Masihi kutoka mbinguni atashuka katika jeshi la nani ilhali Mahdi hayupo? Vitabu vingi hivyo nilivyotaja hivi sasa vinatolewa kwa lengo hili kwamba kwa kumsaidia Mahdi, atakuja Masihi. Sasa, asipokuwapo Mahdi mwenyewe, Masihi atakujaje? Khalifa anapaswa kutoka katika Makureishi ambaye hayupo.

Angalieni, twasema kwa uadilifu kwamba Hadithi zilizopo katika vitabu vilivyotajwa juu, zilikuwa na miguu miwili; mguu moja kuhusu Mahdi, ambao Maulawii Muhammad Husain ameuvunja, sasa mguu wa pili

kuhusu ushukaji wa Masihi kutoka mbinguni twauvunja sisi. Kwani, kati ya sehemu mbili inapobatilika sehemu moja, basi yalazimu sehemu ya pili nayo pia ibatilike. Kwa Isa[as], Ukhalifa haukukubalika, kwani yeye siye miongoni mwa Makureishi, na Bwana Maulawii mwenyewe amefuta habari kuhusu Mahdi. Hivyo, kwa nini Isa[as] akalifishwe kuja tena ardhini; amezoea kukaa bila kazi tangu miaka elfu mbili na kuzoea starehe; sasa kumsumbua tena bila sababu yoyote haifai.

Isitoshe, kati ya Hadithi hizo kuna hitilafu kiasi hiki kwamba ikitafutwa Hadithi kinyume cha Hadithi yoyote, mara moja itapatikana. Kwa hiyo, kuacha mambo bayana ya Kurani Tukufu na kupoteza imani kwa ajili ya Hadithi kama hizo zinazopinzana ni kazi ya afkani, si ya mwenye akili.

Tena, tafakarini hii pia kwamba kama kinyume cha Kurani, Hadithi zina uzito wowote, basi Hadithi zielezazo sala zilipaswa kuwa za muhimu sana na kufululiza, lakini kuhusu hizo pia mnahitilafiana na mnafarakana. Haithibitiki mikono yapaswa kufunga wapi. Hitilafu za kuinua mikono, kutoinua mikono kusoma Sura Faatiha nyuma ya Imamu, kusema 'Amin' kwa sauti kubwa na kadhalika bado hazijakaribia kwisha; na baadhi yao wanapinga Hadithi za wengine. Kama Wahabi mmoja akienda msikitini mwa Mahanafii ainue mikono,

asome Sura Faatiha nyuma ya Imamu afunge mikono kifuani na aseme ‘Amin’ kwa sauti kubwa, huyo ingawa awasomee Hadithi sahihi mia nne kuthibitisha kitendo chake, hata hivyo lazima atarudi akiisha tandikwa barabara. Inathibitikia kwa jambo hilo kwamba tangu mwanzo Hadithi hazikuthamaniwa, na Imamu Mkuu aliyepita kabla ya Imam Bukhari hazijali Hadithi za Bukhari. Na zama zake zilikuwa karibu zaidi na zake; Hadithi zile zingepasa kumfikia. Hivyo, yafaa Kurani isiachwe kwa ajili ya Hadithi, waila imani itapotea. إِنَّ الظَّنَّ لَا يُغْنِىْ مِنَ الْحَقِّ شَيْـًٔا[27]. Kisha, kama uamuzi wa Mwamuzi pia usikubalike, basi yu Mwamuzi wa kitu gani?

Zaidi ya hii, kama tukilegeza sana, twaweza kuzipa Hadithi hizi daraja ya dhana na huo ndio msimamo wa muhaddithina. Na dhana inaweza kuwa na uongo. Basi, kuweka msingi wa imnai juu ya dhana tu na kutupa nyuma Neno la Mungu lenye yakini mkataa ni akili na uaminifu gani? Hatusemi, tupeni Hadithi zote kama kitu kisicho na thamani, bali twasema, zikubalini katika hizo zisizopingana na Kurani ili msiangamie. Haithibitiki kutokana na Hadithi yoyote kwamba umri wa Isa[as] utakuwa miaka elfu mbili au miaka elfu tatu; bali imeandikwa miaka mia moja na ishirini. Sasa semeni, miaka hiyo mia na ishirini mpaka sasa imekwisha au

[27] Hakika dhana haifai mbele ya haki hata kidogo. (Yuunus 10:37)

hapana. Katika Hadithi yoyote ambayo *isnadi* yake inaungana na kumfikia Mtume[saw] imeandikwa wapi kwamba Hadhrat Isa[as] akipasua paa la nyumba akapanda mbinguni, na ili kwa kulaaniwa alikuwa amewekwa mwanafunzi wake mmoja au adui yake. Kama alikuwa mwanafunzi, basi kwa sababu ya kusulubiwa, mwaminifu mmoja akafanywa maluuni sawa na Torati. Je kitendo hiki kiovu kinaweza kunasibishwa kwa Mungu! Na kama alikuwa ni Myahudi mmoja, basi kwa nini akanyamaza wakati wa kutundikwa msalabani? Na je mkewe na jamaa zake wengine wote walikuwa wamekwishakufa, na je alikuwa bubu ambaye hakuweza kuwatuliza wahusika ili kujiondolea lawama?

Zaidi ya hayo, Maulawii Muhammad Husain anayeitwa wakili wa Muwahhidina [Mawahabi] anaandika katika gazeti lake *Isha'atus Sunnah,* alimoandika maoni yake kuhusu *Baraahine Ahmadiyya*, kwamba watu wanaokutana na Mtume Mtukufu[saw] katika kashfi, hawawezi kufuata rai ya *muhaddithina*. Baadhi ya Hadithi ambazo sawa na rai ya *Muhaddithina* ni sahihi, hao sawa na kashfi zao wanaziona kuwa *maudhu'i* [za kuzitungwa]; na baadhi ya Hadithi zilizo sawa na *muhaddithina* ni za kutungwa, hao kwa ushahidi wa kashfi yao wanayo yakini ya usahihi wa hizo. Kama ni hivyo, basi anayedai kuwa Masihi Mau'udi na Mwamuzi, kwa nini bwana Maulawii

anamkasirikia kwamba haamini kashfi yake hata kuwa sawa na kashfi ya wengine ilihali hii inaafikiana na Kurani. Kurani na kashfi zilipopatana, bali baadhi ya Hadithi pia zimeitilia nguvu, basi yapasa kukubali kauli yake, waila yafaa nini kumwita Masihi Mau'udi kuwa Hakam (Mwamuzi)!

Baadhi ya masheikh wajanja husema kwamba hata kama mtu akishuka kutoka mbinguni na kusema Hadithi hizi mnazoamini si sahihi, hatutakubali kamwe na tutamchapa usoni. Jibu lake ni hili tu kwamba naam, twawatarajieni hivyo tu; lakini twasema kwa adabu kwamba neno '*Hakam*' lililotumika katika Sahihi Bukhari kumhusu Masihi Mau'udi, lifasirie tu. Mpaka sasa tulifahamu kwamba حَكَمٌ (Mwamuzi) ni yule ambaye amri yake ikubaliwe kwa kuondoa hitilafu, na uamuzi wake uchukuliwe kuwa mkataa hata kama aziite Hadithi elfu pia kuwa za kubuniwa. Mtu atakayekuja kutoka kwa Mungu hatakuja kuchapwa usoni nanyi; Mwenyezi Mungu Mwenyewe Atamfungulia njia. Mtu ambaye Mungu Akamjaalia kashfi na ufunuo na kadhihirisha ishara kubwa kubwa mkononi mwake, na sawa na Kurani Akamwonyesha njia, basi kwa nini ataachana na njia hii ya wazi na ya yakini kwa baadhi ya Hadithi za kudhaniwa. Na je hawajibiki kutenda sawa na Aliyomwamuru Mungu; na kama akikuta maana fulani ya Hadithi kuwa

kinyume cha ufunuo mtakatifu wa Mungu na akiona wahyi wake kuwa sawa na Kurani na akute Hadithi pia zinamsadikisha, basi aachane na Hadithi hizo na akubali Hadithi zile tu zilizo sawa na Kurani na si kinyume cha wahyi wake.

Nashangaa, bwana wakili ana tabia ya aina gani kwamba anaamini mawalii wa zamani waliopita ambao kwa kumlaki Mtume[saw] walikuwa wakiamua kuhusu Hadithi Sahihi kuwa ni ya kubuniwa, na ile Hadithi iliyokuwa ya kubuniwa kuwa ni sahihi, lakini anaona aibu kumpa Masihi Mau'udi pia aliye *Hakam* (Mwamuzi) daraja hii. Na ni ajabu kwamba wafuasi wake ni wa aina gani wasiomwuliza kwamba mawalii wengine wanazo hiari hizo, basi kwa nini unamkufurisha *Hakam* (Mwamuzi) kwa sababu ya hitilafu hizo, na kwa nini humchi Mungu. Nashangaa kwamba kwa sababu ya kuzeeka kumbukumbu ya Maulawii Muhammad Husain imeharibika kiasi hiki kwamba hakumbuki aliandika nini katika *Isha'atus Sunnah* na sasa anasema nini. Ee Bwana, baada ya ikrari ya mtu, kadhi hawezi kukubali kanusho lake. Umeshakiri kwamba wapatao kashfi na maongezi na Mungu wanayo daraja ya juu, hao hawalazimiki kukubali bila sababu ukosoaji wa *muhaddithina*; bali *muhaddithina* wamesimulia kutoka kwa wafu ilihali waonao kashfi wanasikiliza kutoka kwa Mzima wa milete na Mhifadhi wa kudumu. Basi, unamdhaniaje

mtu aliyeitwa ***Hakam*** (Mwamuzi); je hana hata daraja unayowapendekezea wengine.

Tena, Maulawii Thana'ullah anasema kwamba ulipataje moyoni mwako fikira ya bishara kuhusu Masihi Mau'udi, hiyo nayo imechukuliwa kutoka katika Hadithi tu; basi kwa nini alama zingine zilizoelezwa katika Hadithi hazikubaliwi? Watu hao wa kawaida wanasema hivyo kwa kuzusha au kwa sababu ya ujinga tu. Kwa kuijibu twasema kwa kuapa kwa Mwenyezi Mungu kwamba msingi wa madai yangu si Hadithi, bali ni Kurani na Wahyi ulioniteremkia. Naam, kwa kuyatilia nguvu twatoa Hadithi pia ziafikianazo na Kurani na hazipingani na wahyi wangu, na Hadithi zingine twazitupia kama kitu kisichofaa. Kama Hadithi zisingekuwepo duniani, hata hivyo madai yangu yasingepata madhara yoyote. Naam, katika wahyi wangu, Mungu Ametoa Kurani Tukufu mara kwa mara. Hivyo, utaona katika ***Baraahine Ahmadiyya*** kwamba kuhusu madai haya haikuelezwa Hadithi yoyote; mara kwa mara Mwenyezi Mungu Ametoa Kurani katika wahyi wangu.

Sasa nafikiri kwamba upinzani alioleta Maulawii Thana'ullah kwa kudanganya katika mjadala wa kijijini Mudd, wote umeshajibiwa. Naam, nimekumbuka kwamba wazo moja hili pia alitoa kwamba Hadithi kuhusu kupatwa kwa jua na mwezi ni alama ya Mahdi

kudhihiri iliyopo katika *Dar Kutni* na *Ikmalud Din*, humo kupatwa kwa mwezi kutakuwa katika tarehe kabla ya tarehe kumi na tatu ambamo twaweza kuuita mwezi kuwa *Kamar* قَمَر . Basi, ikumbukwe kwamba hii ndiyo kutoma maneno kama Wayahudi. Mungu Ameweka mausiku matatu sawa na suna yake kwa mwezi kupatwa, na kadhalika siku tatu kwa jua kupatwa. Na katika Hadithi imetajwa waziwazi kwamba katika zama atakapozaliwa Mahdi, mwezi utapatwa usiku wa kwanza katika tarehe zilizowekwa na kanuni ya Mungu kwa mwezi kupatwa, na jua litapatwa siku ya katikati katika siku zilizopangwa katika suna ya Mungu kwa kupatwa kwa jua. Kuacha maana hii iliyonyoka na kuhangaikia upande mwingine kama si bahati mbaya, ni nini basi?

Isitoshe, kwa Waarabu usiku ambamo *hilali* inaitwa *Kamar*, sio usiku wowote mahususi usio na hitilafu. Baadhi yao husema hilali ndiyo kwa usiku moja tu wa kwanza; usiku wa pili inakuwa Kamar; wengine wanasema, mwezi wa usiku wa tatu ni قَمَر (Kamar). Sawa na wengine tena mwezi unaendelea kuwa hilali kwa mausiku saba. Hivyo, katika hali hii kwa kudhihiri bishara hauwi usiku wowote maalumu.

Na kusema kwamba kupatwa kwa jua na mwezi sawa na suna ya Mungu si jambo lililo kinyume cha kawaida, ni ujinga wa pili. Shabaha yenyewe ya bishara hii si siyo

kuahidi kutokea kwa ajabu fulani kinyume cha kawaida, bali shabaha yenyewe ni kueleza alama fulani ambamo mwingine asishiriki.

Basi, Hadithi imeelezwa alama hii kwamba Mahdi wa kweli atakapodai, katika zama zile mwezi )قَمَر( utapatwa usiku wa kwanza, miongoni mwa mausiku ya kupatwa, katika mwezi wa Ramadhani, na tukio la namna hii litakuwa halikutokea hapo kabla. Na katika zama za Mahdi mwongo mwezi na jua havikupatwa ndani ya mwezi wa Ramadhani katika tarehe hizo. Na kama imetokea hivyo, basi uleteni uthibitisho, waila hali hii yenyewe kwa ujumla ni ya ajabu, basi kuna haja gani ya kuitafsiri kwa njia nyingine kinyume cha suna ya Mungu. Lengo lilikuwa kueleza alama moja, na hilo likapatikana; kama sivyo, basi toeni mfano wowote wa tukio hili kutoka katika historia, na ikumbukwe kwamba hamtaweza kutoa katu.

## Shairi la Kiurdu

کیوں نہیں لوگو تمہیں حق کا خیال      دِل میں آتا ہے مِرے سَو سَو اُبال

Enyi watu, mbona hamjali haki? nasikitika sana mno moyoni mwangu.

آنکھ تر ہے دِل میں میرے درد ہے      کیوں دِلوں پر اِس قدر یہ گرد ہے

Machozi yananilengalenga, moyo wangu unaumia; kwa nini nyoyo zimepatwa na vumbi jingi hivyo!

دِل ہوا جاتا ہے ہردم بے قرار      کِس بیاباں میں نکالوں یہ بخار

Wakati wote moyo unakosa utuvu, nilie katika pori gani kujituliza!

ہو گئے ہم درد سے زیر و زبر      مَر گئے ہم پر نہیں تم کو خبر

Tupo taabani kwa maumivu; tumekufa lakini nyinyi hamna habari.

آسماں پر غافلو اِک جوش ہے      کچھ تو دیکھو گر تمہیں کچھ ہوش ہے

Enyi mlioghafilika, kuna hamasiko huko mbinguni, angalieni kidogo ikiwa mnao ufahamu kidogo.

ہو گیا دیں کفر کے حملوں سے چُور      چُپ رہے کب تک خداوندِ غیور

Dini imejeruhiwa sana kwa mashambulizi ya kufuru, mpaka lini Anyamaze Mungu Mwenye ghera.

اِس صدی کا بیسواں اب سال ہے      شرک و بدعت سے جہاں پامال ہے

Huu ni mwaka wa ishirini wa karne hii; dunia imekanyagiliwa mbali na shirki na bidaa.

بدگماں کیوں ہو خدا کچھ یاد ہے    افترا کی کب تلک بنیاد ہے

Mbona mna dhana mbaya; je mwamkumbuka kidogo Mungu? Uzushi utaendelea mpaka lini!

وہ خدا میرا جو ہے جوہر شناس    اِک جہاں کو لا رہا ہے میرے پاس

Mungu wangu Yule Ajuaye sifa za ndani za watu Anaendelea kuwaongoza watu kunijia.

لعنتی ہوتا ہے مَردِ مُفتری    لعنتی کو کب ملے یہ سروری

Hulaaniwa aliye mtu mzushi; mlaaniwa anapataje uongozi huu!

Jambo moja limebakia lililolazimika kueleza, nalo ni kwamba katika mjadala wa Mudd, rafiki yetu mwaminifu, Seyid Muhammad Sarwar Shah, alipotoa *I'jazul Masihi* kilicho kitabu changu kwa Kiarabu kama ishara kwamba hiki ni muujiza, na wapinzani hawakuweza kuleta mfano wake, hapo Maulawii Thana'ullah akimtaja Maulawii Muhammad Husain wa Batala akasema kwamba yeye ametayarisha orodha ndefu ya makosa yaliyomo katika *I'jazul Masihi*. Twakubali kwamba pengine ameitayarisha, lakini itakuwa orodha kama vile bwana Maulawii alikosoa sentensi yangu moja kwamba *lam* haitumika kama kiwakilishi rejeshi kwa neno *'Ajab*, na akasisistiza sana. Lakini alipoonyeshwa beti za ustadhi wa zamani na za washairi wa zama za kabla ya Islam, bali baadhi ya Hadithi pia ambamo *lam* imetumika kuwa kiwakilishi

rejeshi, hapo Bwana Maulawii akaghariki 'kisimani', mwa majuto hata kwamba rafiki yake yeyote mtaalamu pia hakuweza kumwokoa humo kisimani. Hii ni habari ya siku zile ilipotolewa bishara kuhusu kudhalilika kwa Bwana Maulawii huyo na ikaandikwa katika tangazo kwamba bishara ile imetimia kwa njia mbili.

Ya kwanza, mwenendo wa kiunafiki wa Bwana Maulawii ulithibitika kwamba anatuliza serikali kwamba Mahdi si kitu chochote, Hadithi zote ni batili, hazitegemewi, ni Mahdi gani, na Masihi gani yule atakayekuja kutoka mbinguni kwa kumsaidia yeye; mambo yote hayana asili. Na kwa kueleza mambo haya anaonekana anatamani zawadi kubwa. Na ikiwa angekana Mahdi na Masihi wa aina hii kwa moyo basi sisi pia tungemfurahia kwani msema kweli anapaswa kuheshimika; na kwa sababu hii kama serikali ingempatia ardhi si tu katika Lyallpur bali hata kama ingempa Batala nzima kama miliki yake basi ingekuwa haki yake. Lakini, haturidhiki wala hatuwezi kamwe kwamba mtu kwa unafiki wake tu akitoa mbele ya serikali orodha ya Hadithi dhaifu na batili kuhusu Mahdi anataka kuiyakinishia kwamba Waislamu hawamsubiri Mahdi na Masihi wa namna hii atakayepigana na Wakristo. Na anaiyakinishia kwamba itikadi yangu ndiyo kwamba Mahdi yeyote wa aina hii hatakuja atakayemwaga sana damu wala hakuna Masihi yeyote atakayeshuka

kutoka mbinguni kumsaidia katika kazi hii. Kisha kisirisiri anawaambia watu wake kwamba kumkanusha Mahdi wa aina hii ni kufuru. Na ni la kushangaza kwamba kwa matendo yake hayo haikutokea kasoro yoyote katika heshima yake, wala heshima ya wafuasi wake haikuvunjika.

Ilmuradi, hiyo ndiyo ilikuwa ni dhila iliyomsibu Maulawii Muhammad Husain ambamo Ja'far Zatalli na wafuasi wake wengine wanayo sehemu, waihisi au wasihisi kwa utovu wa haya. Na dhila ya pili ikamsibu kuhusu elimu yake kwamba bila haki akapiga kelele mbele ya watu kwamba *Laam* haitumiki kamwe kama kiwakilishi rejeshi kwa neno *'ajab*, basi nilikosea sana. Lakini nia ya Maualwii Thana'ullah inaonekana kwamba dhila hizi si kitu chochote; ingefaa kuwa dhila nyingine. Na anasema kwamba yeye amepewa ardhi, ilihali ardhi hii hii inashuhudia dhila yake na yashuhudia unafiki wake. Maadamu anayo ardhi ile, unafiki huu pia utafahamika kuwa tunda la ardhi ile; au mfahamu hivi kwamba ardhi ni tunda la unafiki wake; na mfanye utafiti kwamba ushindi huo wote ni matokeo ya tendo la unafiki. Ikiwa mnataka kujua itikadi za siri za watu hao, basi inapasa kusoma vitabu vya Siddik Hasan ambamo, Mungu Apishe mbali, anamhudhurisha Malkia Muadhama pia mbele ya Mahdi na amemtaja kwa maneno mabaya sana

na ujeuri ambayo hatuwezi kuyanukuu hapa kwa njia yoyote. Atakaye avitazame vitabu hivyo. Huyu ndiye Siddik Hasan yule yule ambaye Muhammad Husain alikuwa amemfanya kuwa Mujadidi. Kivipi na kwa njia gani rai yake yaweza kuwa tofauti na rai ya Mujadidi wake; la hasha. Ni vizuri sana kwamba serikali ya Kiingereza isaidiwe na iondolewe mioyoni mawazo ya masiala potofu ya jihadi na akataliwe Mahdi mwaga damu na Masihi mwaga damu wa aina hii. Lakini, laiti kama kwa ukweli wa moyo Maulawii Muhammad Husain angeeleza mambo hayo mbele ya serikali, bila shaka angesifika machoni petu pia. Lakini, sasa vitabu vyake vinavyopinzana vyaeleza mambo tofauti mbele ya serikali na anayowaeleza chumbani mbele ya ndugu zao vinathibitisha mwendo wake wa unafiki; na mnafiki hudhalilika mbele ya Mungu pia na mbele ya viumbe vilevile. Watu hao kwa hakika wako matatizoni; itikadi zao kadhaa ni kinyume cha masilahi ya serikali. Sasa wasipofuata njia ya unafiki, basi wafanyeje.

Ilmuradi, twatambua ujuzi wa Kiarabu wa Maulawii Muhammad Husain si kuanzia leo bali tangu aliposema kwamba *Lam* haitumiki kabisa kama kiwakilishi rejeshi kwa neno *'Ajab*. Kama mtaalamu mkubwa wa aina hii ametayarisha orodha ndefu ya makosa ya *I'jazul Masihi* basi hatukatai, lazima atakuwa akaitayarisha. Maulawii

Thana'ullah anajua kwamba mtu wa kwanza wa kulengwa na shindano la ujuzi wa Kiarabu ni huyu huyu mtaalamu ambaye nilimwandikia kwamba kwa kila kosa twaweza kumpatia zawadi ya rupia tano sharti uthibitishe kwanza u mtaalamu wa lugha ya Kiarabu kwa njia hii kwamba ukikaa pamoja nami uandike maelezo ya aya yoyote kiasi cha *juzuu*[28] moja au *juzuu* mbili; hapo hatukupata jibu lolote kutoka kwake. Kila mtu aweza kuelewa kwamba kukosoa ni haki ya mtu ambaye kwanza athibitishe ubingwa wake, waila ni porojo tu. Kwa mfano, kama mtu ni jahili mtupu asiye na ufundi wa ujenzi na aendelee kusem kwamba waashi wa nchi hii wanakosea katika kazi yao, je hatapaswa kuambiwa, Ee mjinga, huwezi kuweka hata tofali moja barabara, mbona unawakosoa hao waashi ambao yapo majengo mengi waliyojenga kwa mikono yao.

Sasa, ikumbukwe kwamba ingawaje mpaka sasa nimeshachapisha vitabu takriban kumi na saba kwa Kiarabu visivyo na mfano ambavyo kukabiliana navyo wapinzani hawajachapisha hata kitabu kimoja katika muda huu wa miaka kumi, lakini leo nimepata wazo kwamba kwa vile vitabu hivyo sivyo tu katika lugha fasaha ya Kiarabu bali ndani mwao mna maarifa ya ndani sana ya Kurani, kwa hiyo yumkini watu hao waseme

[28] *Juzuu* katika istilahi ya uchapaji inamaanisha kurasa 16. Mwenezi.

kwamba hatujui maarifa ya ndani; kama ingekuwa nudhumu tu kwa Kiarabu fasaha kama vile kasida za kawaida, basi bila shaka tungeweza kuleta mfano wake. Isitoshe, nilipata wazi hili pia kwamba Maulawii Thana'ullah akiambiwa mfano wa kitabu *I'jazul Masihi* tu, basi lazima atasema kwamba ithibitikeje kwamba kitabu hicho kiliandikwa katika siku sabini tu; na akitoa hoja hii kwamba kitabu hiki kimeandikwa katika miaka miwili na sisi pia tupewe muda wa miaka miwili, hapo itakuwa vigumu twaweze kuthibitisha waziwazi siku sabini. Kwa sababu hizo ikaonekana afadhali nimwombe Mwenyezi Mungu kwamba Anisaidie kwa Roho Mtakatifu kuandika kasida ya kawaida ambamo utajwe mjadala wa Mudd ili isiwe shida kufahamu kwamba kasida imetungwa katika siku ngapi. Basi nikaomba kwamba Ee Mungu Mweza, Unijaalie kama ishara kutunga kasida kama hiyo. Na dua yangu hiyo ikakubalika na nikasaidiwa kimuujiza kutoka kwa Roho Mtakatifu, nami nikamaliza kasida katika siku tano tu. Laiti nisingelazimika na shughuli nyingine basi kasida ile ingekamilika katika siku moja tu. Laiti isingechelewa kidogo[29] kuchapwa, basi ingeweza kuenezwa kasida ile mpaka 9 Novemba 1902.

---

[29] Hii pia ilikuwa sababu ya kuchelewa kwamba nikalazimika kwenda Batala katika mahakama ya hakimu tarehe 7 Novemba

Hii ni ishara adhimu ambayo shahidi wake ni Maulawii Thana'ullah mwenyewe, kwani inathibitika kutoka katika kasida kwamba imetungwa baada ya mjadala wake, na mjadala ulifanyika tarehe 29 na 30 Oktoba 1902. Na baada ya kurudi marafiki zetu tarehe 8 Novemba 1902 kasida hii ikaanza kutungwa na tarehe 12 Novemba 1902 ikamalizika pamja na ibara hii ya Kiurdu. Kwa vile najua kwa yakini kwamba hii ni ishara kubwa ya msaada wa Mungu ili Amfedheheshe mpinzani na kufumba mdomo wake, kwa hiyo namtolea Maulawii Thana'ullah na wasaidizi wake ishara hii pamoja na zawadi ya rupia elfu kumi kwamba ikiwa katika muda huo, yaani katika siku tano, wachapishe kasida ya aina hii pamoja na kujibu makala ya Kiurdu kiasi hicho, ambayo pia ni ishara, basi bila kuchelewa nitawakabidhi rupia elfu kumi. Kwa kuchapisha nampa muda wa wiki moja zaidi. Kwa jumla siku hizi ni kumi na mbili, na siku mbili kwa kutuma kwa posta pia ni haki yao. Kwa hiyo, kama kuanzia tarehe itakapowafikia kasida hii na ibara ya Kiurdu apate kuchapisha beti fasaha kiasi hicho zisizopungua kadiri na idadi hiyo katika siku kumi na nne, basi nitatoa zawadi ya rupia elfu kumi. Atakuwa na hiari apate kusaidiwa na Maualwii Muhammad Husain au mtu mwingine. Isitoshe,

1902. Muda wa kuandika ulikuwa ni siku tatu tu, na siku mbili zikazidi kwa shida hiyo. Mwandishi

anapaswa kujitahidi kwa sababu hii pia kwamba katika tangazo langu moja imetolewa habari kama bishara kwamba mpaka mwisho wa Desemba 1902 itadhihirika ishara isiyo ya kawaida. Ingawa ishara ile imeshadhihirika kwa sura zingine pia, lakini kwa Maulawii Thana'ullah na wahusika wengine hawakuandika au kuandikisha kasida na jibu la makala ya Kiurdu ndani ya muda huu, basi ishara ile itatimia kwa njia yao. Basi, wanawajibika kwamba ikiwa wanadhania kazi yangu kuwa hila ya mtu,[30]

[30] Kwa vile matusi na ukadhibishaji umefika keleleni ambao karatasi zake nimezihifadhi katika mfuko mkubwa, na watu hao katika matangazo yao wanazikadhibisha mara kwa mara ishara za zamani na kuomba ishara mpya, kwa hiyo twawapa ishara hii. Kadhalika Wakristo pia wameniandikia mara kwa mara kwamba imo katika Injili kwamba Masihi waongo watakuja, na wakaniita Masihi mwongo ilihali siku hizi huko London hasa yupo Masihi mwongo miongoni mwa Wakristo anayeitwa Pigott anayedai kuwa Mungu na Masihi na anatimiza bishara za Injili. Lakini, katika siku zijazo yeyote akitaka kuniita mwongo, basi alazimika ashindane nami katika ishara zangu. Katika Wakristo pia wako wengi walioritadi wanaodai kuwa masheikh. Ikiwa mapadri ni wakweli katika kunikadhibisha, basi wawafanye masheikh hao kutunga kasida ya aina hii katika siku tano na kupokea kutoka kwangu rupia elfu kumi, na wazitumie katika shughuli za misheni. Lakini mtu atakayepayuka baada ya tarehe iliyowekwa au kuonyesha maandishi yoyote, maandishi yake yatapaswa kutupwa katika mfereji wa uchafu. Mwandishi

basi kwa kushindana wazuie kwa njia yoyote ishara hii isitimie. Na angalieni, nasema kwa kuapa kwamba yeye peke yake au kwa kusaidiwa na wengine katika muda uliowekwa akichapisha kasida sawasawa na kasida yangu na ibara ya Kiurdu, sawa na idadi yao, na kunitumia kupitia posta katika siku kumi na mbili kuanzia tarehe ya kupokea, basi sitafanya hii tu kwamba nitampa zawadi ya rupia elfu kumi, bali kwa ushindi huu wake nitathibitika kuwa mwongo. Katika hali hii Maulawii Thana'ullah na marafiki zake hawatakuwa na haja ya kuzusha bila haki na watapata ushindi wa bure; la sivyo hawatakuwa na haki tena ya kuniita mwongo au kukadhibisha ishara zangu. Angalieni, nasema nikiweka mbingu na ardhi kuwa mashahidi kwamba kuanzia tarehe ya leo najiwekea ishara hii ya ukweli wangu. Kama mimi ni mkweli, na Mwenyezi Mungu Ajua kwamba mimi ni mkweli, basi haitayumkinika kwamba Maulawii Thana'ullah na masheikh wao wote kuweza kutunga kasida katika siku tano na kuweza kujibu ibara ya Kiurdu, kwani Mwenyezi Mungu Atazivunjilia mbali kalamu zao na Atawapumbaza akili zao. Na Maulawii Thana'ullah hawezi kudhania vibaya na kusema kuwa kasida ilitungwa mapema, kwani akifungua jicho kidogo aone kwamba mjadala wa Mudd umetajwa humo. Basi, ikiwa nilitunga mapema basi wanapaswa kukubali kwamba mimi ni mjuzi wa mambo ya ghaibu. Kwa vyovyote hii pia ni ishara. Kwa hiyo, sasa

hawana pa kukimbilia; na ufunuo umetimia leo Alionifunulia:

قادر کے کاروبار نمودار ہو گئے
کافر جو کہتے تھے وہ گرفتار ہو گئے

'Kazi za Mweza zimedhihirika,

Walionikufurisha wamekamatwa.'

Na ibainike kwamba kupitia Maulawii Thana'ullah zitatimia karibuni ishara zangu tatu. (1) Hatanijia kamwe Qadian kwa kupeleleza bishara zote, na itakuwa ni kama mauti yake kusadikisha bishara za kweli kwa kalamu yake. (2) Akiwa tayari kwa changamoto hii kwamba mwongo afe kabla ya mkweli, basi lazima atakufa kabla yangu. (3) Na awali ya yote kwa kushindwa katika kujibu ibara hii ya Kiurdu na kutunga kasida ya Kiarabu fedheha yake haraka sana itathibitika.

Na kwa kuwa siku hizi Maualwii Muhammad Husain ameisifu sana elimu ya Mehr Ali Golarawii katika gazeti lake *Isha'atus Sunnah*, na Bwana Ali Ha'irii Mshia anajisifu sana, kwa hiyo nawakaribisha pia kwa mashindano haya. Kwa kutukana na kufanya masihara ulimi wa watu hao ni mrefu, lakini sasa nitaona kwamba wanaweza kupata msaada kiasi gani kutoka kwa Mungu. Nimeandika kidogo kuhusu watu hao pia katika kasida hii ili niamshe ghera yao. Huu ni uamuzi wa mwisho. Mshia aombe msaada

kutoka kwa Husain, na Bwana Golarawii kutoka kwa kiongozi wake yeyote, na Maualwii Thana'ullah na marafiki zake ambao wenyewe huitwa masheikh, watumie nguvu zao zote.

Niliyoandika katika kasida hii kuhusu Imam Husain[ra] au kuhusu Hadhrat Isa[as], huu sio utendaji wa kibinadamu. Yu mtu habithi ambaye kwa matamanio ya nafsi yake anawatukana wakamilifu na wakweli. Nina yakini kwamba kwa kumtukana mkweli kama Husain[ra] au Hadhrat Isa[as] hawezi kubaki hai hata kwa usiku mmoja, na onyo la مَنْ عَادٰى لِيْ وَلِيًّا linamkamata haraka.

Basi, amebarikiwa anayeelewa busara za mbingu na kuzingatia hekima ya mikakati yake. Na kutoka kwangu, siyo ahadi ya zawadi ya rupia elfu kumi tu bali mkorofi asiyejizuia kutusi wala hakomi kufanya mzaha wala haachani na tabia ya kuvunja heshima, na hukanusha ishara zangu katika kila kikao, anapaswa kwamba alete mfano wa ishara hii katika muda uliowekwa, waila kwa kudumu na mpaka mwisho wa dunia ataendelea kulaaniwa kutoka mbinguni. Hususani Maulawii Thana'ullah aliyedai mwenyewe kunihusu kwamba maandishi ya mtu huyu si muujiza, anapaswa kuogopa isije akakanyagwa chini ya laana hizi kwa kunyamaza. Na laana zile ni hizi:

| | |
|---|---|
| 1. Laana | ١ لعنة |
| 2. Laana | ٢ لعنة |
| 3. Laana | ٣ لعنة |
| 4. Laana | ٤ لعنة |
| 5. Laana | ٥ لعنة |
| 6. Laana | ٦ لعنة |
| 7. Laana | ٧ لعنة |
| 8. Laana | ٨ لعنة |
| 9. Laana | ٩ لعنة |
| 10. Laana | ١٠ لعنة |

وتلك عشرة كاملة

Na hizi ni kumi kamili.

Sasa kwa kumtegemea Mungu Mweza, Karimu, Mtakatifu na Mwenye ghera, naandika kasida na kumwomba Msaidizi na Mhisani wangu kusaidiwa. Ee Mweza wangu Mpendwa na Shahidi wa siri za mioyo, nisaidie na fanya hivi kwamba ishara Yako hii inga're duniani na mpinzani yeyote asiweze kutunga mfano wake katika muda uliowekwa. Ee Mpendwa wangu, fanya hivyo, na uwaongoze wengi kwa ishara hii na kwa ibara yote hii. Amin, tena Amin.

Na kasida ile ni hii:

# اَلْقَصِيْدَةُ الْاِعْجَازِيَّةُ

## Kasida Isiyoshindika

اَ يَا اَرْضَ مُدٍّ قَدْ دَفَاكِ مُدَمِّرٌ          وَ اَرْدَاكِ ضِلِّيْلٌ وَّ أَغْرَاكِ مُوْغِرُ

Ee ardhi ya Mudd[31], aliyehilikika amekuhilikisha ulipokuwa hoi[32]; na mpotevu mmoja amekuangamiza na mchochezi mmoja akakuchochea.

دَعَوْتِ كَذُوْبًا مُّفْسِدًا صَيْدِىَ الَّذِىْ          كَحُوْتِ غَدِيْرٍ اَخْذُهٗ لَا يُعَذَّرُ

Ulimleta mwongo mkubwa mfitini, windo langu, ambaye kumshika si vigumu kama kuvua samaki wa bwababawani.

وَ جَاءَكِ صَحْبِىْ نَاصِحِيْنَ كَاِخْوَةٍ          يَقُوْلُوْنَ لَا تَبْغُوْا هَوًى وَ تَصَبَّرُوْا

Na marafiki zangu wakakujia wakikusihi kama ndugu, wakasema msielekee matamanio, na subirini.

فَظَلَّ أُسَارَاكُمْ اُسَارٰى تَعَصُّبٍ          يُرِيْدُوْنَ مَنْ يَّعْوِىْ كَذِئْبٍ وَّ يَخْتِرُ

Na miongoni mwenu walionaswa na chuki, wakataka kumtafuta mtu abwekaye kama mbwamwitu na anadanganya.

---

[31] Mudd ni nomino sahihi ya Kiarabu, si ya Kiajemi. Nchi walizoendea Waislamu na majina waliyozipa sehemu mbalimbali, mengi zaidi yalikuwa ya Kiarabu. Mwandishi

[32] Maana ya دفو ndiyo kukiangamiza kilichokuwa hai. Basi wakazi wa Mudd waliokuwa na hali mbovu akawahilikisha Thana'ullah kwa kuwaendea na kuwaelezea uongo; naye mwenyewe alikuwa ameangamia, yaani mbele yetu alikuwa aliyehilikika. Basi, aliyehilikika akawahilikisha majahili hawa. Mwandishi.

فَجَاءُوْا بِذِئْبٍ بَعْدَ جُهْدٍ اَذَابَهُمْ          وَ نَعْنِىْ ثَنَاءَ اللهِ مِنْهُ وَ نُظْهِرُ

Basi, baada ya juhudi kubwa wakamleta mbwamwitu, twamaanisha Thana'ullah na twadhihirisha.

فَلَمَّا اَتَاهُمْ سَرَّهُمْ مِّنْ تَصَلُّفٍ          وَ قَالَ افْرَحُوْا اِنِّىْ كَمِىٌّ مُّظَفَّرُ

Na alipowafikia akawachangamsha kwa maringo yake; akasema furahini, mimi ni shujaa, mshindi.

وَ قَالَ اسْتُرُوْا اَمْرِىْ وَاِنِّىْ اَرُوْدُهُمْ          اَخَافُ عَلَيْهِمْ اَنْ يَّفِرُّوْا وَ يُدْبِرُوْا

Akasema, ficheni habari ya ujio wangu, kwani nawatafuta; nahofia isije wakakimbia.

وَ اَرْضَى اللِّئَامَ اِذَا دَنَا مِنْ اَرْضِهِمْ          عَلَى النَّارِ مَشَّاهُمْ وَ قَدْ كَانَ يَبْطَرُ

Na akawafurahisha watu dhalili alipokaribia ardhi yao; akawatembeza juu ya moto na kafurahi sana.

تَكَلَّمَ كَالْاَجْلَافِ مِنْ غَيْرِ فِطْنَةٍ          وَ يَأْتِيْكَ بِالْاَخْبَارِ مَنْ كَانَ يَنْظُرُ

Akanena bila akili kama watu duni; na watazamaji watakuja kukuhadithia.

وَ اِنْ كُنْتَ فِىْ شَكٍّ فَسَلْ يَا مُكَذِّبِىْ          دَهَاقِيْنَ مُدٍّ وَّ الْحَقِيْقَةُ اَظْهَرُ

Na ikiwa una shaka, basi waulize wakulima wa Mudd; na hakika ilibainika.

فَلَمَّا الْتَقَى الْجَمْعَانِ لِلْبَحْثِ وَ الْوَغَا          وَ نُوْدِىَ بَيْنَ النَّاسِ وَ الْخَلْقُ اُحْضِرُوْا

Basi, makundi mawili yalipojumuika kufanya mjadala, na ikatangazwa baina ya watu, na halaiki ya watu wakahudhuria.

وَ اَوۡجَس خِيۡفَةَ شَرِّهٖ بَعۡض رُفۡقَتِیۡ      لِمَا عَرَفُوۡا مِنۡ خُبۡثِ قَوۡمٍ تَنَمَّرُوۡا

Na baadhi ya marafiki zangu wakahisi moyoni mwao hofu ya shari yake, kwani walikwishajua ukatili wa watu hao.

فَاُنۡزِلَ مِنۡ رَّبِّ السَّمَاءِ سَکِيۡنَةٌ      عَلٰی صُحۡبَتِیۡ واللّٰهُ قَدۡ کَانَ يَنۡصُرُ

Basi, marafiki zangu wakateremshiwa utuvu kutoka kwa Mola wa mbingu, na Mungu ndiye alikuwa akisaidia.

وَ اَعۡطَاهُمُ الرَّحۡمٰنُ مِنۡ قُوَّةِ الۡوَغٰی      وَ اَيَّدَهُمۡ رُوۡحٌ اَمِيۡنٌ فَاَبۡشَرُوۡا

Na Rahmani Akawajalia nguvu ya kupigana, na Roho Mwaminifu akawasaidia, basi wakafurahi.

وَ کَانَ جِدَالٌ يَطۡرُدُ الۡقَوۡمَ بِالضُّحٰی      اِلٰی خِطَّةٍ اَوۡمٰی اِلَيۡهَا الۡمَعۡشَرُ

Na karibu saa mbili asubuhi watu wakaelekea kwenye sehemu ile waliyoashiria watu hao, kujionea wenyewe mjadala.

تَحَرَّوۡا لِهٰذَا الۡبَحۡثِ اَرۡضًا شَجِيۡرَةً      اِلَی الۡجَانِبِ الۡغَرۡبِیِّ وَ الۡجُنۡدُ جُمِّرُوۡا

Kwa mjadala huu wakachagua ardhi yenye miti, na sehemu hiyo ilikuwa nje ya kijiji upande wa magharibi, na marafiki zetu wakapangiwa kukaa hapo.

فَکَانَ ثَنَاءُ اللّٰهِ مَقۡبُوۡلَ قَوۡمِهٖ      وَ مِنَّا تَصَدّٰی لِلتَّخَاصُمِ سَرۡوَرُ

Na Thana'ullah akakubaliwa na watu wake, na kutoka kwa upande wetu Maulawii Seyid Muhammad Sarwar Shah akajitokeza kufanya mjadala.

كَاَنَّ مَقَامَ الْبَحْثِ كَانَ كَاَجَمَةٍ بِهِ الذِّئْبُ يَعْوِى وَ الغَضَنْفَرُ يَزْئَرُ

Kana kwamba mahali pa mjadala palikuwa kama pori ambamo upande moja mbwamsitu alikuwa akibweka na upande mwingine simba akanguruma.

وَ قَامَ ثَنَاءُ اللّٰهِ يُغْوِىْ جُنُوْدَهُ وَ يُغْرِىْ عَلٰى صَحْبِىْ لِئَامًا وَّ يَهْذُرُ

Na Thana'ullah akainuka akiwapoteza kundi lake na kuwachochea dhidi ya marafiki zangu na kubwabwaja.

وَ كَانَ طَوٰى كَشْحًا عَلٰى مُسْتَكِنَّةٍ وَ مَا رَادَ نَهْجَ الْحَقِّ بَلْ كَانَ يَهْجُرُ

Na akawa na chuki moyoni, na hakutafuta njia ya haki bali akaendelea kutumia mdomo mchafu.

سَعٰى سَعْىَ فَتَّانٍ لِتَكْذِيْبِ دَعْوَتِىْ وَ كَانَ يُدَسِّى مَا تَجَلّٰى وَ يَمْكُرُ

Akajaribu kukadhibisha madai yangu kama mtu mfitini, na akaficha haki na kufanya hila.

وَ اَظْهَرَ مَكْرًا سَوَّلَتْ نَفْسُهُ لَهُ وَلَمْ يَرْضَ طُوْلَ الْبَحْثِ فَالْقَوْمُ سُحِّرُوْا

Na akadhihirisha hila iliyozuka moyoni mwake na akakataa kuendeleza mjadala na watu wakadanganyika.

فَشَقَّ عَلٰى صَحْبِىْ طَرِيْقٌ اَرَادَهُ وَ قَدْ ظُنَّ اَنَّ الْحَقَّ يُخْفٰى وَ يُسْتَرُ

Basi, marafiki zangu wakaona vigumu kuvumilia njia ile aliyonuia, na wakadhani haki itafichika kwayo.

رَءَوْا بُرْجَ بُهْتَانٍ تُشَادُ وَ تُعْمَرُ فَقَالُوْا لَحَاكَ اللّٰهُ كَيْفَ تُزَوِّرُ

Wakaona anasingizia sana mno; basi wakasema Mungu Akulaumu, unaongopaje hivyo!

اَقَلُّ زَمَانِ الْبَحْثِ مِقْدَارُ سَاعَةٍ      فَلَمْ يَقْبَلِ الْحُمْقٰى وَ صَحْبِیْ تَنَفَّرُوْا

Muda wa majadiliano unapaswa kuwa saa moja kwa akali, lakini wajinga hawakukubali; na marafiki zangu wakauchukia muda uliowekwa.

رَضُوْا بَعْدَ تَكْرَارٍ وَّ بَحْثٍ بِثُلْثِهَا      وَ فِي الصَّدْرِ حُزَّازٌ وَ فِي الْقَلْبِ خَنْجَرُ

Hatimaye, baada ya mabishano na majadiliano, wakakubali kujadiliana kwa dakika ishirini ishirini, huku wakawa na hasira kifuani na hanjari moyoni.

دَهَاهُمْ عَمَايَاتُ الْاُنَاسِ وَ حُمْقُهُمْ      رَأَوْا مُدَّ قَوْمٌ وَّ الْمُدٰى قَدْ شَهَّرُوْا

Ujinga wa kaumu ukawafanya hoi, wakakiona kijiji cha Mudd kuwa ni watu waliochomoa visu vyao.

فَصَارُوْا بِمُدٍّ لِلرِّمَاحِ دَرِيَّةً      وَ يَعْلَمُهَا اَحْمَدْ عَلِيُّ الْمُدَبِّرُ

Basi, marafiki zangu wakawa lengo la mikuku huko Mudd, na Ahmad Ali aliyekuwa mwenyekiti wa hadhara anajua vizuri habari hii.

وَ كَانَ ثَنَاءُ اللّٰهِ فِيْ كُلِّ سَاعَةٍ      يُأَجِّجُ نِيْرَانَ الْفَسَادِ وَ يُسْعِرُ

Na Thana'ullah kila saa alikuwa akichochea moto wa machafuko.

أَرٰى مَنْطِقًا مَا يَنْبَحُ الْكَلْبُ مِثْلَهُ      وَ فِيْ قَلْبِهِ كَانَ الْهَوٰى يَتَزَخَّرُ

Naona akatamka maneno ambayo hata mbwa habweki hivyo, na moyoni mwake matamanio yakafurika.

وَ اِنَّ لِسَانَ الْمَرْءِ مَالَمْ يَكُنْ لَّهُ　　　اُصَاةٌ عَلٰى عَوْرَاتِهٖ هُوَ مشعرُ

Na ulimi wa mtu asipokuwa na akili, ni dalili ya aibu zake zilizofichika.

يُكَلِّمُ حَتّٰى يَعْلَمَ النَّاسُ كُلُّهُمْ　　　جَهُوْلٌ فَلَا يَدْرِىْ وَ لَا يَتَبَصَّرُ

Mtu kama huyo analonga mpaka watu wote wanajua kuwa yu jahili, hana akili wala busara.

وَ لَوْ لَا ثَنَاءُ اللّٰهِ مَا زَالَ جَاهِلٌ　　　يَشُكُّ وَ لَا يَدْرِىْ مَقَامِىْ وَ يَحْصُرُ

Na lau kama asingekuwa Thana'ullah, mtu jahili angekuwa na shaka kunihusu na kunisumbua kwa maswali, asijue daraja yangu.

فَهٰذَا عَلَيْنَا مِنَّةٌ مِّنْ اَبِى الْوَفَا　　　اَرٰى كُلَّ مَحْجُوْبٍ ضِيَائِىْ فَنَشْكُرُ

Basi, hii ni hisani ya Abul-Wafaa (Maulawii Thana'ullah) aliyotufanyia kwamba alimwonyesha kila mwenye kughafilika nuru yetu, basi twamshukuru.

اَرَى الْمَوْتَ يَعْتَامُ الْمُكَفِّرَ بَعْدَهٗ　　　بِمَا ظَهَرَتْ آىُ السَّمَاءِ وَ تَظْهَرُ

Sasa namwona akufurishaye atajifia, kwani kwa ushindi wetu ishara ya Mungu imedhihirika.

وَ لَمَّا اعْتَدَى الْاَمْرَتْسَرِىْ بِمَكَائِدٍ　　　وَ اَغْرٰى عَلٰى صَحْبِىْ لِئَامًا وَّ كَفَّرُوْا

Na mtu wa Amritsar (Thana'ullah) alipovuka mpaka kwa hila zake, na akawachochea watu dhidi ya marafiki zangu,

فَقَالُوْا لِيُوْسُفَ مَانَرَى الْخَيْرَ هٰهُنَا        وَ لٰكِنَّهُ مِنْ قَوْمِهِ كَانَ يَحْذَرُ

Basi, wakamwambia Munshi Muhammad Yusuf kwamba hatuoni heri katika mjadala kama huu na katika kuweka dakika ishirini; lakini yeye akawaogopa watu wake.

هُنَاكَ دَعَوْا رَبًّا كَرِيْمًا مُّؤَيِّدًا        وَ قَالُوْا حَلَلْنَا اَرْضَ رُجْزٍ فَنَصْبِرُ

Ndipo wakamwomba Mola Karimu Msaidizi, na wakasema, tumeingia ardhi hii chafu, basi tunasubiri.

فَمَا بَرِحُوْهَا وَ الرِّمَاحُ تَنُوْشُهُمْ        وَ لَا طَعْنَ رُمْحٍ مِثْلَ طَعْنٍ يُكَرَّرُ

Kwa hiyo hawakuondoka ardhi hii ilhali mikuki ilikuwa ikiwachoma, na hakuna mkuki uliokuwa kama masingizio yakaririwayo.

وَ قَامَ ثَنَاءُ اللّٰهِ فِي الْقَوْمِ وَاعِظًا        فَصَارُوْا بِوَعْظِ الْغُوْلِ قَوْمًا تَنَمَّرُوْا

Na Thana’ullah akainuka, akawatolea watu waadhi, basi kwa mawaidha ya mtu katili wakawa kama chui.

وَ ذَكَّرَهُمْ صَحْبِيْ مُكَافَاتَ كُفْرِهِمْ        وَ هَلْ يَنْفَعَنْ اَهْلَ الْهَوٰى مَا يُذَكَّرُ

Na marafiki zangu wakawakumbusha adhabu ya kukataa, lakini nasaha yoyote yawezaje kuwanufaisha wafuatao matamanio yao?

تَجَنّٰى عَلَيَّ ابُو الْوَفَاءِ ابْنُ الْهَوٰى        لِيُبْعِدَ حُمْقٰى مِنْ جَنَايَ وَ يَزْجُرُ

Thana’ullah mpenda matamanio yake akaanza kunikosoa ili kuwanyima wajinga tunda langu.

وَ خَاطَبَ مَنْ وَّافَاهُ فِيْ اَمْرِ دَعْوَتِيْ          وَ قَالَ يَمِيْنُ اللّٰهِ مَكْرٌ تَخَيَّرُوْا

Na kila aliyemjia, akaongea naye kuhusu madai yangu na akasema, wallahi, hii ni hila waliyojichagulia.

وَ اَقْسَمَ بِاللّٰهِ الْغَيُوْرِ مُكَذِّبًا          فَيَا عَجَبًا مِّنْ مُّفْسِدٍ كَيْفَ يَجْسُرُ

Na akaapa kwa Mungu Mwenye ghera akikadhibisha; namsikitikia mkorofi jinsi anavyojasiri.

فَطَائِفَةٌ قَدْ كَفَّرُوْنِيْ بِوَعْظِهٖ          وَ طَائِفَةٌ قَالُوْا كَذُوْبٌ يُّزَوِّرُ

Basi, kundi moja likanikufurisha kwa kusikia mawaidha yake, na kundi lingine likasema mtu huyu yu mwongo, anaongopa,

وَ مَا مَسَّهٗ نُوْرٌ مِّنَ الْعِلْمِ وَ الْهُدٰى          فَيَا عَجَبًا مِّنْ بَقَّةٍ يَّسْتَنْسِرُ

Ilhali Thana'ullah hana hadhi ya nuru ya elimu na mwongozo, basi nashangaa juu ya mbu huyu anayetaka kuwa tumbusi.

فَلَمَّا اعْتَدٰى وَ احَسَّ صَحْبِيْ اَنَّهٗ          يُصِرُّ عَلٰى تَكْذِيْبِهٖ لَا يُقَصِّرُ

Basi, alipopita mipaka na marafiki zangu wakaelewa kwamba anang'ang'ania kukadhibisha na hajizuii,

دَعَوْهُ لِيَبْتَهِلَنْ لِمَوْتِ مُزَوِّرٍ          مُضِلٍّ فَلَمْ يَسْكُتْ وَ لَمْ يَتَحَسَّرُ

Wakamwita ili aombe kwa kujinyenyekeza kifo cha mwongo [33] anayewapoteza watu, lakini Thnau'llah hakunyamaza wala hakuchoka.

[33] Nilisema hivyo kwa kumwona Thana'ullah kupita mipaka katika kukadhibisha, na kumwona pia akijigamba kwa hayo. Mwandishi

وَ كَذَّبَ اِعْجَازَ الْمَسِيْحِ وَ اٰيَهُ    وَ غَلَّطَهُ كِذْبًا وَّ كَانَ يُزَوِّرُ

Na akakiita kitabu changu *I'jazul Masih* kuwa uongo na akakadhibisha ishara ya ufasaha wake, na akakiita kwa njia ya uongo kuwa ni chenye makosa na akaongopa.

وَ قِيْلَ لِاِمْلَاءِ الْكِتَابِ كَمِثْلِهِ    فَقَالَ كَاَهْلِ الْعُجْبِ اِنِّيْ سَاَسْطُرُ

Hivyo, akaambiwa aandike kitabu mfano wa *I'jazul Masih*, basi akasema kwa kujigamba nitaandika.

وَ اَنْكَرَ اٰيَاتِيْ وَ اَنْكَرَ دَعْوَتِيْ    وَ اَنْكَرَ اِلْهَامِيْ وَ قَالَ مُزَوِّرُ

Na akakana ishara zangu na kukataa mwito wangu, na akakanusha ufunuo wangu na akasema yu mtu mwongo.

وَ كَذَّبَنِيْ بِالْبُخْلِ مِنْ كُلِّ صُوْرَةٍ    وَ خَطَّأَنِيْ فِيْ كُلِّ وَعْظٍ اُذَكِّرُ

Na akanikadhibisha kwa kila hali, na akanikosoa kwa kila waadhi niliotoa.

فَاُفْرِدْتُّ اِفْرَادَ الْحُسَيْنِ بِكَرْبَلَا    وَ فِي الْحَيِّ صِرْنَا مِثْلَ مَنْ كَانَ يُقْبَرُ

Hivyo, nikabaki peke yangu hapo kama Husain[ra] katika ardhi ya Karbala, na baina ya watu hawa tukawa kama mfu anayezikwa.

تَصَدّٰى لِاِنْكَارِيْ وَ اِنْكَارِ آيَتِيْ    وَ كَانَ لِحِقْدٍ كَالْعَقَارِبِ يَأْبُرُ

Akajitokeza kwa kunikataa na kukanusha ishara zangu, na kwa sababu ya chuki akauma kama nge.

فَقَدْ سَرَّنِیْ فِیْ هٰذِهِ الصُّوْرِ صُوْرَةٌ    لِیَدْفَعَ رَبِّیْ كُلَّمَا كَانَ یَحْشُرُ[34]

Hivyo, katika hali hizi nikaona njia moja nzuri, ili Mola wangu Aondoe dhoruba aliyoibua.

فَأَلَّفْتُ هٰذَا النَّظْمَ اَعْنِیْ قَصِیْدَتِیْ    لِیُخْزِیَ رَبِّیْ كُلَّ مَنْ كَانَ یَهْذِرُ

Basi, nilitunga shairi hili, yaani kasida yangu hii, ili Mungu awadhalilishe wanaopayuka.

وَ هٰذَا عَلٰی اِصْرَارِهٖ فِیْ سُؤَالِهٖ    فَكَیْفَ بِهٰذَا السُّؤْلِ اُغْضِیْ وَ اَنْهَرُ

Na kasida hii imetungwa kwani alisisitiza kushindana, kwa hiyo nisijalije ombi lake hilo na nimkemeeje mwombaji!

وَ لَیْسَ عَلَیْنَا فِی الْجَوَابِ جَرِیْمَةٌ    فَنَهْدِیْ لَهٗ كَالْاٰكِلِ مَا كَانَ یَبْذُرُ

Na hatukufanya dhambi kutoa jibu hili, na tunampa kama zawadi matunda ya alichokipanda.

فَاِنْ اَكُ كَذَّابًا فَیَأْتِیْ بِمِثْلِهَا    وَ اِنْ اَكُ مِنْ رَّبِّیْ فَیُغْشٰی وَ یُثْبَرُ

Basi, ikiwa mimi ni mwongo, basi atatunga kasida kama hii, na kama nimetoka kwa Mungu, basi ufahamu wake utafifia na atazuiliwa.

وَ هٰذَا قَضَاءُ اللّٰهِ بَیْنِیْ وَ بَیْنَهُمْ    لِیُظْهِرَ اٰیٰتِهٖ وَ مَا كَانَ یُخْبِرُ

Na huu ndio uamuzi wa Mwenyezi Mungu baina yetu na baina yao, ili Azidhihirishe ishara zake, na Adhihirishe ishara hii iliyobashiriwa hapo kabla.

---

[34] هٰذَا الشِّعْرُ مِنْ وَحْیِ اللّٰهِ تَعَالٰی جَلَّ شَأْنُهٗ yaani, ubeti huu ndio wahyi kutoka kwa Mwenyezi Mungu, Mwenye adhama kubwa.

قَطَعْنَا بِهٰذَا دَابِرَ الْقَوْمِ كُلِّهِمْ          وَ غَادَرَهُمْ رَبِّیْ كَغُصْنٍ تُجَذَّرُ

Sisi tumekata mzizi wa wote hao kwa njia ya ishara hii, na Mola wangu Amewafanya kama matawi yanayokatwa.

اَرٰی اَرْضَ مُدٍّ قَدْ اُرِیْدَ تَبَارُهَا          وَ غَادَرَهُمْ رَبِّیْ كَغُصْنٍ تُجَذَّرُ

Naiona ardhi ya Mudd kwamba maangamizi yake yamekaribia, na Mola wangu Akawafanya kama tawi lililokatwa.

اَ یَا مُحْسِنِیْ بِالْحُمْقِ وَ الْجَهْلِ وَ الرُّغَا          رُوَیْدَكَ لَا تُبْطِلْ صَنِیْعَكَ وَ احْذَرُ

Ewe ‘mhisani’ wangu, achana na ujinga na ujahili wako, na kutoa mguno kama ngamia, wala usibatilishe hisani yako, ujihadhari.

اَ تَشْتِمُ بَعْدَ الْعَوْنِ وَ الْمَنِّ وَ النَّدٰی          اَتَنْسٰی نَدٰی مُدٍّ وَّ مَا كُنْتَ تَنْصُرُ

Je, utatoa matusi baada ya kutoa msaada na hisani na msamaha? Je, utasahau msamaha ulioufanya huko Mudd na msaada uliotoa!

تَرٰی كَیْفَ اَغْبَرَتِ السَّمَاءُ بِآیِهَا          اِذَا الْقَوْمُ آذَوْنِیْ وَ عَابُوْا وَ غَبَّرُوْا

Unaona jinsi mbingu ilivyoanza kunyesha mvua kubwa ya ishara waliponiudhi watu na kunilaumu na kusababisha fujo.

فَلَا تَتَخَیَّرْ سُبُلَ غَیٍّ وَّ شَقْوَةٍ          وَ لَا تَبْخَلَنْ بَعْدَ النَّوَالِ وَ فَكِّرُ

Basi, usijichagulie njia ya upotevu na balaa wala usiwe bahili baada ya kutoa na utafakari.

وَ لَا تَأْكُلُوْا لَحْمِیْ بِسَبٍّ وَّ غِیْبَةٍ    وَ لَحْمِیْ بِوَجْهِ الْحِبِّ سَمٌّ مُّدَمِّرُ

Wala usile nyama yangu kwa kutusi na kusengenya; na naapa kwa uso wa Mpendwa Yule kwamba nyama yangu ni sumu ya kufisha.

بِأَجْنِحَةِ الْاَشْوَاقِ جِئْنَا فِنَاءَكُمْ    بِمَا قُدِّمَتْ مِنْكُمْ عَطَایَا فَنَحْضُرُ

Tumekuja nyumbani kwako kwa shauku; tumefika kwa sababu ya hisani zako zilizo juu yetu.

وَ اِنْ كُنْتَ قَدْ سَاءَتْكَ اَمْرُ خِلَافَتِیْ    فَسَلْ مُرْسِلِیْ مَا سَاءَ قَلْبَكَ وَ احْصُرُ

Na kama umeona vibaya ukhalifa wangu, basi Muulize kung'ang'ania Aliyenituma kwamba kwa nini Alifanya hivyo?

اَ تُنْكِرُنِیْ وَ اللّٰهُ نَوَّرَ دَعْوَتِیْ    أَ تَلْعَنُ مَنْ هُوَ مِثْلَ بَدْرٍ مُّنَوَّرُ

Je, unanikana na Mungu Ameangazia madai yangu; je unamlaani mtu anayeangaza kama mwezi?

یُصَدِّقُ اَمْرِیْ كُلُّ مَنْ كَانَ فِیْ السَّمَا    فَمَا اَنْتَ یَا مِسْكِیْنُ اِنْ كُنْتَ تَكْفُرُ

Wote waliopo mbinguni wananisadikisha. Ewe maskini, u kitu gani, ukikataa?

وَ اِنِّیْ قَتِیْلُ الْحِبِّ فَاخْشَوْا قَتِیْلَهُ    وَ لَا تَحْسَبُوْنِیْ مِثْلَ نَعْشٍ یُّنَكَّرُ

Na mimi ni mfia Mpendwa wangu, basi mwogopeni mfia Wake, na msinichukulie kama kilili cha jeneza kilichogeuzwa sura yake kisitambulikane.

اَطُوْفُ لِمَرْضَاةِ الْحَبِيْبِ كَهَائِمٍ وَّ اَسْعٰى وَ اِنِّىْ مُسْتَهَامٌ وَّ مُغْبِرُ

Nazunguka kwa ajili ya radhi ya Mpendwa wangu kama aliyetunduwaa; nami ninakimbia, na ninaduwaa, na nimekuwa mwenye mavumbi kutokana na kukimbia sana.

اَذَابَتْ مُحَبَّتُهُ عِظَامِىْ جَمِيْعَهَا وَ هَبَّتْ عَلٰى نَفْسِىْ رِيَاحٌ تُكَسِّرُ

Upendo wake uliyeyusha mifupa yangu, na upepo wake mkali ulivuma juu ya nafsi yangu, uliokuwa wenye kuivunjilia mbali.

ذَرُوْا حِرْصَ تَفْتِيْشِىْ فَاِنِّىْ مُغَيَّبٌ غُبَارٌ عِظَامِىْ قَدْ سَفَتْهَا صَرَاصِرُ

Achana na hamu ya kuchunguza uhakika wangu kwani nipo mbali na macho yako; mifupa yangu ni vumbi, iliyopeperushwa na upepo mkali.

اِذَا مَا انْقَضٰى وَقْتِىْ فَلَا وَقْتَ بَعْدَهٗ لَدَيْنَا مَعِيْنٌ لَّا يُحَاكِيْهِ اٰخَرُ

Utakapopita wakati wangu, kutakuwa hakuna wakati baada yake, tunayo maji safi yasiyo na kifani.

دُعَاءِىْ حُسَامٌ لَّا يُؤَخَّرُ وَقْعُهٗ وَ صَوْلِىْ عَلٰى اَعْدَاءِ رَبِّىْ مُفَقِّرُ

Dua yangu ni upanga asioweza yeyote kuzuia pigo lake, na shambulio langu dhidi ya maadui wa Mola wangu ni upanga mkali uvunjao uti wa mgongo.

وَ اِنِّىْ اُبَلِّغُ عَنْ مَّلِيْكِىْ رِسَالَةً وَ اِنِّىْ عَلَى الْحَقِّ الْمُنِيْرِ وَ نَيِّرُ

Nami nafikisha ujumbe wa Mfalme wangu, na mimi nipo juu ya haki inayong'aa, nami ndimi jua.

تَصَدّٰی لِنَصْرِ الدِّیْنِ فِیْ وَقْتِ عُسْرَةٍ نَذِیْرٌ مِّنَ الرَّحْمٰنِ فَالْاٰنَ یُنْذِرُ

Mwonyaji mmoja alisimama wakati wa dhiki kutoka kwa Rahmani kusaidia dini, naye sasa anaonya.

مَکِیْنٌ اَمِیْنٌ مُقْبِلٌ عِنْدَ رَبِّهٖ مُخَلِّصُ دِیْنِ الْحَقِّ مِمَّا یُحَسِّرُ

Yu mheshimiwa mwaminiwa machoni pa Mungu, na ndiye anayeiokoa dini katika mikasa inayodhoofisha,

وَ مِنْ فِتَنٍ یُّخْشٰی عَلَی الدِّیْنِ شَرُّهَا وَ مِنْ مِّحَنٍ کَانَتْ کَصَخْرٍ تُکَسِّرُ

Na katika fitina zilizohofiwa, na katika mabalaa yanayovunja kama jiwe.

اُرِیْ اٰیَةً عُظْمٰی وَ جِئْتُ اَرُوْدُکُمْ فَهَلْ فَاتِكٌ اَوْ ضَیْغَمٌ اَوْ اَغْبَرُ

Ninaonyesha ishara kubwa, nami nawatafuteni. Je yupo shujaa yeyote au simba au mbwamwitu.

وَ قَالَ ثَنَاءُ اللّٰهِ لِیْ اَنْتَ کَاذِبٌ فَقُلْتُ لَكَ الْوَیْلَاتُ أَنْتَ سَتُحْسَرُ

Na Maulawii Thana'ullah akaniambia, u mwongo. Nikamwambia, ole wako, muda si mrefu utafanywa rabana.

تَعَالَوْا جَمِیْعًا وَّ انْحِتُوْا اَقْلَامَکُمْ وَ اَمْلُوْا کَمِثْلِیْ اَوْ ذَرُوْنِیْ وَ خَیِّرُوْا

Njooni nyote, zichongeni kalamu zenu na andikeni kama mimi, au niacheni na nifahamuni kuwa mwenye hiari.

وَ اَعْطَیْتُ اٰیَاتٍ فَلَا تَقْبَلُوْنَهَا فَلَا تَلْطَخُوْا اَرْضِیْ وَ بِالْمَوْتِ طَهِّرُوْا

Niliwatoleeni ishara, nanyi hamzikubali; basi msiichafue ardhi yangu, na itakaseni kwa mauti.

وَ خَيْرُ خِصَالِ الْمَرْءِ خَوْفٌ وَّ تَوْبَةٌ    فَتُوْبُوْا اِلَى اللهِ الْكَرِيْمِ وَ اَبْشِرُوْا

Na sifa bora ya mwanadamu ni hofu na toba, basi tubuni kwa Mungu na kuchangamka.

سَئِمْنَا تَكَالِيْفَ التَّطَاوُلِ مِنْ عِدًا    تَمَادَتْ لَيَالِى الْجَوْرِ يَا رَبِّ انْصُرُ

Tulipata uchungu mwingi wa dhuluma kutoka kwa maadui, na mausiku ya dhuluma yakawa marefu; Ee Mola wangu nisaidie.

وَ جِئْنَاكَ كَالْمَوْتٰى فَاَحْيِ اُمُوْرَنَا    نَخِرُّ اَمَامَك كَالْمَسَاكِيْنِ فَاغْفِرُ

Na tumekujia kama wafu, basi yahuishe mambo yetu; tunaanguka mbele yako kama maskini basi tusamehe.

اِلٰهِىْ فَدَتْكَ النَّفْسُ اِنَّكَ جَنَّتِىْ    وَ مَا اَنْ اَرٰى خُلْدًا كَمِثْلِكَ يُثْمِرُ

Ee Mungu, ninajitolea uhai wangu kwako, U Pepo yangu na sijaona Pepo yoyote inayotoa matunda kama Wewe.

طُرِدْنَا لِوَجْهِكَ مِنْ مَّجَالِسِ قَوْمِنَا    فَاَنْتَ لَنَا حِبٌّ فَرِيْدٌ وَّ مُؤْثَرُ

Mola wangu, kwa sababu Yako Wewe tulikataliwa katika vikao vya kaumu yetu; basi, Wewe ndiwe Mpendwa wetu wa pekee Uliyechaguliwa.

اِلٰهِىْ بِوَجْهِكَ اَدْرِكِ الْعَبْدَ رَحْمَةً    وَ لَيْسَ لَنَا بَابٌ سِوَاكَ وَ مَعْبَرُ

Ee Mungu wangu, mjalie rehema mtumishi wako kwa hisani Yako, nasi hatuna mlango wowote minghairi Yako wala njia ya kuendea.

اِلٰی اَیِّ بَابٍ یَا اِلٰھِیْ تَرُدُّنِیْ وَ مَنْ جِئْتُهُ بِالرِّفْقِ یَزْرِ وَ یَصْعَرُ

Mungu wangu, Utanirudisha kwenye mlango wa nani? Yeyote ninayemwendea kwa upole, anadharau na anageuza uso upande mwingine.

صَبَرْنَا عَلٰی جَوْرِ الْخَلَائِقِ کُلِّھِمْ وَ لٰکِنْ عَلٰی ھَجْرٍ سَطَا لَا نَصْبِرُ

Tumevumilia udhalimu wa dunia nzima, lakini hatuweza kuvumilia kuachana Nawe.

تَعَالَ حَبِیْبِیْ اَنْتَ رَوْحِیْ وَ رَاحَتِیْ وَ اِنْ کُنْتَ قَدْ اٰنَسْتَ ذَنْبِیْ فَسَتِّرُ

Njoo Rafiki yangu, U starehe yangu na raha yangu, na kama Umeona dhambi yoyote basi nisitiri.

بِفَضْلِکَ اِنَّا قَدْ عُصِمْنَا مِنَ الْعِدَا وَ اِنَّ جَمَالَكَ قَتَّالِیْ فَأْتِ وَ انْظُرُ

Kwa fadhili yako tulikingwa na maadui, lakini uzuri Wako umetuua, Njoo, basi, Ukaone.

وَ فَرِّجْ کُرُوْبِیْ یَا اِلٰھِیْ وَ نَجِّنِیْ وَ مَزِّقْ خَصِیْمِیْ یَا نَصِیْرِیْ وَ عَفِّرُ

Na niondolee huzuni yangu, Ee Mungu wangu, na niokoe; na Ee Msaidizi wangu wavunje adui vipande-vipande adui yangu na mdhalilishe.

وَجَدْنَاكَ رَحْمَانًا فَمَا الْھَمُّ بَعْدَهٗ رَأَیْنَاكَ یَا حِبِّیْ بِعَیْنٍ تُنَوَّرُ

Tukakukuta Mwingi wa rehema, basi baada yake haikubaki huzuni yoyote. Tukakuona, Ee Mpendwa wangu, kwa jicho linalong'arishwa.

اَنَا الْمُنْذِرُ الْعُرْيَانُ يَا مَعْشَرَ الْوَرٰى    اُذَكِّرُكُمْ اَيَّامَ رَبِّیْ فَاَبْصِرُوْا

Enyi watu, mimi ni mwonyaji wazi, nawakumbusheni siku za *adhabu* za Mungu; basi tazameni.

بَلَاءٌ عَلَيْكُمْ وَ الْعِلَاجُ اِنَابَةٌ    وَ بِالْحَقِّ اَنْذَرْنَا وَ بِالْحَقِّ نُنْذِرُ

Kuna balaa juu yenu, na tiba yake ni kutubu na kujiepusha na kila dhambi. Tumeshaonya barabara, na tunaendelea kuonya kikweli-kweli.

دَعُوْا حُبَّ دُنْيَاكُمْ وَ حُبَّ تَعَصُّبٍ    وَ مَنْ يَّشْرَبِ الصَّهْبَاءَ يُصْبِحْ مُسَكَّرُ

Acheni mapenzi ya dunia na kupenda chuki; na atakayeinywa mvinyo usiku, atapatwa na shida ya kulewa asubuhi.

وَ كَمْ مِّنْ هُمُوْمٍ قَدْ رَأَيْنَا لِاَجْلِكُمْ    وَ نَضْرَمُ فِیْ الْقَلْبِ اضْطِرَامًا وَّ نَضْجَرُ

Na huzuni nyingi zilioje tulizopata kwa ajili yenu, na bado moyoni mwetu mna moto kwa ajili yenu tunaoficha.

اَصِيْحُ وَ قَدْ فَاضَتْ دُمُوْعِیْ تَاَلُّمًا    وَ قَلْبِیْ لَكُمْ فِیْ كُلِّ اٰنٍ يُوَغَّرُ

Ninalia na machozi yangu yanachurukiza kwa maumivu, na moyo wangu unatiliwa sana uchungu kila saa kwa ajili yenu.

فَسَلْ اَيُّهَا الْقَارِیْ اَخَاكَ اَبَا الْوَفَا    لِمَا يَخْدَعُ الْحَمْقٰى وَ قَدْ جَاءَ مُنْذِرُ

Basi, ewe msomaji mwulize ndugu yako Thana'ullah, kwa nini anawadanganya wajinga, na mwonyaji amekwishafika tayari.

اَلَا رُبَّ خَصْمٍ قَدْ رَأَيْتُ جِدَالَهُ وَ مَا إِنْ رَأَيْنَا مِثْلَهُ مَنْ يُّزَوِّرُ

Habedari, nimeona wabishi wengi, lakini sijamuona laghai kama yeye.

عَجِبْتُ لِمَبْحَثِهِ اِلٰى ثُلْثِ سَاعَةٍ اَ كَانَ مَحَلُّ الْبَحْثِ اَوْ كَانَ مَيْسِرُ

Nilishangaa kwamba aliweka dakika ishirini kwa majadiliano. Je, hayo yalikuwa majadiliano au kucheza kamari?

اَ مُكْفِرِ مَهْلًا كُلَّمَا كُنْتَ تَذْكُرُ وَ اَمْلِ كَمِثْلِيْ ثُمَّ اَنْتَ مُظَفَّرُ

Ewe unayenikufurisha, yaache yote yaliyopita, na andika kasida mfano wa kasida yangu. ndipo utakuwa mshindi.

رَضِيْتُ بِاَنْ تَخْتَارَ فِي النَّمْقِ رُفْقَةً وَ اِنَّا عَلٰى اِمْلَاءِهِمْ لَا نُعَيِّرُ

Nimekubali hii pia kwamba, *ukishindwa,* jichagulie marafiki zako kwa kutunga, nasi hatutakusuta kwa sababu ya wao kuandika.

فَمَا الْخَوْفُ فِيْ هٰذَا الْوَغَا يَا اَبَا الْوَفَا لِيُمْلِ حُسَيْنٌ اَوْ ظَفَرْ اَوْ اَصْغَرُ

Basi, ewe Thana’ullah, unaogopa nini katika vita hii, kwamba Muhammad Husain aandike jibu au Kazi Dhafaruddin au Asghar Ali.

وَ اِنِّيْ اَرٰى فِيْ رَأْسِهِمْ دُوْدَ نَخْوَةٍ فَاِنْ شَاءَ رَبِّيْ يُخْرِجَنَّ وَ يَجْذُرُ

Nami naona wadudu wa kiburi kichwani mwao, na Mwenyezi Mungu akitaka atatoa wadudu hao na kuwang'olea mbali.

وَ اِنْ كَانَ شَأْنُ الْاَمْرِ اَرْفَعَ عِنْدَكُمْ      فَاَيْنَ بِهٰذَا الْوَقْتِ مَنْ شَانَ جَوْلَرُ

Na kama unafikiri kazi hii inazidi uwezo wa hao watu, basi yuko wapi Meher Ali Shah wakati huu aliyeiaibisha Golara?

اَمَيْتٌ بِقَبْرِ الْغَيِّ لَا يَنْبَرِىْ لَنَا      وَ مَنْ كَانَ لَيْثًا لَا مَحَالَةَ يَزْئَرُ

Je yu mfu, hatajitokeza sasa; na aliye simba hana budi kunguruma.

وَ اِنْ كَانَ لَا يَسْطِيْعُ اِبْطَالَ اٰيَتِىْ      فَقُلْ خُذْ مَزَامِيْرَ الضَّلَالَةِ وَ ازْمُرُ

Na kama hawezi kubatilisha ishara yangu hii, basi mwambie ashike kazi ya kupiga zumari, anahusikaje na elimu!

اَ غَلَّطَ اِعْجَازِىْ حُسَيْنٌ بِعِلْمِهٖ      وَ هَيْهَاتَ مَاحَوْلُ الْجُهُوْلِ أَتَسْخَرُ

Je Muhammad Husain alikosoa kitabu changu *I'jazul Masih*? Hawezi kabisa; anawezaje Muhammad Husain. Je unafanya masihara?

وَ اِنْ كَانَ فِىْ شَىْءٍ بِعِلْمٍ حُسَيْنُكُمْ      فَمَا لَكَ لَا تَدْعُوْهُ وَ الْخَصْمُ يَحْصُرُ

Na kama Muhammad Husain wenu ni kitu chochote, kwa nini humwiti ilhali adui anasuta sana.

وَ نَحْسَبُهٗ كَالْحُوْتِ فَأْتِ بِنَظْمِهٖ      مَتٰى حَلَّ بَحْرًا نَقْتَنِصُهٗ وَ نَأْسِرُ

Na tunamwona kama ni samaki; basi lilete shairi lake; atakapoingia katika bahari yoyote tutamvua na kumkamata.

وَ اِنْ يَّأْتِنِىْ اَصْبَحْهُ كَأْسًا مِنَ الْهُدٰى      فَاَحْضِرْهُ لِلْاِمْلَاءِ اِنْ كَانَ يَقْدِرُ

Kama akija kwangu, nitamnywesha asubuhi ile kikombe cha mwongozo basi umhudhurishe kuandika ikiwa anao uwezo wa kuandika.

اِذَا مَا ابْتَلَاهُ اللهُ بِالْاَرْضِ سُخْطَةً      بِلَائِلَ قَالُوْا مُكْرَمٌ وَّ مُعَزَّزُ

Mungu Alipomjaribu kumpa ardhi huko Lyallpur kama karaha, wapinzani wakasema ana heshima na jaha.

وَ مَا الْعِزُّ اِلَّا بِالتَّوَرُّعِ وَ التُّقٰى      وَ بُعْدٍ مِّنَ الدُّنْيَا وَ قَلْبٍ مُّطَهَّرُ

Na heshima huwa kwa kumcha Mungu na kwa kujitenga na dunia na kujitakasa moyo.

وَ اِنَّ حَيَاةَ الْغَافِلِيْنَ لَذِلَّةٌ      فَسَلْ قَلْبُهُ زَادَ الصَّفَا اَوْ تَكَدَّرُ

Na maisha ya walioghafilika ni dhila, basi muulize kama moyo wake ni safi kuliko hapo kabla au umechafuka kwa uchafu wa dunia.

اِذَا نَحْنُ بَارَزْنَا فَاَيْنَ حُسَيْنُكُمْ      وَ اِنْ كُنْتَ تَحْمَدُهُ فَاَعْلِنْ وَ اَخْبِرُ

Tutakapoingia medanini, Muhammad Husain wako atakuwa wapi, na ikiwa unamsifu, basi umhabarishe.

اَ تَحْسَبُهُ حَيًّا وَ تَاللهِ اِنَّنِىْ      اَرَاهُ كَمَنْ يُّدْفٰى وَ يُفْنٰى وَ يُقْبَرُ

Je unamfikiria kuwa hai, nami Wallahi namwona kama mfu, aliyekufa na kuzikwa kaburini.

وَ لَوْ شَاءَ رَبِّيْ كَانَ يَبْغِيْ هِدَايَتِيْ    وَ لَوْ شَاءَ رَبِّيْ كَانَ مِمَّنْ يُبَصَّرُ

Na lau kama Mola wangu Angetaka, angekubali mwongozo; na lau kama Mola wangu Angetaka, angenitambua.

وَ مَا اِنْ قَنَطْنَا وَ الرَّجَاءُ مُعَظَّمٌ    كَذٰلِكَ وَحْيُ اللّٰهِ يُدْرِيْ وَ يُخْبِرُ

Na hatujakata tamaa na imani yake bali kuna matumaini makubwa; ndivyo wahyi wa Mungu unavyohabarisha.

وَ اِنَّ قَضَاءَ اللّٰهِ مَا يُخْطِئُ الْفَتٰى    لَهٗ خَافِيَاتٌ لَّا يَرَاهَا مُفَكِّرُ

Na hukumu ya Mungu haimsahau mja mwema, kuna siri zake asiweze kuziona hata mwenye kufikiria.

سَيُبْدِيْ لَكَ الرَّحْمٰنُ مَقْسُوْمَ حِبِّكُمْ    سَعِيْدٌ فَلَا يُنْسِيْهِ يَوْمٌ مُّقَدَّرُ

Mwenyezi Mungu Atakudhihirishia bahati ya rafiki yako Muhammad Husain; kama yu mwenye bahati njema, basi siku ya hesabu Mungu Hatamsahau.

وَ يُحْيٰى بِاَيْدِي اللّٰهِ وَاللّٰهُ قَادِرٌ    وَ يَأْتِيْ زَمَانُ الرُّشْدِ وَ الذَّنْبُ يُغْفَرُ

Na atahuishwa kwa Mikono ya Mungu, na Mungu Yu Mweza; na zama za mwongozo zitawadia na dhambi itasamehewa.

فَيَسْقُوْنَهٗ مَآءَ الطَّهَارَةِ وَ التُّقٰى    نَسِيْمُ الصَّبَا تَأْتِيْ بِرَيَّا يُّعَطِّرُ

Basi, watamnywesha maji ya utakaso na takwa, na upepo wa matlai utaleta mnukio na kutia marashi.

وَ اِنَّ كَلَامِیْ صَادِقٌ قَوْلُ خَالِقِیْ     وَ مَنْ عَاشَ مِنْكُمْ بُرْهَةً فَسَيَنْظُرُ

Na kauli yangu ni kweli, ni kauli ya Mungu wangu; na atakayeishi miongoni mwenu kwa muda kidogo ataona.

اَ تَعْجَبُ مِنْ هٰذَا فَلَا تَعْجَبَنْ لَّهٗ     كَلَامٌ مِّنَ الْمَوْلٰى وَ وَحْیٌ مُّطَهَّرُ

Je, unastaajabia hii? Usistaajabie, hii ni kauli ya Mungu na ni wahyi mtakatifu.

وَ مَا قُلْتُهٗ مِنْ عِنْدِ نَفْسِیْ كَرَاجِمٍ     أُرِيْتُ وَ مِنْ اَمْرِ الْقَضَا اَتَحَيَّرُ

Nami sikulonga haya kwa kubahatisha, bali nilionyeshwa katika kashfi nami ninashangaa.

اَ قَلْبُ حُسَيْنٍ يَّهْتَدِیْ مَنْ يَّظُنُّهٗ     عَجِيْبٌ وَّ عِنْدَ اللهِ هَيْنٌ وَّ اَيْسَرُ

Je moyo wa Muhammad Husain utapata kuongoka; nani aweza kudhania? Ni la ajabu hili; lakini ni rahisi na jepesi kwa Mungu.

ثَلٰثَةُ اَشْخَاصٍ بِهٖ قَدْ رَاَيْتُهُمْ     وَ مِنْهُمْ اِلٰهِیْ بَخْش فَاسْمَعْ وَ ذَكِّرُ

Nimeona watu watatu wengine wapo pamoja naye; miongoni mwao yupo Ilahi Bakhsh, Mhasibu wa Multani; basi usikilize na kusikilizisha.

لَعَمْرُكَ ذُقْنَا دُوْنَ ذَنْبٍ رِمَاحَهُمْ     فَمَا سَرَّنَا اِلَّا دُعَاءٌ يُّكَرَّرُ

Kwa kiapo cha maisha yako, tulionja ladha ya mikuki yao pasipo dhambi yoyote; basi tuliona vyema kuendelea kuwaombea.

مَتٰی ذُکِّرُوْا یَغْتَمُّ قَلْبِیْ بِذِکْرِھِمْ        بِمَا کَانَ وَقْتٌ بِالْمُلَا قَاۃِ نُبْشِرُ

Wanapotajwa, moyo wangu huhuzunika kwa sababu nakumbuka wakati fulani tulipokuwa tukifurahi kukutana.

أَ اُرْضِعْتَ مِنْ غُوْلِ الْفَلَا یَا اَبَا الْوَفَا        فَمَا لَکَ لَا تَخْشٰی وَ لَا تَتَفَکَّرُ

Ewe Thana'ullah, je ulinyonyeshwa uongo? Umekuwaje, huogopi wala hufikiri.

تَرَکْتُمْ سَبِیْلَ الْحَقِّ وَ الْخَوْفِ وَ الْحَیَا        وَ جُزْتُمْ حُدُوْدَ الْعَدْلِ وَ اللّٰہُ یَنْظُرُ

Umeiacha haki[35] na ukairuka mipaka ya uadilifu, na Mwenyezi Mungu Anaona.

وَکَیْفَ تَرٰی نَفْسٌ حَقِیْقَۃَ وَحْیِنَا        یُصِرُّ عَلٰی کِذْبٍ وَّ بِالسُّوْءِ یَجْھَرُ

Anatambuaje hakika ya wahyi wetu mtu anayeung'ang'ania uongo na kusingizia hadharani.

وَ اِنْ کُنْتُ کَذَّابًا کَمَا ھُوَ زَعْمُکُمْ        فَکِیْدُوْا جَمِیْعًا لِّیْ وَ لَا تَسْتَأْخِرُوْا

Na kama mimi ni mwongo kwenu, basi jaribuni nyote pamoja kuniangamiza wala msirudi nyuma.

وَ اِنَّ ضِیَائِیْ یَبْلُغُ الْاَرْضَ کُلَّھَا        اَ تُنْکِرُھَا فَاسْمَعْ وَ اِنِّیْ مُذَکِّرُ

Na nuru yangu itaenea kote ardhini. Je unakataa? Basi isikilize vizuri, nami nakukumbusha.

[35] Katika ubeti huu sehemu fulani ya tafsiri imeachika. Tafsiri kamili itakuwa hivi: "Umeiacha njia ya haki, hofu na haya." Mwenezi

عَقَرْتَ بِمُدٍّ صُحْبَتِیْ یَا اَبَا الْوَفَا بِسَبٍّ وَّ تَوْهِیْنٍ فَرَبِّیْ سَیَقْهَرُ

Ewe Thana'ullah, uliwaudhi marafiki zetu huko Mudd, kwa kutusi na kufedhehesha; basi si muda mrefu Mola wangu Atashinda.

جَلَالَكَ رَبِّیْ اَبْتَغِیْ لَا جَلَالَتِیْ وَ اَنْتَ تَرٰی قَلْبِیْ وَ عَزْمِیْ وَ تُبْصِرُ

Ewe Mola wangu, nataka utukufu Wako, sio utukufu wangu; nawe Unaona moyo wangu na kusudi langu.

اِلَیْكَ اَرُدُّ مَحَامِدِیْ رُدْتُّ كُلَّهَا وَ مَا اَنَا اِلَّا مِثْلُ ذَرْقٍ یُّعَفَّرُ

Nazielekeza kwako sifa zote ninazozikusudia, na mimi si chochote ila kama mavi ya ngombe yafunikwayo na udongo.

وَ قَالُوْا عَلَی الْحَسْنَیْنِ فَضَّلَ نَفْسَهٗ اَقُوْلُ نَعَمْ وَ اللّٰهُ رَبِّیْ سَیُظْهِرُ

Na wakasema kwamba mtu huyu alijiona bora kuliko Imam Hasan na Husain; nasema, naam, na Mungu, Mola wangu Ataidhihirisha hivi punde.

وَ لَوْ كُنْتُ كَذَّابًا لَمَا كُنْتُ بَعْدَهٗ كَمِثْلِ یَهُوْدِیٍّ وَّ مَنْ یَّتَنَصَّرُ

Na kama ningekuwa mwongo, basi baada ya hapo nisingekuwa hata kama Myahudi na yule aliyetanasari.

وَ لٰكِنَّنِیْ مِنْ اَمْرِ رَبِّیْ خَلِیْفَةٌ مَسِیْحٌ سَمِعْتُمْ وَعْدَهٗ فَتَفَكَّرُوْا

Lakini mimi ni Khalifa kwa amri ya Mungu wangu, na Masihi Mau'udi; basi zingatieni.

فَمَا شَأْنُ مَوْعُوْدٍ وَّ مَا فِيْهِ عِنْدَكُمْ    مِنَ الْقَوْلِ قَوْلِ نَبِيِّنَا فَتَدَبَّرُوْا

Basi, Masihi Mau'udi ana utukufu gani, na mnayo kauli gani ya Mtume[saw] kumhusu yeye? Fikirini basi.

حَدِيْثٌ صَحِيْحٌ عِنْدَكُمْ تَقْرَءُوْنَهٗ    فَلَا تَكْتُمُوْا مَا تَعْلَمُوْنَ وَ اَظْهِرُوْا

Mnayo Hadithi Sahihi mnayoisoma; basi msifiche mnayoyajua na yadhihirisheni.

وَ مَنْ يَّكْتُمَنَّ شَهَادَةً كَانَ عِنْدَهٗ    فَسَوْفَ يَرٰى تَعْذِيْبَ نَارٍ تُسَعَّرُ

Na atakayeficha ushahidi alionao, basi hivi punde ataona adhabu ya moto utakaowashwa.

فَلَا تَجْعَلُوْا كِذْبًا عَلَيْكُمْ عُقُوْبَةً    وَ دَعْ يَا ثَنَاءَ اللّٰهِ قَوْلًا تُزَوِّرُ

Basi, msiufanye uongo kuwa sababu ya kuadhibiwa kwenu. Na Ewe Thana'ullah, achana na kusema uongo.

تَرَكْتَ طَرِيْقَ كِرَامِ قَوْمٍ وَّ خُلْقَهُمْ    هَجَوْتَ بِمُدٍّ عَامِدًا لِّتُحَقِّرُ

Uliachana na njia ya waungwana wa kaumu na hulka zao, na ulitukashifu makusudi kijijini Mudd ili kutuhakirisha.

وَ شَتَّانَ مَا بَيْنَ الْكِرَامِ وَ بَيْنَكُمْ    وَ اِنَّ الْفَتٰى يَخْشَى الْحَسِيْبَ وَ يَحْذَرُ

Tofauti kubwa ilioje baina yenu na waungwana! Mtu mwema humcha Mungu na kujitahadhari.

تَرَكْنَاكَ حَتّٰى قِيْلَ لَا يَعْرِفُ الْقِلٰى    فَجِئْتَ خَصِيْمًا اَيُّهَا الْمُسْتَكْبِرُ

Tulikuacha tu mpaka mkasema mbona huandiki chochote sasa? Basi, umekuja mwenyewe kupigana, ewe mwenye kiburi.

اَلَا اَيُّهَا اللَّعَّانُ مَالَكَ تَهْجُرُ وَ تَلْعَنُ مَنْ هُوَ مُرْسَلٌ وَّ مُوَقَّرُ

Ewe mlaanizi, mbona unapayuka na unamlaani aliyetumwa na Mungu na aliyejaliwa heshima Naye.

شَتَمْتَ وَ مَا تَدْرِىْ حَقِيْقَةَ بَاطِنِىْ وَ كُلُّ امْرِءٍ مِّنْ قَوْلِهٖ يُسْتَفْسَرُ

Umenitukana na hujui hali yangu; na kila mtu ataulizwa kuhusu kauli yake.

صَبَرْنَا عَلٰى سبٍّ بِهٖ آذَيْتَنَا وَ لٰكِنْ عَلٰى مَا تَفْتَرِىْ لَا نَصْبِرُ

Tumevumilia matusi uliyotuumiza kwayo mioyo yetu, lakini hatuwezi kuyavumilia uliyotuzushia.

وَ وَاللّٰهِ اِنِّىْ صَادِقٌ لَسْتُ كَاذِبًا فَلَا تَهْلِكُوْا مُسْتَعْجِلِيْنَ وَ فَكِّرُوْا

Na Wallahi, mimi ni mkweli, si mwongo, kwa hiyo msiangamie kwa kufanya haraka na tafakarini kwa makini.

وَ لَوْ كُنْتُ كَذَّابًا شَقِيًّا لَضَرَّنِىْ عَدَاوَةُ قَوْمٍ كَذَّبُوْنِىْ وَ كَفَّرُوْا

Na lau kama ningekuwa kadhabu mwenye bahati mbaya, ungenidhuru uadui wa watu walionikadhibisha na kunikufurisha.

وَ شَاهَدْتَّ اَنَّ الْقَوْمَ كَيْفَ تَدَاكَئُوْا عَلَيَّ وَ كَيْفَ رَمَوْا سِهَامًا وَّ جَمَّرُوْا

Nawe ukaona jinsi watu walivyofanya fujo dhidi yangu na namna walivyonirushia mishale, na kujumuika dhidi yangu.

رَمَوْا كُلَّ صَخْرٍ كَانَ فِيْ اَذْيَالِهِمْ    بِغَيْظٍ فَلَمْ اَقْلَقْ وَ لَمْ اَتَحَيَّرُ

Wakatupa mawe yote yaliyokuwa nayo, na walifanya hivyo kwa hasira, kwa hiyo sikufadhaika wala kushangaa.

وَ جُرِّحَ عِرْضِيْ مِنْ رِمَاحِ اِهَانَةٍ    وَ اُلْقِيْ مِنْ سَبٍّ اِلَيَّ الْخَنْجَرُ

Na heshima yangu ilijeruhiwa kwa ‘mikuki’ ya matusi, na nikatupiwa ‘hanjari’ ya matukano.

وَ قَالُوْا كَذُوْبٌ مُّفْتِنٌ غَيْرُ صَادِقٍ    فَقُلْنَا اخْسَئُوْا اِنَّ الْخَفَايَا سَتَظْهَرُ

Na wakasema yu mwongo, mzushi, si mkweli. Nasi tukasema, tokeni nyote, hatimaye ukweli huu uliofichika utadhihirika.

وَ سَبُّوْا وَ اٰذَوْنِيْ بِاَنْوَاعِ سَبِّهِمْ    وَ سَمَّوْنِ دَجَّالًا وَّ سَمَّوْنِ اَبْتَرُ

Walinitukana na wakaniudhi kwa matukano ya aina aina na wakaniita dajali na wakaniita mtu asiye na heri yoyote.

وَ سَمَّوْنِ شَيْطَانًا وَّ سَمَّوْنِ مُلْحِدًا    وَ سَمَّوْنِ مَلْعُوْنًا وَّ قَالُوْا مُزَوِّرُ

Na wakaniita shetani na wakaniita mkana mungu, na wakaniita maluuni, na wakasema yu mtu mwongo.

فَصِرْتُ كَاَنِّيْ لِلرِّمَاحِ دَرِيَّةٌ    وَ اُوْذِيْتُ حَتّٰى قِيْلَ عَبْدٌ مُّحَقَّرُ

Basi nikawa kama shabaha ya mikuki. Nikaudhiwa mpaka ikasemwa yu mtu hakiri sana.

وَ مَا غَادَرُوْا كَيْدًا لِّدَوْسِيْ وَ بَعْدَهٗ    عَلَيَّ حَضَوْا زَمْعَ الْاُنَاسِ وَ ثَوَّرُوْا

Na wakatumia kila njia ya kunikanyagilia mbali, kisha wakawachochea waovu dhidi yangu na kuwakasirisha.

وَ لٰكِنْ مَآلُ الْاَمْرِ كَانَ هَوَانُهُمْ    وَ اُنْزِلَ لِيْ آيٌ تُنِيْرُ وَ تَبْهَرُ

Lakini hatimaye wakafedheheka, na kwa ajili yangu ishara angavu, zishindazo zikadhihirishwa.

فَأُوْصِيْكَ يَا رِدْفَ الْحُسَيْنِ اَبَا الْوَفَا    اَنِبْ وَ اتَّقِ اللّٰهَ الْمُحَاسِبَ وَ احْذَرُ

Kwa hiyo ninakunasihi, ewe Thana'ullah umfuataye Muhammad Husain, utubu na umwogope Mungu Atakayekutaka hesabu, na ujitahadhari.

وَ لَا تُلْهِكَ الدُّنْيَا عَنِ الدِّيْنِ وَ الْهَوٰى    وَ اِنَّ عَذَابَ اللّٰهِ اَدْهٰى وَ اَكْبَرُ

Wala dunia na matamanio ya nafsi yasikuzuie kufuata dini; na adhabu ya Mwenyezi Mungu ni kali na kubwa.

وَ لَا تَحْسَبِ الدُّنْيَا كَنَاطِفِ نَاطِفِيْ    اَ تَدْرِيْ بِلَيْلِ مَسَرَّةٍ كَيْفَ تُصْبِحُ

Wala usiufikirie ulimwengu kuwa halua inayotayarishwa na mpishi. Je, unajua baada ya usiku wa furaha utaingia asubuhi katika hali gani?

اَلَا تَتَّقِي الرَّحْمٰنَ عِنْدَ تَصَنُّعٍ    وَ مَنْ كَانَ اَتْقٰى لَا اَبَالَكَ يَحْذَرُ

Je, humwogopi Rahmani unapojisingizia; lakini amchaye Mungu lazima anaogopa.

اَلَا لَيْتَ شِعْرِيْ هَلْ تُشَاهِدُ بَعْدَنَا    مَسِيْحًا يَحُطُّ مِنَ السَّمَآءِ وَ يُنْذِرُ

Laiti ungeelewa, je Masihi mwingine utamwona akishuka kutoka mbinguni baada yangu na ataonya?

وَ لِلّٰهِ دَرُّ مُذَكِّرٍ قَالَ اِنَّهٗ    يَعَافُ الْهُدٰى شِكْسٌ زَنِيْمٌ مُّدَعْثَرُ

Na vizuri sana kauli ya mtoaji nasaha aliyesema kwamba mwenye tabia mbaya, mwovu na mwenye kuangamia anachukia mwongozo.

ذَكَرْتَ بِمُدٍّ عِنْدَ بَحْثِكَ بِالْهَوٰى    اَحَادِيْثَ وَ الْقُرْاٰنَ تُلْغِيْ وَ تَهْجُرُ

Ulisema katika majadiliano huko Mudd kwamba tunazo Hadithi hizi, na ukaichukulia Kurani kuwa ni bure tu na batili.

نَبَذْتُمْ كَلَامَ اللّٰهِ خَلْفَ ظُهُوْرِكُمْ    تَرَكْتُمْ يَقِيْنًا لِلظُّنُوْنِ فَفَكِّرُوْا

Mkalitupa Neno la Mwenyezi Mungu nyuma ya migongo yenu na mkaiacha yakini kwa ajili ya dhana.

فَصَارَ كَاٰثَارٍ عَفَتْ وَ تَغَيَّبَتْ    مَدَارُ نَجَاةِ النَّاسِ يَا مُتَكَبِّرُ

Basi Kurani ikawa kama alama zilizofutika, na chimbuko la wokovu likafichika, Ewe mwenye kiburi.

وَ اِنَّ شِفَاءَ النَّاسِ كَانَ بَيَانُهٗ    فَهَلْ بَعْدَهٗ نَحْوَ الظُّنُوْنِ نُبَادِرُ

Na maelezo yake yalikuwa ni ponyo kwa watu; basi je tuiache Kurani na tuzikimbilie dhana?

وَ فَاضَتْ دُمُوْعُ الْعَيْنِ مِنِّيْ تَأَلُّمًا    اِذَا مَا سَمِعْتُ الْبَحْثَ يَا مُتَهَوِّرُ

Basi, machozi yangu yakatiririka kwa sababu ya uchungu niliposikiliza mjadala wako, ewe jeuri.

كَذَبْتَ بِمُدٍّ عَامِدًا فَتَمَايَلَتْ    عَلَيْكَ شَطَايِبُ جَاهِلِيْنَ وَ ثَوَّرُوْا

Ulisema uongo makusudi kijijini Mudd; basi majahili wakakuelekea na kupiga kelele.

وَ وَ اللهِ فِي الْقُرْاٰنِ كُلُّ حَقِيْقَةٍ     وَ آيَاتُهُ مَقْطُوْعَةٌ لَّا تَغَيَّرُ

Na Wallahi ndani ya Kurani Tukufu mna kila ukweli na Aya zake ni za mkataa ambazo hazibadiliki.

مَعِيْنٌ مَّعِيْنُ الْخُلْدِ نُوْرُ مُعِيْنِنَا     هُدَاهُ نَمِيْرُ الْمَاءِ لَا يَتَكَدَّرُ

Ni maji safi *hii Kurani*, maji ya Peponi, nuru ya Msaidizi wetu; mwongozo wake ni maji safi sana siyo machafu.

اَرٰى آيَهٗ كَالْغِيْدِ جَاءَتْ مِنَ السَّمَا     وَ فِيْهَا شِفَاءٌ لِّلَّذِىْ يَتَدَبَّرُ

Aya zake ni nzuri zilizoshuka kutoka mbinguni, na ndani yake ma ponyo kwa wale wanaotafakari katika aya hizi.

وَ يُصْبِىْ قُلُوْبَ النَّاسِ بِالنُّوْرِ وَ الْهُدٰى     وَ يُرْوِى الْعَطَاشٰى بِالْمَعِيْنِ وَ يَظْئَرُ

Na inazivuta nyoyo za watu kwa nuru na mwongozo, na huwatosheleza wenye kiu kwa maji safi, na huwanyonyesha kama mama wa kunyonyesha.

وَ قَدْ كَانَ صُحُفٌ قَبْلَهُ مِثْلَ خَادِجٍ     فَجَاءَ لِتَكْمِيْلِ الْوَرٰى لِيُغَزَّرُ

Na Vitabu vya zamani vilikuwa kama ngamia jike anayezaa kabla ya wakati wake, basi ikaja Kurani kuwakamilisha watu ili maziwa yote yakamuliwe mara moja.

بِلَيْلٍ كَمَوْجِ الْبَحْرِ اَرْخٰى سُدُوْلَهُ     تَجَلّٰى وَ اَدْرٰى كُلَّ مَنْ كَانَ يُبْصِرُ

Ikaja katika usiku uliojitandaza kama mavimbi ya bahari, kuziangaza zama na kumwonyesha kila mtu aliyeweza kuona.

اَ يَا اَيُّهَا الْمُغْوِیْ اَ تُنْكِرُ شَأْنَهُ          وَ مَا فِیْ يَدَيْنَا غَيْرُهُ يَا مُزَوِّرُ

Ewe mpotoshaji, je unakanusha utukufu wa Kurani; na ewe mzushi, mikononi mwetu tuna nini isipokuwa Kurani?

لِقَوْمٍ هَذٰی لَا بَارَكَ اللهُ مُدَّهُمْ          جَهُوْلٌ فَاَدّٰی حَقَّ كِذْبٍ فَاَبْشَرُوْا

Mtu huyu alipayuka kwa ajili ya watu, Mungu Asikibariki kijiji chao Mudd. Mtu huyu ni jahili, akatimiza haki ya kuongopa, basi watu hao wakafurahi.

لَهُ جَسَدٌ لَّا رُوْحَ فِيْهِ وَ لَا صَفَا          كَقِدْرٍ يَّجُوْشُ و لَيْسَ فِيْهِ تَدَبُّرُ

Ni mwili tu huyo, usio na roho ndani mwake, wala usafi; anachemka kama sufuria, asitafakari.

نَبَذْتُمْ هُدَی الْمَوْلٰی وَرَآءَ ظُهُوْرِكُمْ          فَدَعْنِیْ اُبَيِّنْ كُلَّمَا كَانَ يُسْتَرُ

Mlitupa mwongozo wa Mola nyuma ya migongo yenu, basi niache nikaeleze yaliyofichwa.

وَ اِنِّیْ اَخَذْتُ الْعِلْمَ مِنْ مَّنْبَعِ الْهُدٰی          وَ اَجْرٰی عُيُوْنِیْ فَضْلُهُ الْمُتَكَثِّرُ

Nami nimejipatia elimu kutoka kwenye chemchemi ya mwongozo, na fadhili Yake nyingi imetiririsha chemchemi zangu.

وَ اُعْطِيْتُ مِنْ رَّبِّیْ عُلُوْمًا صَحِيْحَةً          وَ اَعْلَمُ مَا لَا تَعْلَمُوْنَ وَ اُعْثَرُ

Na nimejaliwa elimu sahihi kutoka kwa Mola wangu, nami najua msiyoyajua na ninahabarishwa.

وَ كَأْسٍ سَقَانِيْ رُوْحُ رُوْحِيْ كَأَنَّهَا رَحِيْقٌ كَنَجْمٍ نَاصِعِ اللَّوْنِ اَحْمَرُ

Na Mpendwa wangu Ameninywesha vikombe vingi, kana kwamba ni mvinyo nyekundu halisi kama nyota.

فَلَا تُبْشِرُوْا بِالنَّقْلِ يَا مَعْشَرَ الْعِدَا وَ كَمْ مِّنْ نُّقُوْلٍ قَدْ فَرَاهَا مُسَحِّرُ

Kwa hiyo, enyi wapinzani, msifurahie maandiko tu, na kuna maandiko mengi na Hadithi walizobuni laghai.

هَلِ النَّقْلُ شَيْءٌ بَعْدَ اِيْحَاءِ رَبِّنَا فَاَيَّ حَدِيْثٍ بَعْدَهُ نَتَخَيَّرُ

Na ni nini uhakika wa maandiko baada ya wahyi wa Mwenyezi Mungu? Basi, tukubali Hadithi gani baada ya wahyi wa Mwenyezi Mungu.

وَ قَدْ مُزِّقَ الْاَخْبَارُ كُلَّ مُمَزَّقٍ فَكُلٌّ بِمَا هُوَ عِنْدَهُ يَسْتَبْشِرُ

Na Hadithi zenyewe zikawa vipande vipande, na kila kundi linafurahia Hadithi zao.

اَ عِنْدَكَ بُرْهَانٌ قَوِيٌّ مُّنَقَّحٌ عَلٰى فَضْلِ شَيْخٍ عَابَ اَوْ اَنْتَ تَهْذِرُ

Je, unao uthibitisho wowote wa ubora wa Maualwii Muhammad Husain anayekosoa maandishi yangu, au wewe unapayuka tu.

اَ تَحْسَبُ مِنْ حُمْقٍ حُسَيْنًا مُّحَقِّقًا وَ فِيْ كَفِّهٖ حَمْأٌ وَّ مَاءٌ مُّكَدَّرُ

Je kwa ujinga wako unamfikiria Muhammad Husain kuwa mwanachuoni, ilihali mkononi mwake mna matope meusi na maji machafu.

اَ تُخْبِرُنِیْ مِنْ تَّآزِلٍ مَّا رَأَيْتَهُ       وَ تَذْكُرُ اَخْبَارًا دَفَاهَا التَّغَيُّرُ

Je unaniambia habari za anishukiaye usiyemwona na unataja Hadithi ambazo zimeharibiwa kwa kutomwa.

وَ تَعْلَمُ اَنَّ الظَّنَّ لَيْسَ بِقَاطِعٍ       وَ اَنَّ الْيَقِيْنَ الْبَحْتَ يُرْوِیْ وَ يُثْمِرُ

Na unajua kuwa dhana siyo hoja ya mkataa, na kwamba yakini inamwagilia na kuzaa matunda.

وَ لَسْتُ كَمِثْلِكَ فِی الظُّنُوْنِ مُقَيَّدًا       وَ اِنِّیْ اَرَی اللهَ الْقَدِيْرَ وَ اُبْصِرُ

Na sikuzuiliwa na dhana kama wewe; namtazama Mungu wangu Mweza na ninamshuhudia.

اَخَذْنَا مِنَ الْحَيِّ الَّذِیْ لَيْسَ مِثْلُهُ       وَ اَنْتُمْ عَنِ الْمَوْتٰی رَوَيْتُمْ فَفَكِّرُوْا

Tulichukua kutoka Kwake Yeye Aliye Mzima wa Milele na wa pekee; nanyi mnasimulia kutoka kwa wafu.

اُرَبّٰی بِفَضْلِ اللهِ فِیْ حُجْرِ لُطْفِهٖ       وَ فِیْ كُلِّ مَيْدَانٍ اُعَانُ وَ اُنْصَرُ

Nililelewa kwa fadhili ya Mungu mapajani mwa ukarimu Wake, nami naauniwa na kusaidiwa katika kila uwanja.

وَ قَدْ خَصَّنِیْ رَبِّیْ بِفَضْلٍ وَّ رَحْمَةٍ       وَ نَصْرٍ وَّ تَأْيِيْدٍ وَّ وَحْيٍ يُّكَرَّرُ

Na Mola wangu Akanifanya muhtasi kwa fadhili na rehema yake, na kwa nusura na msaada na wahyi ufululizao.

سَقَانِیْ مِنَ الْاَسْرَارِ كَأْسًا رَوِيَّةً       هَدَانِیْ اِلٰی نَهْجٍ بِهِ الْحَقُّ يَبْهَرُ

Akaninywesha kikombe kitoshelezacho na akaniongoza kwenye njia ambayo kwayo haki inang'aa.

فَدَعْ اَيُّهَا الْمُغْوِىْ حُسَيْنًا وَّ ذِكْرَهٗ  اَ تَذْكُرُ لَيْلًا عِنْدَ شَمْسٍ تُنَوِّرُ

Kwa hiyo, Ee mpotoshaji, mwache Muhammad Husain na kumtaja-taja, je utataja usiku dhidi ya jua liangazalo.

وَ نَحْنُ كُمَاةُ اللّٰهِ جِئْنَا بِاَمْرِهٖ  حَلَلْنَا بِلَادَ الشِّرْكِ وَ اللّٰهُ يَخْفُرُ

Sisi tu wapanda farasi wa Mungu, tumekuja kwa amri Yake; mijini mwa shirki tumeingia, na Mungu Anaongoza.

اَقُوْلُ وَ لَا اَخْشٰى فَاِنِّىْ مَسِيْحُهٗ  وَ لَوْ عِنْدَ هٰذَا الْقَوْلِ بِالسَّيْفِ اُنْحَرُ

Nasema pasipo kuogopa kwamba mimi ni Masihi Mau‘udi wa Mungu, hata nikiuawa kwa upanga kwa kauli hii.

وَ قَدْ جَاءَ فِى الْقُرْآنِ ذِكْرُ فَضَائِلِىْ  وَ ذِكْرُ ظُهُوْرِىْ عِنْدَ فِتَنٍ تُثَوَّرُ

Na fadhila zangu zimo ndani ya Kurani na pia habari za kudhihiri kwangu katika zama za msukosuko.

وَ مَا اَنَا اِلَّا مُرْسَلٌ عِنْدَ فِتْنَةٍ  فَرُدَّ قَضَاءَ اللّٰهِ اِنْ كُنْتَ تَقْدِرُ

Nami nimetumwa na Mungu katika zama za msukosuko; badili basi hukumu ya Mungu ikiwa unao uwezo.

تَخَيَّرَنِىْ الرَّحْمَانُ مِنْ بَيْنِ خَلْقِهٖ  لَهُ الْحُكْمُ يَقْضِىْ مَا يَشَاءُ وَ يَاْمُرُ

Mungu Amenichagua mimi miongoni mwa mahuluku wake; hukumu ni yake tu Hufanya Ayatakayo.

وَ وَاللّٰهِ مَا اَفْرِىْ وَ اِنِّىْ لَصَادِقٌ  وَ اِنَّ سَنَا صِدْقِىْ يَلُوْحُ وَ يَبْهَرُ

Na Wallahi, mimi si mzushi; ni mkweli, na nuru ya ukweli wangu inang'aa.

تَرَاءَتْ لَنَا كَالشَّمْسِ صَفْوَةُ اَمْرِنَا     وَ اَرْوَتْ حَدَائِقَنَا عُيُوْنٌ تُنَضِّرُ

Uhalisi wa hali yetu ulidhihirika kama jua, na chemchemi zilimwagilia bustni zetu, zinazong'arisha.

تَكَدَّرَ مَاءُ السَّابِقِيْنَ وَ عَيْنُنَا     اِلٰى اٰخِرِ الْاَيَّامِ لَا تَتَكَدَّرُ

Maji ya wengine waliokuwa miongoni mwa umati yamekauka, lakini chemchemi yetu haitakauka mpaka siku za mwisho.

اِذَا مَا غَضِبْنَا يَغْضَبُ اللّٰهُ صَائِلًا     عَلٰى مُعْتَدٍ يُّؤْذِيْ وَ بِالسُّوْءِ يَجْهَرُ

Tunapokasirika, Mungu Humkasirikia mtu anayevuka mipaka akiudhi na anafanya maovu hadharani.

وَ يَأْتِيْ زَمَانٌ كَاسِرٌ كُلَّ ظَالِمٍ     وَ هَلْ يُهْلَكَنَّ الْيَوْمَ اِلَّا الْمُدَمَّرُ

Na unawadia wakati utakaovunja kila dhalimu; na hakuna atakayeangamia isipokuwa aliyekwisha angamia tayari.

وَ اِنِّيْ لَشَرُّ النَّاسِ اِنْ لَّمْ يَكُنْ لَّهُمْ     جَزَاءَ اِهَانَتِهِمْ صَغَارٌ يُّصَغِّرُ

Nami nitakuwa mbaya zaidi kuliko watu, wasipodhalilika wadhalilishao.

وَ وَاللّٰهِ اِنِّيْ مَا ادَّعَيْتُ تَعَلِّيًا     وَ اَبْغِيْ حَيَاةً مَّا يَلِيْهَا التَّكَبُّرُ

Na Wallahi, sikudai kwa kujigamba; nami nataka maisha yasiyo na kiburi hata chembe.

وَ قَدْ سَرَّنِيْ اَنْ لَّا يُشَارَ بِاِصْبَعٍ     اِلَيَّ وَ اُلْقٰى مِثْلَ عَظْمٍ يُعَفَّرُ

Na ilikuwa furaha yangu kwamba nisijulikane, na nitupwe kama mfupa wenye mavumbi.

فَلَمَّا اَجَزْنَا سَاحَةَ الْكِبْرِ كُلَّهَا     اَتَانِيْ مِنَ الرَّحْمٰنِ وَحْيٌ يُّكَبِّرُ

Basi, tulipotengana kabisa na kiburi, ndipo wahyi wa Rahmani ulinijia ulionitukuza.

اِذَا قِيْلَ اِنَّكَ مُرْسَلٌ خِلْتُ اَنَّنِيْ     دُعِيْتُ اِلٰى اَمْرٍ عَلَى الْخَلْقِ يَعْسُرُ

Nilipoambiwa, umetumwa na Mungu, nikafikiri kwamba nimeitwa kwenye jambo litakalokuwa zito kwa watu.

وَ لَوْ اَنَّ قَوْمِيْ اٰنَسُوْنِيْ كَطَالِبٍ     دَعَوْتُ لِيُعْطَوْا عَيْنَ عَقْلٍ وَ بُصِّرُوْا

Na kama watu wangu wangenijia kama mtafuta haki, ningewaombea wajaliwe ufahamu na busara.

وَ لٰكِنَّهُمْ عَابُوْا وَ اٰذَوْا وَ زَوَّرُوْا     وَ حَثُّوْا عَلَيَّ الْجَاهِلِيْنَ وَ ثَوَّرُوْا

Lakini wakanikosoa na kuniudhi na kusema uongo, na kuwachochea wajinga dhidi yangu.

وَ عَيَّرَنِي الْوَاشُوْنَ مِنْ غَيْرِ خُبْرَةٍ     وَ نَاشُوْا ثِيَابِيْ مِنْ جُنُوْنٍ وَّ اَعْذَرُوْا

Na wapinzani walinikaripia pasipo kujua habari zangu na wakashika nguo zangu kwa umajununi na kuzidi sana.

عَجِبْتُ لَهُمْ فِيْ حَرْبِنَا كَيْفَ خَالَطُوْا     وَ لَمْ يَبْقَ ضِغْنٌ بَيْنَهُمْ وَ تَنَمُّرُ

Nilishangaa kwamba hao walichangamanaje katika mapambano yetu, na haikubaki baina yao chuki yoyote wala kijicho.

وَ قَضَّوْا مَطَاعِنَ بَيْنَهُمْ ثُمَّ اَصْدَرُوْا     اِلَيْنَا الْاَسِنَّةَ وَ الْخَنَاجِرَ شَهَّرُوْا

Hao waliendelea kutukana kwa muda, kisha wakaelekeza mikuki yao upande wetu na kuchomoa panga zao.

فَقُلْتُ لَهُمْ يَا اَيُّهَا النَّاسُ مَا لَكُمْ    اَثَرْتُمْ غُبَارًا مِّنْ كَلَامٍ يُّزَوَّرُ

Basi nikawaambia: Enyi watu, mmekuwaje, mlifanya fujo hivyo kwa kusema uwongo.

عَلَى الْحُمْقِ جَيَّاشُوْنَ مِنْ غَيْرِ فِطْنَةٍ    كَمَا زَلَّتِ الصَّفْوَاءُ حِيْنَ تُكَوَّرُ

M wenye kuhamaki kwa ujinga wenu pasipo kutumia busara, kama vile jiwe safi huteleza chini haraka sana linapotupwa chini.

فَمَا بَرِحَتْ اَقْدَامُنَا مَوْطِنَ الْوَغٰى    وَ مَا ضَعُفَتْ حَتّٰى اَعَانَ الْمُظَفِّرُ

Basi, miguu yetu haikuondoka medani ya vita wala haikuchoka hadi Mungu Alitupatia ushindi.

وَ كُنْتُ اَرَى الْاِسْلَامَ مِثْلَ حَدِيْقَةٍ    مُبَعَّدَةٍ مِّنْ عَيْنِ مَاءٍ يُّنَضِّرُ

Na nilikuwa nikiiona Islam kama bustani iliyo mbali na chemchemi inayong'arisha.

فَمَازِلْتُ اَسْقِيْهَا وَ اَسْقِيْ بِلَادَهَا    مِنَ الْمُزْنِ حَتّٰى عَادَ حِبْرٌ مُّدَعْثَرُ

Basi, nikaimwagilia bustani hii na ardhi yake kwa maji ya mvua ya mbinguni mpaka uzuri wake uliopotea ukarudi.

وَ جَاشَتْ اِلَيَّ النَّفْسُ مِنْ فِتْنَةِ الْعِدَا    فَاَنْزَلَ رَبِّيْ حَرْبَةً لَّا تُكَسَّرُ

Na nikafadhaika kwa sababu ya fitina ya maadui, basi Mola wangu Akateremsha mkuki usiovunjika.

فَاَصْبَحْتُ اَسْتَقْرِى الرِّجَالَ رِجَالَهُمْ    لِاُفْحِمَ قَوْمًا جَابِرِيْنَ وَ اُنْذِرُ

Basi, asubuhi nikaanza kuwasaka hao watu, ili niwatimizie hoja wadhalimu.

وَ قَدْ كَانَ بَابُ اللُّدِّ مَرْكَزَ حَرْبِهِمْ     كَلَامٌ مُّضِلٌّ لَّا حُسَامٌ مُشَهَّرُ

Na njia yao ya mapigano ilikuwa ni kubishana tu, yaani kusema maneno ya kuwapoteza watu, si kutumia upanga uliochomolewa kwa ajili ya dini.

فَوَافَيْتُ مَجْمَعَ لُدِّهِم وَ قَتَلْتُهُمْ     بِضَرْبٍ وَّ لَمْ اَكْسَلْ وَ لَمْ اَتَحَسَّرُ

Basi, nikaja kwenye mkusanyiko wa wapiganaji na kuwaulia mbali kwa pigo moja, sikulegea wala sikuchoka.

وَ اِنِّيْ اَنَا الْمَوْعُوْدُ وَ الْقَائِمُ الَّذِىْ     بِهٖ تُمْلَأَنَّ الْاَرْضُ عَدْلًا وَّ تُثْمِرُ

Nami ndimi Masihi Mau'udi na Imamu Kaim [Mahdi] ambaye kwa njia yake ardhi itajaa adili na kuzaa matunda.

بِنَفْسِىْ تَجَلَّتْ طَلْعَةُ اللهِ لِلْوَرٰى     فَيَاطَالِبِىْ رُشْدٍ عَلٰى بَابِىَ احْضُرُوْا

Kwa njia yangu utawadhihirikia mahuluku Uso wa Mungu, basi enyi watafutao mwongozo hudhuruni mlangoni pangu.

خُذُوْا حَظَّكُمْ مِّنِّىْ فَاِنِّىْ اِمَامُكُمْ     اُذَكِّرُكُمْ اَيَّامَكُمْ وَ اُبَشِّرُ

Chukueni hadhi yenu kwangu, kwani mimi ni imamu wenu, nawakumbushieni siku zenu na kuwapeni habari njema.

وَ قَدْ جِئْتُكُمْ يَا قَوْمِ عِنْدَ ضَرُوْرَةٍ     فَهَلْ مِنْ رَشِيْدٍ عَاقِلٍ يَّتَدَبَّرُ

Na enyi watu wangu, nimekujieni wakati wa haja; basi, je yupo miongoni mwenu mwongofu na mwenye busara azingatiaye jambo hili?

وَ مَا الْبِرُّ اِلَّا تَرْكُ بُخْلٍ مِّنَ التُّقٰى          وَ مَا الْبُخْلُ اِلَّا رَدُّ مَنْ يَّتَبَقَّرُ

Na wema ndio kuachana na ubahili kwa sababu ya takwa. Na ubahili ndio tu kumkatalia mbali mtu bora mwenye elimu pana na kamilifu.

وَ قَالُوْا اِلَى الْمَوْعُوْدِ لَيْسَ بِحَاجَةٍ          فَاِنَّ كِتَابَ اللهِ يَهْدِىْ وَ يُخْبِرُ

Na wakasema, hatuna haja ya Masihi Mau‘udi, kwani Kitabu cha Mwenyezi Mungu kinaongoza na kujulisha.

وَ مَا هِىَ اِلَّا بِالْغَيُوْرِ دُعَابَةٌ          فَيَا عَجَبًا مِّنْ فِطْرَةٍ تَتَهَوَّرُ

Na huku ndiko kumfanyia Mungu Mwenye ghera masihara; ajabu ilioje juu ya tabia ya ujasiri kama hii!

وَ قَدْ جَاءَ قَوْلُ اللهِ بِالرُّسْلِ تَوْأَمًا          وَ مِنْ دُوْنِهِمْ فَهْمُ الْهُدٰى مُتَعَسِّرُ

Na ukweli halisi ni huu kwamba Neno la Mungu na Mitume ni ‘mapacha’. Pasipo hayo ni vigumu kuelewa Neno la Mungu.

فَاِنَّ ظُبَى الْاَسْيَافِ تَحْتَاجُ دَائِمًا          اِلٰى سَاعِدٍ يُّجْرِى الدِّمَاءَ وَ يُنْدِرُ

Kwani, makali ya panga huwa yanahitaji mkono unaotiririsha damu na kutenganisha kichwa na mwili.

بِعَضْبٍ رَّقِيْقِ الشَّفْرَتَيْنِ هَزِيْمَةٌ          اِذَا نَاشَهُ طِفْلٌ ضَعِيْفٌ مُّحَقَّرُ

Hata kama makali ya upanga yamenolewa namna gani, ushinde tu utatokea kama ataushika mtoto dhaifu, mnyonge.

وَ اَمَّا اِذَا اَخَذَ الْكَمِيُّ مُفَقِّرًا     كَفَى الْعَوْدَ مِنْهُ الْبَدْءُ ضَرْبًا وَّ يَنْحَرُ

Lakini, mtu shujaa anapoushika upanga mkali, pigo lake la kwanza halitahitaji pigo la pili na litamchinja tu.

اِذَا قَلَّ تَقْوَى الْمَرْءِ قَلَّ اقْتِبَاسُهُ     مِنَ الْوَحْيِ كَالسَّلْخِ الَّذِىْ لَا يُنَوِّرُ

Takwa ya mtu inapopungua, uwezo wake wa kupata maarifa ya wahyi pia hupungua, kama vile mwanga usivyobaki usiku wa mwisho wa mwezi.

فَيَا اَسَفًا اَيْنَ التُّقَاةُ وَ اَرْضُهَا     وَ اِنِّىْ اَرٰى فِسْقًا عَلَى الْفِسْقِ يَظْهَرُ

Ni masikitiko, ipo wapi takwa na ardhi yake; nami naona unadhihiri uasi juu ya uasi.

أَرَى ظُلُمَاتٍ لَّيْتَنِىْ مِتُّ قَبْلَهَا     وَ ذُقْتُ كُئُوْسَ الْمَوْتِ اَوْ كُنْتُ اُنْصَرُ

Nami naona giza totoro ambalo laiti ningekufa kabla yake, na ningeonja vikombe vya mauti au ningesaidiwa.

أَرَى كُلَّ مَحْجُوْبٍ لِدُنْيَاهُ بَاكِيًا     فَمَنْ ذَا الَّذِىْ يَبْكِىْ لِدِيْنٍ يُحَقَّرُ

Namwona kila aliyekingiwa pazia kwa Mungu akililia dunia yake; yu nani, basi, anayeililia dini hii inayodharauliwa.

وَ لِلدِّيْنِ اَطْلَالٌ اَرَاهَا كَلَاهِفٍ     وَ دَمْعِىْ بِذِكْرِ قُصُوْرِهٖ يَتَحَدَّرُ

Na zipo alama za magofu ya dini, ninazotazama kwa huzuni, na machozi yangu yatiririka kwa kukumbuka majumba yake.

تَرَاءَتْ غَوَايَاتٌ كَرِيْحٍ مُّجِيْحَةٍ وَ اَرْخٰى سَدِيْلَ الْغَيِّ لَيْلٌ مُّكَدَّرُ

Upotevu ukadhihiri kama kimbunga kinachong'olea mbali miti, na usiku wa giza ukatandaza upotevu.

تَهُبُّ رِيَاحٌ عَاصِفَاتٌ كَأَنَّهَا سِبَاعٌ بِاَرْضِ الْهِنْدِ تَعْوِىْ وَ تَزْءَرُ

Vimbunga vinavuma vikali, kana kwamba vi wanyama mbuai nchini India wanaolia kama mbwamwitu na wananguruma kama simba.

اَرَى الْفَاسِقِيْنَ الْمُفْسِدِيْنَ وَ زُمْرَهُمْ وَ قَلَّ صَلَاحُ النَّاسِ وَ الْغَيُّ يَكْثُرُ

Ninaona mafasiki na wafisadi makundi kwa makundi, na wema umepungua na upotovu umekithiri.

أَرَى عَيْنَ دِيْنِ اللهِ مِنْهُمْ تَكَدَّرَتْ بِهَا الْعِيْنُ وَ الْآرَامُ تَمْشِىْ وَ تَعْبُرُ

Naona chemchemi ya dini ya Mwenyezi Mungu imechafuka, na ndani yake wanyama wa pori wanapita na kuvuka.

اَرَى الدِّيْنَ كَالْمَرْضٰى عَلَى الْاَرْضِ رَاغِمًا وَ كُلُّ جَهُوْلٍ فِي الْهَوٰى يَتَبَخْتَرُ

Naona dini imelazika chini kama wagonjwa, na kila jahili anatembea kwa maringo katika matamanio yake.

وَ مَا هَمُّهُمْ اِلَّا لِحَظِّ نُفُوْسِهِمْ وَ مَا جُهْدُهُمْ اِلَّا لِحَظٍّ يُّوَفَّرُ

Na hamu yao siyo zaidi ya kujipatia ladha ya nafsi, na juhudi zao si zaidi ya kutaka ladha ya nafsi kwa wingi.

نَسُوْا نَهْجَ دِيْنِ اللهِ خُبْثًا وَّ غَفْلَةً وَ قَدْ سَرَّهُمْ سُكْرٌ وَّ فِسْقٌ وَّ مَيْسِرُ

Wakasahau njia ya dini kwa sababu ya uovu na uzembe; na ulevi ufuska na kamari vikawapendeza.

أَرَى فِسْقَهُمْ قَدْ صَارَ مِثْلَ طَبِيْعَةٍ          وَ مَا اِنْ أَرَى عَنْهُمْ شَقَاهُمْ يُقَشَّرُ

Naona ufasiki wao umekuwa ni tabia yao; nionavyo, haiwezekani kutenganisha nao bahati yao mbaya.

فَلَمَّا طَغَى الْفِسْقُ الْمُبِيْدُ بِسَيْلِهِ          تَمَنَّيْتُ لَوْ كَانَ الْوَبَاءُ الْمُتَبِّرُ

Basi, ufasiki uangamizao ulipofurika kupita kiasi, nikatamani tauni iangamizayo iambukizike.

فَإِنَّ هَلَاكَ النَّاسِ عِنْدَ أُولِى النُّهٰى          اَحَبُّ وَ اَوْلٰى مِنْ ضَلَالٍ يُّدَمِّرُ

Kwani sawa na rai ya wenye akili kufa kwa watu ni afadhali kuliko upotevu uangamizao.

وَ مَنْ ذَا الَّذِىْ مِنْهُمْ يَخَافُ حَسِيْبَهُ          وَ مَنْ ذَا الَّذِىْ يَبْغِى السَّدَادَ وَ يُؤْثِرُ

Na ni nani kati yao anayemcha Mungu wake? Na yu nani miongoni mwao anayeshika njia iliyo sawa?

وَ مَنْ ذَا الَّذِىْ لَا يَفْجُرُ اللّٰهَ عَامِدًا          وَ مَنْ ذَا الَّذِىْ بَرٌّ عَفِيْفٌ مُّطَهَّرُ

Na ni nani miongoni mwao asiyemwasi Mungu makusudi; na ni nani miongoni mwao aliye mwema, mnyofu na mwenye moyo safi?

وَ مَنْ ذَا الَّذِىْ مَا سَبَّنِىْ لِتُقَاتِهِ          وَ قَالَ ذَرُوْنِىْ كَيْفَ أُوْذِىْ وَ أُكْفِرُ

Na ni nani kati yao asiyenitusi kwa sababu ya takwa yake, na akasema niacheni, kivipi nimtese na kumkufurisha?

وَ كَيْفَ وَ اِنَّ اَكابر الْقَوْمِ كُلَّهُمْ          عَلَىَّ حِرَاصٌ وَّ الْحُسَامُ مُشَهَّرُ

Na yawezekanaje kuepuka na kutukanwa, kwani wakuu wote wa kaumu wana hamu ya kuniua na upanga umeshachomolewa.

وَ لٰكِنْ عَلَيْهِمْ رُعْبُ صِدْقِيْ مُعَظَّمٌ فَكَيْفَ يُبَارِى اللَّيْثَ مَنْ هُوَ جَوْذَرُ

Lakini wanayo hofu kubwa ya ukweli wangu; basi ndama anawezaje kushindana na simba!

فَلَيْسَ بِاَيْدِى الْقَوْمِ اِلَّا لِسَانُهُمْ مُنَجَّسَةً بِالسَّبِّ وَ اللّٰهُ يَنْظُرُ

Basi, watu hao hawana kitu isipokuwa ulimi tu wao ulionajisika na uchafu wa matusi, ilhali Mungu Huona.

قَضَى اللّٰهُ اَنَّ الطَّعْنَ بِالطَّعْنِ بَيْنَنَا فَذَالِكَ طَاعُوْنٌ اَتَاهُمْ لِيُبْصِرُوْا

Mungu Ameamua kuwa malipo ya mchomo ni mchomo, kwa hiyo tauni hii ndiyo imewajia ili wafumbuliwe macho.

وَ لَيْسَ عِلَاجُ الْوَقْتِ اِلَّا اِطَاعَتِيْ اَطِيْعُوْنِ فَالطَّاعُوْنُ يُفْنٰى وَ يُدْحَرُ

Tiba kwa wakati huu ni kunitii; basi nitiini mimi na tauni itaondoka na kupotea.

وَ قَدْ ذَابَ قَلْبِيْ مِنْ مَّصَائِبِ دِيْنِنَا وَ اَعْلَمُ مَا لَا يَعْلَمُوْنَ وَ اُبْصِرُ

Na moyo wangu umeyeyuka kwa misiba ya dini, nami najua mambo wasiyoyajua.

وَ بَثِّيْ وَ حُزْنِيْ قَدْ تَجَاوَزَ حَدَّهُ وَ لَوْ لَا مِنَ الرَّحْمٰنِ فَضْلٌ اُتَبَّرُ

Na ghamu yangu na huzuni yangu imevuka mipaka, kama si fadhili ya Mungu ningehilikika.

وَ عِنْدِىْ دُمُوْعٌ قَدْ طَلَعْنَ الْمَآقِيَا وَ عِنْدِىْ صُرَاخٌ لَّا يَرَاهُ الْمُكَفِّرُ

Na ninayo machozi yanayoipanda kona ya jicho, na ninayo siahi asiyoona anikufurishaye.

وَ لِیْ دَعَوَاتٌ صَاعِدَاتٌ اِلَی السَّمَا    وَ لِیْ کَلِمَاتٌ فِیْ الصَّلَایَۃِ تَقْعَرُ

Dua zangu zinaendelea kupanda mbinguni; na maneno yangu yanapenya ndani ya mawe.

وَ اُعْطِیْتُ تَأْثِیْرًا مِّنَ اللّٰہِ خَالِقِیْ    وَ تَأْوِیْ اِلٰی قَوْلِیْ قُلُوْبٌ تُطَھَّرُ

Nami nimejaliwa athari kutoka kwa Mungu aliye Mwumba wangu, na mioyo iliyotakasika inanielekea.

وَ اِنَّ جَنَانِیْ جَاذِبٌ بِصِفَاتِہٖ    وَ اِنَّ بَیَانِیْ فِی الصُّخُوْرِ یُؤَثِّرُ

Na moyo wangu unavutia kwa sifa zake, na kauli yangu inayaathiri mawe.

حَفَرْتُ جِبَالَ النَّفْسِ مِنْ قُوَّۃِ الْعُلٰی    فَصَارَ فُؤَادِیْ مِثْلَ نَھْرٍ تُفَجَّرُ

Nilichimba milima ya nafsi kwa uwezo wa kimbingu, basi moyo wangu ukawa kama mfereji unaotiririshwa.

وَ اُعْطِیْتُ مِنْ خَلْقٍ جَدِیْدٍ مِّنَ الْھُدٰی    فَکُلَّ بَیَانٍ فِی الْقُلُوْبِ اُصَوِّرُ

Na nimejaliwa umbo jipya, basi naimarisha nyoyoni kila niyasemayo.

فَرِیْقٌ مِّنَ الْاَحْرَارِ لَا یُنْکِرُوْنَنِیْ    وَ حِزْبٌ مِّنَ الْاَشْرَارِ آذَوْا وَ اَنْکَرُوْا

Kundi moja la watu wema halinikatai; na kundi la washari wananiudhi na kukanusha.

وَ قَدْ زَاحَمُوْا فِیْ کُلِّ اَمْرٍ اَرَدْتُّہٗ    فَاَیَّدَنِیْ رَبِّیْ فَفَرُّوْا وَ اَدْبَرُوْا

Na kila jambo nililokusudia wakalipinga; basi Mola wangu Akanisaida, ndipo wakakimbia na kugeuka.

وَ كَيْفَ عَصَوْا وَ اللّٰهِ لَمْ يُدْرَ سِرُّهَا　　　وَ كَانَ سَنَا بَرْقِيْ مِنَ الشَّمْسِ اَظْهَرُ

Na kwa nini waliasi? Wallahi, haikujulikana siri yake, ilhali mwanga wa umeme wangu ulikuwa dhahiri zaidi hata kuliko jua.

لَزِمْتُ اصْطِبَارًا عِنْدَ جَوْرِ لِئَامِهِمْ　　　وَ كَانَ الْاَقَارِبُ كَالْعَقَارِبِ تَأْبُرُ

Nikavumilia dhuluma yao na nikasubiri, na jamaa zangu walikuwa wakaniuma kama nge.

وَ يَعْلَمُ رَبِّيْ سِرَّ قَلْبِيْ وَ سِرَّهُمْ　　　وَ كُلُّ خَفِيٍّ عِنْدَهُ مُتَحَضِّرُ

Na Mola wagu Anazijua siri zangu na siri zao, na kila kilichofichika kipo mbele yake.

وَ لَيْسَ لِعَضْبِ الْحَقِّ فِي الدَّهْرِ كَاسِرًا　　　وَ مَنْ قَامَ لِلتَّكْسِيْرِ بَغْيًا فَيُكْسَرُ

Na hakuna avunjaye upanga wa Mungu, na atakaye kuuvunja atavunjika mwenyewe.

وَ مَنْ ذَا يُعَادِيْنِيْ وَ اِنِّيْ حَبِيْبُهُ　　　وَ مَنْ ذَا يُرَادِيْنِيْ اِذِ اللّٰهُ يَنْصُرُ

Na ni nani anayeweza kuwa adui yangu ilhali Mungu ni rafiki yangu, na ni nani awezaye kupigana nami kwa kunirushia mawe ilihali Mwenyezi Mungu Yu msaidizi wangu.

وَ لَوْ كُنْتُ كَذَّابًا كَمَا هُوَ زَعْمُهُمْ　　　لَقَدْ كُنْتُ مِنْ دَهْرٍ اَمُوْتُ وَ اُقْبَرُ

Na kama ningekuwa kadhabu kama wadhaniavyo, basi ningekuwa nimekufa kitambo na kutiwa kaburini.

يَظُنُّوْنَ اَنِّیْ قَدْ تَقَوَّلْتُ عَامِدًا    بِمَكْرٍ وَّ بَعْضُ الظَّنِّ اِثْمٌ وَّ مُنْكَرُ

Hao wanadhani nimezua uongo makusudi kwa hila, na baadhi ya dhana ni dhambi ambazo Sheria na akili vinakataa kuzikubali.

وَ كَيْفَ وَ اِنَّ اللّٰهَ اَبْدٰى بَرَاءَتِیْ    وَ جَآءَ بِآيَاتٍ تَلُوْحُ وَ تَبْهَرُ

Na lawezekanaje hili ilhali Mwenyezi Mungu Ameishadhihirisha umaasumu wangu na Akaonyehsa ishara bayana zing'aazo.

وَ يَأْتِيْكَ وَعْدُ اللّٰهِ مِنْ حَيْثُ لَا تَرٰى    فَتَعْرِفُهٗ عَيْنٌ تُحَدُّ وَ تُبْصِرُ

Na ahadi ya Mwenyezi Mungu itakufikia namna usiyojua; basi litaitambua siku ile jicho litakalokuwa kali na lenye kuona.

اَ مُكْفِرِ مَهْلًا بَعْضَ هٰذَا التَّهَكُّمِ    وَ خَفْ قَهْرَ رَبٍّ قَالَ لَا تَقْفُ، فَاحْذَرُ

Ee mkufurishaji wangu, punguza hasira hii na iogope ghadhabu ya Mungu Aliyesema usiyafuate usiyoyajua.

وَ اِذْ قُلْتُ اِنِّیْ مُسْلِمٌ قُلْتَ كَافِرٌ    فَاَيْنَ التُّقٰى يَا اَيُّهَا الْمُتَهَوِّرُ

Na niliposema, mimi ni Mwislamu, ukasema u kafiri. Basi iko wapi takwa yako, ewe ujasiriye.

وَ اِنْ كُنْتَ لَا تَخْشٰى فَقُلْ لَّسْتَ مُؤْمِنًا    وَّ يَأْتِیْ زَمَانٌ تُسْئَلَنَّ وَ تُخْبَرُ

Na kama huogopi, basi sema tu kuwa wewe si muumini; zawadia zama utakapoulizwa na kujulishwa.

وَ اِنِّیْ تَرَکْتُ النَّفْسَ وَ الْخَلْقَ وَ الْھَوٰی   فَلَا السَّبُّ یُؤْذِیْنِیْ وَ لَا الْمَدْحُ یُبْطِرُ

Nami nimeachana na nafsi, mahuluku na tamaa, basi matusi hayaniumizi sasa wala maneno ya sifa hayanifurahishi.

وَ کَمْ مِّنْ عَدُوٍّ کَانَ مِنْ اَکْبَرِ الْعِدَا   فَلَمَّا اَتَانِیْ صَاغِرًا صِرْتُ اَصْغَرُ

Na kuna wengi walikuwa maadui zangu wakali, lakini aliponijia adui wa aina hii akijinyenyekeza, nikajinyenyekeza zaidi kuliko yeye.

وَ لَسْتُ بِذِیْ کُھُرُوْرَةٍ غَیْرَ اَنَّنِیْ   اِذَا زَادَ فُحْشًا ذُوْ عِنَادٍ اُصَعِّرُ

Mimi si mwenye chuki. Naam, mwenye inadi anaporuka mipaka katika kutukana, nageuza uso wangu.

وَ لَا غِلَّ فِیْ قَلْبِیْ وَ لَا مِنْ جَبَانَةٍ   وَ اُلْقِیْ حُسَامِیْ مُغْضِیًا وَّ اُشَھِّرُ

Na sina mfundo moyoni, mwangu wala mimi si mwoga. Nami nikisamehe natupilia mbali upanga wangu, lakini mapiganoni ninauchomoa pia.

فَاِنْ تَبْغِنِیْ فِیْ حَلْقَةِ السِّلْمِ تُلْفِنِیْ   وَ اِنْ تَطْلُبَنِّیْ فِی الْمَیَادِیْنِ اَحْضُرُ

Basi, ukinitaka kufika kwenye kikao cha amani utanikuta huko; na ukinitafuta katika medani za vita, nitakuwa humo.

وَ اَرْسَلَنِیْ رَبِّیْ لِاِصْلَاحِ خَلْقِهٖ   فَیَاصَاحِ لَا تَنْطِقْ ھَوًی وَّ تَصَبَّرُ

Na Mola wangu Amenituma kusuluhisha mahuluku; basi ee mwenzangu, usiseme kwa matamanio ya nafsi na ushike subira.

وَ اِنْ اَكُ كَذَّابًا فَكِذْبِيْ يُبِيْدُنِيْ وَ اِنْ اَكُ مِنْ رَّبِّيْ فَمَالَكَ تَهْجُرُ

Na ikiwa mimi ni mwongo, basi uongo wangu utaniangamiza; na kama nimetoka kwa Mungu, basi kwa nini unapayuka?

فَذَرْنِيْ وَ رَبِّيْ وَ انْتَظِرْ سَيْفَ حُكْمِهِ لِيَقْطَعَ رَأْسِيْ اَوْ قَفَا مَنْ يُّكَفِّرُ

Basi niache na Mola wangu na ungoje upanga wa hukumu yake ili ukate kichwa changu au cha Yule anikufurishaye.

تَحَامَ قِتَالِيْ وَ اجْتَنِبْ مَاصَنَعْتَهُ وَ اِنَّا اِذَا جُلْنَا فَاِنَّكَ مُدْبِرُ

Jiepushe na kupigana nami, na ujitenge na matendo yako maovu; nasi tukija katika medani, utakimbia.

اَرَى الصَّالِحِيْنَ يُوَفَّقُوْنَ لِطَاعَتِيْ وَ اَمَّا الْغَوِيُّ فَفِي الضَّلَالَةِ يُقْبَرُ

Nawaona watu wema kwamba wanajaliwa kunitii, lakini mpotevu wa tangu azali ataingia kaburini akiwa mpotevu.

وَ ذَالِكَ خَتْمُ اللهِ مِنْ بَدْوِ فِطْرَةٍ وَ اِنَّ نُقُوْشَ اللهِ لَا تَتَغَيَّرُ

Na huu ndio muhuri wa Mungu tangu mwanzo, na maandiko ya Mungu hayawezi kubadilika.

كَذَالِكَ نُوْرُ الرُّشْدِ مَايُخْطِئُ الْفَتٰى وَ كُلُّ نَخِيْلٍ لَّا مَحَالَةَ تُثْمِرُ

Kadhalika nuru ya mwongozo haitengani na mtu huyu, na hatimaye kila mtende huzaa matunda.

وَ مَنْ يَّكُ ذَا فَضْلٍ فَيُدْرِكُ مَقَامَهُ وَ لَوْ فِيْ شَبَابٍ اَوْ بِوَقْتٍ يُّعَمَّرُ

Na aliyejaliwa fadhili ya Mungu, atapata daraja yake, walau katika ujana au atakapozeeka.

وَ لَا يَهْلِكُ الْعَبْدُ السَّعِيْدُ جِبِلَّةً إِذَا مَاعَمِيَ يَوْمًا بِآخَرَ يَنْظُرُ

Na mwenye bahati njema kitabia hataangamia; kama yu kipofu leo, ataona kesho.

وَ لِلْغَيِّ آثَارٌ وَّ لِلرُّشْدِ مِثْلُهَا فَقُوْمُوْا لِتَفْتِيْشِ الْعَلَامَاتِ وَانْظُرُوْا

Na zipo alama za upotofu na kadhalika za uongofu pia; basi zichunguzeni alama na mwangalie kwa uangalifu.

اَرَى الظُّلْمَ يَبْقَى فِي الْخَرَاطِيْمِ وَسْمُهُ وَ يُنْصَرُ مَظْلُوْمٌ ضَعِيْفٌ مُّخَسَّرُ

Naona alama za dhuluma zinabaki puani mwa mtu; na mdhulumiwa dhaifu, mwenye hasara hatimaye anasaidiwa.

وَ قَدْ اَعْرَضُوْا عَنْ كُلِّ خَيْرٍ بِغَيْظِهِمْ كَاَنِّيْ اَرَاهُمْ مِّثْلَ نَارٍ تُسَعَّرُ

Nao wakaukengeuka, kwa kughadhibika kila wema niliowatolea, kana kwamba ninawaona kama moto uwakao.

وَ يُنْصَرُ مَظْلُوْمٌ بِآخِرِ اَمْرِهِ وَ لَا سِيَّمَا عَبْدٌ مِّنَ اللهِ مُنْذِرُ

Na mdhulumiwa hatimaye husaidiwa, hususani mja mwonyaji atokaye kwa Mungu.

إِذَا مَا بَكَى الْمَعْصُوْمُ تَبْكِي الْمَلَائِكُ فَكَمْ مِّنْ بِلَادٍ تُهْلَكَنَّ وَ تُجْذَرُ

Maasumu huyo anapolia, malaika hulia pamoja naye, basi miji mingi yaangamizwa na kung'olewa mbali.

إِذَا ذَرَفَتْ عَيْنَا تَقِيٍّ بِغُمَّةٍ    يُفَرَّجُ كَرْبٌ مَّسَّهُ اَوْ يُبَشَّرُ

Macho ya mcha Mungu yanapotiririsha machozi kwa huzuni, basi huondolewa uchungu ule au hupewa habari njema.

عَلَى الاَرْضِ قَوْمٌ كَالسُّيُوْفِ دُعَاءُهُمْ    فَمَنْ مَّسَّ هٰذَا السَّيْفَ بِالشَّرِّ يُبْتَرُ

Wapo watu duniani ambao dua zao ni kama panga; basi anayepata kuugusa upanga huo, hukatwa.

تَرَى كَيْفَ نَرْقَى وَ الْحَوَادِثُ جُمَّةٌ    وَ يُهْلَكُ مَنْ يَّبْغِي هَلَاكِيْ وَ يَمْكُرُ

Unaona jinsi tunavyoendelea mbele japo matatizo yamekusanyika kutoka pande zote; na anayetaka hilaki yangu na kufanya hila huhilikishwa.

لَنَا كُلَّ آنٍ مِّنْ مُّعِيْنٍ حِمَايَةٌ    نُغَادِرُ صَرْعٰى مَاكِرِيْنَ وَ نَظْفَرُ

Saa zote twasaidiwa na Msaidizi. Tunawaangusha chini wanaofanya hila na tunashinda.

اَ يَا شَاتِمًا لَّا شَاتِمَ الْيَوْمَ مِثْلَكُمْ    وَ مَا اِنْ اَرَى فِيْ كَفِّكُمْ مَا يُبْطِرُ

Ewe unayetukana, hakuna leo mwenye mdomo mchafu kama wewe; nami sioni mkononi mwako kinachokuhimiza kuringa.[36]

[36] Hii ndiyo kujibu mashambulizi ya Mshia Ali Ha'irii.

تَسُبُّ وَ مَا اَدۡرِیۡ عَلٰی مَا تَسُبُّنِیۡ        اَ آذَاكَ قَوۡلِیۡ فِیۡ حُسَیۡنٍ فَتُوۡغَرُ

Unanitukana, na sijui kwa nini unanitukana. Je kauli yangu kumhusu Imam Husain[ra] ilikuudhi kwa hiyo umekasirika?

اَ تَحۡسَبُہٗ اَتۡقَی الرِّجَالِ وَ خَیۡرَھُمۡ        فَمَا نَالَکُمۡ مِّنۡ خَیۡرِہٖ یَا مُعۡذِرُ

Je, unamwona kuwa mcha Mungu zaidi kuliko watu wote? Niambie amekufaa nini kidini, ee mpiga chuku?

اَرَاكُمۡ کَذَاتِ الۡحَیۡضِ لَا مِثۡلَ طَاھِرٍ        تَطِیۡبُ وَ مِنۡ مَّاءِ الۡعَذَابَةِ تَطۡھَرُ

Nakuona u kama mwanamke mwenye hedhi, *si kama mwanamke asiye na hedhi*.[37]

حَسِبۡتُمۡ حُسَیۡنًا اَکۡرَمَ النَّاسِ فِی الۡوَرٰی        وَ اَفۡضَلَ مَا فَطَرَ الۡقَدِیۡرُ وَ یَفۡطُرُ

Mmemfahamu Husain mhashamu kuliko mahuluku wote, na kumchukulia kuwa bora kuliko wanadamu wote Aliowaumba Mungu;

کَاَنَّ امۡرَءًا فِی النَّاسِ مَا کَانَ غَیۡرُہٗ        وَ طَھَّرَہُ الرَّحۡمَانُ وَ الۡغَیۡرُ یَفۡجُرُ

Kana kwamba yeye tu ndiye alikuwa mtu pekee miongoni mwa watu, na akatakaswa na Mungu, na minghairi yake wengine ni wachafu.

---

[37] Ibara ya mshororo wa pili, iliyoandikwa kwa herufi mlazo, ni tafsiri ya mshororo wa kwanza tu. Ikasahaulika kutiwa tafsiri ya mshororo wa pili, ambayo ni hii: "Amejipaka manukato, na majimaji ya kutoka uterasi pia yamekatika baada ya hedhi na ametakasika." Mwenezi.

وَ هٰذَا هُوَ الْقَوْلُ الَّذِیْ فِی ابْنِ مَرْیَمٍ    یَقُوْلُ النَّصَارٰی اَیُّهَا الْمُتَنَصِّرُ

Na hii hii ndiyo kauli wanayosema Wakristo kumhusu Yesu, Ewe unayeshabihiana na Manasara.

فَیَا عَجَبًا کَیْفَ الْقُلُوْبُ تَشَابَهَتْ    فَکَادَ السَّمَا مِنْ قَوْلِکُمْ تَتَفَطَّرُ

Basi, ni ajabu, nyoyo zimeshabihianaje! Basi, karibu mbingu zipasuke kwa kauli zenu hizi.

اَ تُطْرِءُ عَبْدًا مِّثْلَ عِیْسٰی وَ تَنْحِتُ    لَهٗ رُتْبَةً کَالْاَنْبِیَاءِ وَ تَهْذُرُ

Je unamsifu mtu mmoja kupita kiasi kama Isa[as] na unampatia daraja ya manabii.

اَ لَا لَیْتَ شِعْرِیْ هَلْ رَأَیْتَ مَقَامَهٗ    کَمِثْلِ بَصِیْرٍ اَوْ عَلَی الظَّنِّ تَعْمُرُ

Laiti ungefahamu. Je umeishaona cheo chake, au unajenga fikara zako juu ya dhana tu.

اَ تُعْلِیْهِ اِطْرَاءً وَّ کِذْبًا وَّ فِرْیَةً    اَتَسْقِیْهِ کَأْسًا مَا سَقَاهُ الْمُقَدِّرُ

Je, unataka kumwinua kwa kumsifu kupita kiasi na kwa njia ya uongo na uzushi? Je, unamnywesha kikombe ambacho Mungu hakumnywesha?

تَکَادُ السَّمٰوَاتُ الْعُلٰی مِنْ کَلَامِکُمْ    تَفَطَّرْنَ لَوْ لَا وَقْتُهَا مُتَقَرِّرُ

Karibu mbingu zilizo juu zipasuke kwa kauli yenu, kama wakati wake wa kupasuka usingekuwa umewekwa.

اَ کَانَ حُسَیْنٌ اَفْضَلَ الرُّسْلِ کُلِّهِمْ    اَ کَانَ شَفِیْعَ الْاَنْبِیَاءِ وَ مُؤْثَرُ

Je Husain[ra] alikwua mbora kuliko manabii wote? Je alikuwa mwombezi wa Manabii na mbora kupita wote?

اَلَا لَعْنَةُ اللّٰهِ الْغَيُوْرِ عَلَى الَّذِيْ     يَمِيْنُ بِاِطْرَاءٍ وَّ لَا يَتَبَصَّرُ

Habedari! Laani ya Mungu Mwenye ghera iko juu ya mtu anayesema uongo kwa kupiga chuku na haoni.

وَ اَمَّا مَقَامِيْ فَاعْلَمُوْا اَنَّ خَالِقِيْ     يُحَمِّدُنِيْ مِنْ عَرْشِهٖ وَ يُوَقِّرُ

Na kuhusu daraja yangu, basi jueni kuwa Mungu wangu Ananisifu kutoka kwa Arshi na kuniheshimu.

لَنَا جَنَّةٌ سُبُلُ الْهُدٰى اَزْهَارُهَا     نَسِيْمُ الصَّبَا مِنْ شَأْنِهَا تَتَحَيَّرُ

Tunayo Pepo ambayo njia za mwongozo wake ni maua yake na adhama ya upepo wake mwanana wa mashariki inastaajabisha.

تَكَدَّرَ مَاءُ السَّابِقِيْنَ وَ عَيْنُنَا     اِلٰى آخِرِ الْاَيَّامِ لَا تَتَكَدَّرُ

Maji ya waliotangulia yamechafuka, na maji yetu hayatachafuka hadi siku za mwiso.

رَأَيْنَا وَ اَنْتُمْ تَذْكُرُوْنَ رُوَاتَكُمْ     وَ هَلْ مِنْ نُّقُوْلٍ عِنْدَ عَيْنٍ تُبَصَّرُ

Tumeshaona, nanyi mnawataja tu wasimulizi wenu; na je visa vina thamani yoyote mbele ya kujionea mwenyewe?

وَ شَتَّانَ مَا بَيْنِيْ وَ بَيْنَ حُسَيْنِكُمْ     فَاِنِّيْ اُؤَيَّدُ كُلَّ اٰنٍ وَّ اُنْصَرُ

Na kuna tofauti kubwa kati yangu na Husain wenu, kwani mimi naauniwa saa zote na kusaidiwa na Mungu.

وَ اَمَّا حُسَيْنٌ فَاذْكُرُوْا دَشْتَ كَرْبَلَا     اِلٰى هٰذِهِ الْاَيَّامِ تَبْكُوْنَ فَانْظُرُوْا

Lakini Husain, basi ukumbukeni uwanja wa Karbala, mnalia hadi sasa. Fikirini, basi.

وَ اِنِّیْ بِفَضْلِ اللّٰہِ فِیْ حُجْرِ خَالِقِیْ اُرَبّٰی وَ اُعْصَمُ مِنْ لِّیَامٍ تَنَمَّرُوْا

Nami kwa fadhili ya Mungu, nalelewa mapajani mwa Muumbaji wangu, na daima nakingwa na mashambulizi ya watu duni wageukao kuwa chui.

وَ اِنْ یَّأْتِنِی الْاَعْدَاءُ بِالسَّیْفِ وَ الْقَنَا فَوَاللّٰہِ اِنِّیْ اُحْفَظَنَّ وَ اُظْفَرُ

Na maadui wakinijia na panga na mikuki, Wallahi nitahefadhiwa na kupata ushindi.

وَ اِنْ یُّلْقِنِیْ خَصْمِیْ بِنَارٍ مُّذِیْبَۃٍ تَجِدْنِیْ سَلِیْمًا وَّ الْعَدُوُّ یُدَمَّرُ

Na kama akinitupa katika moto uyeyushao, utanikuta nipo salama na adui atahilikishwa.

وَ اَوْعَدَنِیْ قَوْمٌ لِّقَتْلِیْ مِنَ الْعِدَا فَاَدْرَکَھُمْ قَھْرُ الْمَلِیْکِ وَ خُسِّرُوْا

Na baadhi ya maadui waliahidi kuniua; basi ghadhabu ya Mungu ikawashika na wakawa kuhasirika.

کَذَالِکَ تَبْغِیْ قَھْرَ رَبٍّ مُّحَاسِبٍ وَ مَا اِنْ أَرٰی فِیْکَ الْکَلَامَ یُؤَثِّرُ

Vivyo hivyo unaomba ghadhabu ya Mungu Mwenye kuhesabu; nami sioni kauli hii kukuathiri kitu.

بُعِثْتُ مِنَ اللّٰہِ الرَّحِیْمِ لِخَلْقِہٖ لِاُنْذِرَ قَوْمًا غَافِلِیْنَ وَ اُخْبِرُ

Nimetumwa na Mungu Rahimu kwa mahuluku Wake ili niwaonye walioghafilika, na niwajulishe.

وَ ذٰلِکَ مِنْ فَضْلِ الْکَرِیْمِ وَ لُطْفِہٖ عَلٰی کُلِّ مَنْ یَّبْغِی الصَّلَاحَ وَ یَشْکُرُ

Na ujaji wangu ni fadhili ya Mungu Karimu na hisani Yake juu ya wale wote wanaotaka wema na wanashukuru.

اَرَی النَّاسَ یَبۡغُوۡنَ الۡجِنَانَ نَعِیۡمَھَا     وَ اَحۡلٰی اَطَائِبِھَا الَّتِیۡ لَا تُحۡصَرُ

Nawaona watu wakitafuta Pepo na neema zake na starehe bora kabisa za Peponi zisizokoma.

وَ أَبۡغِیۡ مِنَ الۡمَوۡلٰی نَعِیۡمًا یَّسُرُّنِیۡ     وَ مَا ھُوَ اِلَّا فِیۡ صَلِیۡبٍ یُّکَسَّرُ

Na utashi wangu ni lengo nilifurahialo, nalo ni hili kwamba kwa njia yoyote msalaba uvunjiliwe mbali.

وَ ذٰلِكَ فِرۡدَوۡسِیۡ وَ خُلۡدِیۡ وَ جَنَّتِیۡ     فَاَدۡخِلۡنِ رَبِّیۡ جَنَّتِیۡ اَنَا اَضۡجَرُ

Hii ndiyo Firdausi yangu, Pepo yangu na Janna yangu; basi Ee Mola wangu, niingize katika Pepo yangu kwani ninacho kiherehere chake.

وَ اِنِّیۡ وَرِثۡتُ الۡمَالَ مَالَ مُحَمَّدٍ     فَمَا اَنَا اِلَّا آلُهُ الۡمُتَخَیَّرُ

Na nimefanywa mrithi wa mali ya Muhammad[saw]; basi mimi ndimi ali yake mteule niliyerithi.

وَ کَیۡفَ وَرِثۡتُ و لَسۡتُ مِنۡ اَبۡنَاءِهٖ     فَفَکِّرۡ وَ ھَلۡ فِیۡ حِزۡبِکُمۡ مُّتَفَکِّرُ

Na nilifanywaje kuwa mrithi wake ilhali mimi si miongoni mwa kizazi chake; ifikirie, basi, je hayupo mzingativu miongoni mwenu?

اَ تَزۡعَمُ اَنَّ رَسُوۡلَنَا سَیِّدَ الۡوَرٰی     عَلٰی زَعۡمِ شَانِیۡهِ تُوُفِّیَ اَبۡتَرُ

Je, unadhani kuwa Mtume[saw] wetu alikufa mkiwa kama anavyofikiri adui mwenye mdomo mchafu.

فَلَا وَ الَّذِیْ خَلَقَ السَّمَاءَ لِأَجْلِهٖ    لَهٗ مِثْلُنَا وُلْدٌ اِلٰی یَوْمِ یُحْشَرُ

Sivyo kabisa, naapa kwa Aliyeziumba mbingu; bali Mtume wetu[saw] anao watoto wengine pia kama mimi, na wataendelea kuwapo hadi Kiama.

وَ اِنَّا وَرِثْنَا مِثْلَ وُلْدٍ مَتَاعَهٗ    فَاَیُّ ثُبُوْتٍ بَعْدَ ذٰلِكَ یُحْضَرُ

Nasi tukamrithi kama watoto. Basi, kuna uthibitisho gani mwingine zaidi ya huu wa kutolewa?

لَهٗ خَسَفَ الْقَمَرُ الْمُنِیْرُ وَ اِنَّ لِیْ    غَسَا الْقَمَرَانِ الْمُشْرِقَانِ أَ تُنْكِرُ

Kwa ajili yake ishara ya kupatwa kwa mwezi ilidhihirika, na kwa ajili yangu mwezi na jua vyote viwili vikapatwa; je utakataa sasa?

وَ كَانَ كَلَامٌ مُعْجِزٌ آیَةً لَّهٗ    كَذٰلِكَ لِیْ قَوْلِیْ عَلَی الْكُلِّ یَبْهَرُ

Na miongoni mwa miujiza yake kulikuwa na kauli zake pia za kimuujiza; kadhalika nami nimejaliwa kauli ziwashindazo wote.

اِذَا الْقَوْمُ قَالُوْا یَدَّعِی الْوَحْیَ عَامِدًا    عَجِبْتُ فَاِنِّیْ ظِلُّ بَدْرٍ یُنَوِّرُ

Watu waliposema, huyu anadai kupata wahyi kwa ukaidi, nilishangaa kwani mimi ni kivuli cha Mtume[saw].

وَ اَنّٰی لِظِلٍّ اَنْ یُّخَالِفَ اَصْلَهٗ    فَمَا فِیْهِ فِیْ وَجْهِیْ یَلُوْحُ وَ یَزْهَرُ

Na kivuli kinawezaje kuhitilafiana na asili yake. Basi, nuru iliyomo ndani mwake yaangaza ndani mwangu.

وَ اِنِّيْ لَذُوْ نَسَبٍ كَاَصْلٍ اُطِيْعُهٗ    وَ مِنْ طِيْنِهِ الْمَعْصُوْمِ طِيْنِيْ مُعَطَّرُ

Nami ni mwenye nasaba tukufu kama Mtume[saw], na hamira ya udongo wake safi imo ndani mwangu.

كَفَى الْعَبْدَ تَقْوَى الْقَلْبِ عِنْدَ حَسِيْبِنَا    وَ لَيْسَ لِنَسْبٍ ذُوْ صَلَاحٍ مُعَيَّرُ

Na takwa ya moyo yamtosha mja mbele ya Mungu, na mtu mwema hawezi kulaumiwa kwa sababu ya nasaba yake isiyo takatifu.

وَ لٰكِنْ قَضٰى رَبُّ السَّمَا لِاَئِمَّةٍ    لَهُمْ نَسَبٌ كَيْلَا يَهِيْجَ التَّنَفُّرُ

Lakini, Mungu alitaka kwa maimamu wawe wenye nasaba njema ili watu wasiwachukie kwa sababu ya nasaba yao yenye upungufu.

وَ مَنْ كَانَ ذَا نَسَبٍ كَرِيْمٍ وَ لَمْ يَكُنْ    لَهٗ حَسَبٌ فَهُوَ الدَّنِيُّ الْمُحَقَّرُ

Na mtu ambaye ni mwenye nasaba nzuri lakini hana sifa njema, ni mtu duni na hakiri.

وَ لِلّٰهِ حَمْدٌ ثُمَّ حَمْدٌ فَاِنَّنَا    جَمَعْنَاهُمَا حَقًّا فَلِلّٰهِ نَشْكُرُ

Na sifa zote njema, tena sifa zote njema, ni za Mwenyezi Mungu kwani tumejikusanyia ndani mwetu nasaba na staha; basi tunamshukuru Mwenyezi Mungu.

كَذٰلِكَ سُنَنُ اللهِ فِيْ اَنْبِيَائِهٖ    جَرَتْ مِنْ قَدِيْمِ الدَّهْرِ فَاخْشَوْا وَ اَبْصِرُوْا

Ndivyo zilivyo suna za Mwenyezi Mungu ziendeleazo katika mitume wake tangu kale; basi ogopeni na angalieni.

وَ اَمَّا الَّذِیْ مَا جَاءَ مِثْلَ أَئِمَّةٍ فَلَيْسَ لِذَالِكَ شَرْطُ نَسَبٍ فَاَبْشِرُوْا

Lakini, asiye miongoni mwa maimau, hahitaji nasaba, basi furahini.

وَ مَا جِئْتُ اِلَّا مِثْلَ مَطَرٍ وَّ دِيْمَةٍ دَرُوْرٍ وَّ اَرْوَيْتُ الْبِلَادَ وَ اَعْمُرُ

Na nimekuja kama mvua kubwa na mvua inyeshayo polepole kudumu kutwa nzima na maji yake yanaendelea kutiririka, na nimerutubisha miji na kuifanya ifae kukalika.

وَ كَمْ مِّنْ اُنَاسٍ بَايَعُوْنِیْ بِصِدْقِهِمْ وَ مَا خَالَفُوْا قَوْلِیْ وَ مَا هُمْ تَذَمَّرُوْا

Na wapo wengi waliofanya baiati yangu kwa ukweli wa moyo, na hawakupinga maneno yangu wala hawakuwa na roho mbaya.

فَقَرَّبْتُ قُرْبَانًا يُّنَجِّیْ رِقَابَهُمْ وَ يَعْلَمُ رَبِّیْ مَا نَحَرْتُ وَ اَنْحَرُ

Basi, nikatoa dhabihu iliyowakomboa. Mola wangu Anajua dhabihu niliyotoa na ninayoendelea kutoa.

وَ لِیْ عِزَّةٌ فِیْ حَضْرَةِ اللهِ خَالِقِیْ فَطُوْبٰى لِقَوْمٍ طَاوَعُوْنِیْ واٰثَرُوْا

Nami ninayo heshima mbele ya Mungu wangu Aliye Mwumbaji wangu; basi wafurahie maisha mema walionitii na kunihiari.

أَتَى الْعِلْمُ بِالْمُتَقَدِّمِيْنَ وَ بَعْدَهُمْ تَلَافٰى جَمِيْعَ الْفَائِتَاتِ مُؤَخَّرُ

Elimu ikaja kwa njia ya waliotangulia na yaliyoponyoka kwao wakayasawazisha waliokuja baadaye.

وَ مَا اَنَا اِلَّا مِثْلَ مَالِ تِجَارَةٍ    فَمَنْ رَدَّنِيْ كِبْرًا اُبِيْدُوْا وَ خُسِّرُوْا

Na mimi ni kama mali ya biashara, basi walionikataa kwa kiburi wakaangamia na kupata hasara.

وَ مَا هَلَكَ الْاَشْرَارُ اِلَّا لِبُخْلِهِمْ    وَ مَا فَهِمُوْا اَقْوَالَنَا وَ تَنَمَّرُوْا

Na washari wakaangamia kwa sababu ya ubahili wao; hao hawakufahamu maneno yetu na wakageuka kuwa chui.

قُلُوْبٌ تُضَاهِيْ اَجَمَةً مَوْحُوْشَةً    فَمِنْ شَكْلِ اِنْسٍ وَحْشُهَا تَتَنَفَّرُ

Mioyo ya baadhi yao ni kama kichaka chenye wanyama wa porini. Basi hayawani hao wakiona sura ya binadamu huchukia.

كَبِيْرُ أُنَاسٍ شَرُّهُمْ فِيْ زَمَانِنَا    وَ اَعْقَلُهُمْ شَيْطَانُ قَوْمٍ وَ اَمْكَرُ

Katika zama zetu mkubwa ndiye yule aliye mshari sana. Na mwenye akili zaidi ndiye aliye shetani kati ya watu na mdanganyifu kuliko wote.

فَمَنْ يَّتَّقِيْ مِنْهُمْ وَ مَنْ كَانَ خَائِفًا    اُقَلِّبُ طَرْفِيْ كُلَّ آنٍ وَّ اَنْظُرُ

Basi, ni nani anayeogopa kati yao, na ni nani anayehofu saa zote, nageuza macho yangu kila upande na kutazama.

وَ مَنْ كَانَ فِيْهِمْ ذُوْ صَلَاحٍ كَنَادِرٍ    فَكَانَ غَرِيْبًا بَيْنَهُمْ لَا يُوَقَّرُ

Na atakayekuwa mwema kati yao kwa nadra, basi atakuwa ajinabi kati yao asiyeheshimika.

وَ جَاءَ كَرَهْطٍ حَوْلَهُمْ عَامَّةُ الْوَرٰى    شَطَائِبُ شَتّٰى مِثْلَ عُمْيٍ فَاَنْكَرُوْا

Na watu wa kawaida wakawajia kama jamii – makundi mbalimbali waliokuwa kama vipofu; basi wakakataa.

اَنَاخُوْا بِوَادٍ مَا رَأَى وَجْهَ خُضْرَةٍ وَ هَلْ عِنْدَ اَرْضٍ جَدْبَةٍ مَّا يُخَضِّرُ

Wakatua bondeni ambamo hamkuwa na mimea; na je mimea yaweza kuwapo katika ardhi kame?

فَأَبْكِيْ عَلٰى تِلْكَ الثَّلٰثَةِ بَعْدَهُمْ عَلٰى زُمْرَةٍ يَقْفُوْنَهُمْ اَتَحَسَّرُ

Basi, nawalilia hawa watatu, yaani Thana'ullah, Mehr Ali na Ali Ha'irii na pia nasikitikia kundi linaowafuasa.

وَ مَا اِنْ اَرٰى فِيْهِمْ مَّخَافَةَ رَبِّهِمْ شُعُوْبُ لِئَامٍ بِالْمَلَاهِيْ تَمَوَّرُوْا

Na sioni ndani yao hofu ya Mola wao; ni makundi yenye bahati mbaya wanaofurahia michezo yao.

وَ مَا قُمْتُ فِيْ هٰذَا الْمَقَامِ بِمُنْيَتِيْ وَ يَعْلَمُ رَبِّيْ سِرَّ قَلْبِيْ وَ يَشْعُرُ

Nami sikupata daraja hii kwa matamanio yangu; na Mola wangu Huzijua siri za moyo wangu.

وَ كُنْتُ امْرَءًا اَبْغِيْ الْخُمُوْلَ مِنَ الصِّبَا مَتٰى يَأْتِنِيْ مِنْ زَائِرِيْنَ اُصَعِّرُ

Na nilikuwa ni mtu niliyependa kujitenga na watu tangu nilipokuwa mdogo. Mtu alipokuwa akinijia kunitembelea nikajitenga naye.

فَأَخْرَجَنِيْ مِنْ حُجْرَتِيْ حُكْمُ مَالِكِيْ فَقُمْتُ وَ لَمْ اُعْرِضْ وَ لَمْ اَ تَعَذَّرُ

Basi, amri ya Bwana wangu ikanitoa chumbani mwangu, nami nikainuka na sikukengeuka wala kutoa udhuru.

وَ اِنِّيْ مِنَ الْمَوْلَى الْكَرِيْمِ وَ اِنَّهُ يُحَافِظُنِيْ فِيْ كُلِّ دَشْتٍ وَ يَخْفِرُ

Mimi ni kutoka kwa Mola Karimu, Naye ndiye Hunilinda katika kila msitu na kuniongoza.

فَكِيْدُوْا جَمِيْعَ الْكَيْدِ يَاأَيُّهَا الْعِدَا          فَيَعْصِمُنِيْ رَبِّيْ وَ هٰذَا مُقَدَّرُ

Basi nifanyieni kila aina ya hila, enyi maadui; Mola wangu Atanilinda, na hiyo ndiyo takdiri.

مَضٰى وَقْتُ ضَرْبِ الْمُرْهِفَاتِ وَ دَقُّهَا          وَ اِنَّا بِبُرْهَانٍ مِّنَ اللّٰهِ نَنْحَرُ

Zimeshapita siku za kupigana na panga; nasi tunachinja wakanao kwa hoja wazi ya Mwenyezi Mungu.

وَ لِلّٰهِ سُلْطَانٌ وَّحُكْمٌ وَّ شَوْكَةٌ          وَ نَحْنُ كُمَاةٌ بِالْاِشَارَةِ نَحْضُرُ

Ni ya Mwenyezi Mungu enzi, hukumu na utukufu; nasi tu wapanda farasi, tunahudhuria kwa kuashiriwa.

اِذَا مَا رَأَيْنَا حَائِرًا اَجْهَلَ الْوَرٰى          طَوَيْنَا كِتَابَ الْبَحْثِ وَالآىُ اَظْهَرُ

Na nilipomwona Ali Ha'irii, aliye jahili kuliko wote, nikasema, ishara tunazotoa ziko wazi, basi kuna haja gani ya majadiliano?

وَ مَا كُنْتُ بِالصَّمْتِ الْمُخَجِّلِ رَاضِياً          وَ لٰكِنْ رَّأَيْتُ الْقَوْمَ لَمْ يَتَبَصَّرُ

Nami sikuridhika na kimya cha aibu; laini niliona watu hawatafikiri.

اُخَاطِبُ جَهْرًا لَا اَقُوْلُ كَخَافِتٍ          فَاِنِّيْ مِنَ الرَّحْمٰنِ اُوْحٰى وَ اُخْبَرُ

Ninawaambia hadharani, si kisirisiri, kwani ninafunuliwa na kujulishwa na Mungu.

اَ يَا عَابِدَ الْحَسَنَيْنِ اِيَّاكَ وَ اللَّظٰى          وَ مَا لَكَ تَخْتَارُ السَّعِيْرَ وَ تَشْعُرُ

Ee mwabudu Husain na Hasan, uepuke moto wa Jahanamu; umekuwaje unachagua Jahanamu hali unajua.

وَ اَنْتَ امْرَءٌ مِّنْ اَهْلِ سَبٍّ وَّ اِنَّنَا رِجَالٌ لِاِظْهَارِ الْحَقَائِقِ نُؤْمَرُ

Nawe u mtu mwenye mdomo mchafu, nasi ndio watu tuanoamrishwa kudhihirisha kweli.

سَبَبْتَ وَ اِنَّ السَّبَّ مِنْ سُنَنِ دِيْنِكُمْ لِكُلِّ أُنَاسٍ سُنَّةٌ لَّا تُغَيَّرُ

Umetukana na kutukana ni kawaida yako; na kila mtu ana njia isiyobadilika.

تَرٰى سُقْمَ نَفْسِيْ مَا تَرٰى آىَ رَبِّنَا كَاَنَّكَ غُوْلٌ فَاقِدُ الْعَيْنِ اَعْوَرُ

Unaona dosari yangu, na huzioni ishara za Mola wetu, kana kwamba u ghuli mwenye jicho moja, chongo.

وَ مَا اَفْلَحَ الْعُمْرَانِ مِنْ ضَرْبِ لَعْنِكُمْ فَمِثْلِيْ لِهٰذَا اللَّعْنِ اَحْرٰى وَ اَجْدَرُ

Na Hadhrat Abu Bakr[ra] na Hadhrat Umar[ra] hawakusalimika na kulaaniwa nanyi; basi mtu kama mimi nastahili zaidi laana hiyo.

رُوَيْدَكَ دَأْبَ اللَّعْنِ هٰذَا وَصِيَّتِيْ وَ بَعْضُ الْوَصَايَا مِنْ مَّنَايَا تُذَكِّرُ

Achana na tabia ya kulaani; hii ni nasaha yangu; na baadhi ya wasia utakumbukwa wakati wa kufa.

وَ يَأْتِيْ زَمَانٌ يَسْتَبِيْنُ خِفَاءُنَا فَمَالَكَ لَا تَخْشٰى وَ لَا تَتَبَصَّرُ

Na unawadia wakati yatakapodhihirika maficho yetu; basi umekuwaje huogopi wala kutambua haki.

وَ لَا تَذْكُرُوا الْاَخْبَارَ عِنْدِيْ فَاِنَّهَا كَجَلْدَةِ بَيْتِ الْعَنْكَبُوْتِ تُكَسَّرُ

Na usinitajie riwaya hizo, kwani hizo zinaweza kuvunjiliwa mbali kama utando wa buibui.

وَ اَنّٰى لِاَخْبَارٍ مُّقَامٌ وَّمَوْقِفٌ   لَدٰى شَأْنِ فُرْقَانٍ عَظِيْمٍ مُعَزَّزُ

Na riwaya hizo zawezaje kujimudu mbele ya Kitabu hiki kilicho Neno la Mungu, Kurani Tukufu.

فَلَا تَقْفُ اَمْرًا لَسْتَ تَعْرِفُ سِرَّهٗ   فَتُسْأَلُ بَعْدَ الْمَوْتِ يَامُتَهَوِّرُ

Basi, usifuate jambo usilojua siri yake; nawe baada ya kufa lazima utaulizwa, ewe jasiri.

وَ لَسْتُ بِتَوَّاقٍ اِلٰى مَجْمَعِ الْعِدَا   وَ لٰكِنْ مَتٰى يَسْتَحْضِرُ الْقَوْمُ اَحْضُرُ

Na sina shauku ya kuendea hafla ya maadui; lakini wanaponiita wapinzani nahudhuria.

وَ لِلّٰهِ فِيْ اَمْرِيْ عَجَائِبُ لُطْفِهٖ   اُشَاهِدُهَا فِيْ كُلِّ وَقْتٍ وَّ اَنْظُرُ

Na Mungu Anayo maajabu ya hisani yake kuhusu mambo yangu; nayashuhudia kila wakati.

عَجِبْتُ لِخَتْمِ اللهِ كَيْفَ اَضَلَّكُمْ   فَمَا اِنْ اَرٰى فِيْكُمْ رَشِيْدًا يُّفَكِّرُ

Nastaajabia muhuri wa Mungu namna ulivyokuhukumuni kupotea. Sioni kati yenu mwenye akili afikiriye.

وَ هَلْ مِنْ دَلِيْلٍ عِنْدَكُمْ تُؤْثِرُوْنَهٗ   فَاِنْ كَانَ فَأْتُوْنَا فَاِنَّا نُفَكِّرُ

Na je mnayo hoja yoyote mnayoishikilia? Kama ipo, tuleteeni tutaifikiria.

سَيَجْزِى الْمُهَيْمِنُ كَاذِباً تَارِكَ الْهُدٰى   كِلَانَا اَمَامَ اللهِ لَا نَتَسَتَّرُ

Mwenyezi Mungu Atamwadhibu mwongo anayeacha mwongozo; sisi, makundi yote mawili, tupo mbele ya Mungu tusioweza kujificha Kwake.

اَ تَعْصُوْنَ بَغْيًا مَّنْ اَتٰى مِنْ مَّلِيْكِكُمْ     وَ قَدْ تَمَّتِ الْاَخْبَارُ وَ الْاٰىُ تَبْهَرُ

Je, nyinyi mnamwasi aliyekuja kutoka kwa Mfalme wenu, na bishara zimetimia na ishara zinang'aa.

وَ قَدْ قِيْلَ مِنْكُمْ يَأْتِيَنَّ اِمَامُكُمْ     وَ ذٰلِكَ فِي الْقُرْاٰنِ نَبَأٌ مُّكَرَّرُ

Na ilisemwa kwamba Imamu wenu atakuja kutoka miongoni mwenu, na habari hii imekaririwa mara nyingi katika Kurani.

اَتَانِيْ كِتَابٌ مِّنْ كَذُوْبٍ يُّزَوِّرُ     كِتَابٌ خَبِيْثٌ كَالْعَقَارِبِ يَأْبُرُ

Nimepokea kitabu kimoja kutoka kwa kadhabu – kitabu kichafu kiumacho kama nge.[38]

فَقُلْتُ لَكِ الْوَيْلَاتُ يَاأَرْضَ جَوْلَرَ     لُعِنْتِ بِمَلْعُوْنٍ فَاَنْتِ تُدَمَّرُ

Basi, nikasema, ewe ardhi ya Golra, laana iwe juu yako, kwani umelaaniwa kwa sababu ya maluuni; basi utakuwa maangamizini siku ya Kiama.

تَكَلَّمَ هٰذَا النِّكْسُ كَالزَّمْعِ شَاتِمًا     وَ كُلُّ امْرِءٍ عِنْدَ التَّخَاصُمِ يُسْبَرُ

Mnyonge huyu amezungumza akitukana kama watu duni; na kila mtu hujaribiwa wakati wa mabishano.

اَ تَزْعَمُ يَا شَيْخَ الضَّلَالَةِ اَنَّنِيْ     تَقَوَّلْتُ فَاعْلَمْ اَنَّ ذَيْلِيْ مُطَهَّرُ

Ewe sheikh wa upotovu, je unadhani nimezua uwongo? Ujue, basi, mimi ni mtu niliyetakasika.

[38] Hii ni kuhusu Pir Mehr Ali Shah.

اَ تُنْكِرُ حَقًّا جَآءَ مِنْ خَالِقِ السَّمَا سَيُبْدِیْ لَكَ الرَّحْمَانُ مَا أَنْتَ تُنْكِرُ

Je unakataa ukweli uliotoka kwa Mwumba wa mbingu; muda si mrefu Rahman Atakudhihirishia uyakanushayo.

اِذَا مَا رَأَيْنَا اَنَّ قَلْبَكَ قَدْ غَسَا فَفَاضَتْ دُمُوعُ الْعَيْنِ وَ الْقَلْبُ يَضْجَرُ

Tulipoona moyo wako umekuwa mweusi, kwa hiyo machozi yalitiririka machoni na moyo ukakosa utulivu.

اَخَذْتُمْ طَرِيْقَ الشِّرْكِ مَرْكَزَ دِيْنِكُمْ اَ هٰذَا هُوَ الْاِسْلَامُ يَا مُتَكَبِّرُ

Mmeifanya njia ya shirki kuwa kitovu cha dini yenu. Je huu ni Uislamu, ewe mwenye kiburi?

وَ مَا اَنَا اِلَّا نَائِبُ اللهِ فِي الْوَرٰى فَفِرُّوْا اِلَیَّ و جَانِبُوا الْبَغْیَ وَ احْذَرُوْا

Na mimi ni mjumbe wa Mungu kwa mahuluku, basi nikimbilieni, na acheni uasi, na jitahadharini.

وَ اِنَّ قَضَاءَ اللهِ يَأْتِیْ مِنَ السَّمَا وَ مَا كَانَ اَنْ يُّطْوٰى وَ يُلْغٰى وَ يُحْجَرُ

Na takdiri ya Mungu itakuja kutoka mbinguni; na haitayumkini kuiahirisha, na kuibatilisha na kuzuiliwa.

نَطَقْتَ بِكِذْبٍ اَيُّهَا الْغُوْلُ شَقْوَةً خَفِ اللهَ يَا صَيْدَ الرَّدٰى كَيْفَ تَجْسُرُ

Ewe ghuli, umeongopa kwa bahati mbaya. Ee windo la mauti, umwogope Mungu, mbona unajasiri.

اَ تَقْصِدُ عِرْضِیْ بِالْاَكَاذِيْبِ وَ الْجَفَا وَ اَنْتَ مِنَ الدَّيَّانِ لَا تَتَسَتَّرُ

Je unakusudia kunivunjilia heshima yangu kwa uzushi? Wewe hufichiki kwa Mwenye kuadhibu.

وَ اِنۡ تَضۡرِبَن علی الصَّلَاتِ زُجَاجَةً فَلَا الصَّخۡرُ بَلۡ اِنَّ الزُّجَاجَةَ تُکۡسَرُ

Kama ukipiga kioo kwenye jiwe, kioo tu kitavunjika sio jiwe.

تَعَالٰی مَقَامِیۡ فَاخۡتَفٰی مِنۡ عُیُوۡنِکُمۡ وَ کُلُّ رَفِیۡعٍ لَا مَحَالَۃَ یُسۡتَرُ

Daraja yangu ilikuwa juu sana, basi ikafichika kwa macho yenu; na kila kilicho mbali sana na juu kabisa chafichika pasipo shaka.

وَ فِیۡ حِزۡبِکُمۡ اِنَّا نَرٰی بَعۡضَ اٰیِنَا فَاِنَّا دَعَوۡنَا حِزۡبَکُمۡ فَتَأَخَّرُوۡا

Tulipata baadhi ya ishara zetu katika kundi lenu, kwani tuliliita kundi lenu, lakini wakabakia nyuma.

تَبَصَّرۡ خَصِیۡمِیۡ هَلۡ تَرٰی مِنۡ مَّطَاعِنٍ عَلَیَّ خُصُوۡصًا غَیۡرَ قَوۡمٍ تُطَهَّرُ

Ewe adui yangu, fikiria kwamba je ipo mikinzano dhidi yangu hasa na isiyowahusu manabii wengine unaowafahamu kuwa watakatifu?

وَ اَرۡسَلَنِیۡ رَبِّیۡ بِآیَاتِ فَضۡلِهٖ لِاَعۡمُرَ مَاهَدَّ اللِّئَامُ وَ دَعۡثَرُوۡا

Na Mungu Amenituma na ishara za fadhili yake ili nijenge jengo walilobomoa watu duni na kujengua.

وَ فِیۡ الدِّیۡنِ اَسۡرَارٌ وَّ سُبُلٌ خَفِیَّةٌ وَ یُظۡهِرُهَا رَبِّیۡ لِعَبۡدٍ یُخَیِّرُ

Na katika dini zimo siri na njia zilizofichikana, na Mola wangu humdhihirishia hizo mja Wake Anayemteua.

وَ كَمْ مِّنْ حَقَائِقَ لَا يُرٰى كَيْفَ شَبْحُهَا     كَنَجْمٍ بَعِيْدٍ نُوْرُهَا يَتَسَتَّرُ

Na kuna mambo mengi ya kweli ambayo sura zao hazionekani, kwa sababu ya kuwa mbali nuru zao zinafichika kama nyota iliyo mbali sana.

فَيَأْتِيْ مِنَ اللّٰهِ الْعَلِيْمِ مُعَلِّمٌ     وَ يَهْدِيْ اِلٰى اَسْرَارِهَا وَ يُفَسِّرُ

Kwa hiyo, mwalimu anafika kutoka kwa Mungu Mjuzi, na hufichua siri na kuzieleza.

وَ اِنْ كُنْتَ قَدْ آلَيْتَ اَنَّكَ تُنْكِرُ     فَكِذْنِيْ لِمَا زَوَّرْتَ فَالْحَقُّ يَظْهَرُ

Na ikiwa umeapa utaendelea kukataa, basi uendelee utakavyo kudanganya kwa uongo wako, lakini haki haina budi itadhihiri.

وَ سَوْفَ تَرٰى اَنِّيْ صَدُوْقٌ مُؤَيَّدٌ     وَ لَسْتُ بِفَضْلِ اللّٰهِ مَا اَنْتَ تَسْطُرُ

Na muda si mrefu utaona kwamba mimi ni mkweli na nimesaidiwa; nami, kwa fadhili ya Mungu, sivyo uandikavyo.

وَ يُبْدِيْ لَكَ الرَّحْمَانُ اَمْرِيْ فَيَنْجَلِيْ     اَ اِنِّيْ ظَلَامٌ اَوْ مِنَ اللّٰهِ نَيِّرُ

Na Mungu Atakudhihirishia uhakika wangu, basi itadhihirika je ni giza mimi au mwanga.

اُرِيْكَ وَ غَدَّارَ الزَّمَانِ اَبَا الْوَفَا     يَدَ اللّٰهِ فَالضَّوْضَاةُ يُخْفٰى وَ يُسْتَرُ

Nitakuonyesha wewe na msaliti wa zama, Thana’ullah, Mkono wa Mungu, basi, kelele zote zitakoma.

وَ يَعْلَمُ رَبِّيْ مَنْ تَصَلَّفَ وَ افْتَرٰى     وَ مَنْ هُوَ عِنْدَ اللّٰهِ بَرٌّ مُّطَهَّرُ

Na Mola wangu Anajua ni nani mkorofi na mzushi, na yu nani aliye mwema na mtakatifu mbele Yake.

اَ تُطْفِئُ نُوْرًا قَدْ اُرِيْدَ ظُهُوْرُهٗ     لَكَ الْبُهْرُ فِي الدَّارَيْنِ وَ النُّوْرُ يَبْهَرُ

Je unataka kuzima nuru inayokusudiwa kudhihirishwa; una bahati mbaya duniani na Akhera; na nuru haina budi kudhihirika.

اَ لَا اِنَّ وَقْتَ الدَّجْلِ وَ الزُّوْرِقَدْ مَضٰى     وَ جَاءَ زَمَانٌ يُحْرِقُ الْكِذْبَ فَاصْبِرُوْا

Sikiliza, wakati wa udanganyifu na uongo umepita, na umewadia wakati utakaomteketeza mwongo, basi subiri tu.

وَ اِنْ كُنْتَ قَدْ جَاوَزْتَ حَدَّ تَوَرُّعٍ     فَكَفِّرْ وَ كَذِّبْ اَيُّهَا الْمُتَهَوِّرُ

Na ikiwa umevuka mipaka ya takwa, basi nikufurishe na kukadhibisha, ewe jasiri!

اَيَا اَيُّهَا الْمُؤْذِيْ خَفِ الْقَادِرَ الَّذِيْ     يَشُجُّ رُؤُوْسَ الْمُعْتَدِيْنَ وَ يَقْهَرُ

Ee msumbufu, Mche Mungu Mweza Anayeponda vichwa vya warukao mipaka na kuwashushia ghadhabu.

اِذَا مَا تَلَظّٰى قَهْرُهٗ يُهْلِكُ الْوَرٰى     فَلَيْسَ بِوَاقٍ بَعْدَهٗ يَا مُزَوِّرُ

Akasirikapo sana huwahilikisha watu, kisha baada yake hakuna mwenye kulinda, ewe mwongo!

وَ لَسْتَ تُرَاعِيْ نَهْجَ رِفْقٍ وَ لِيْنَةٍ     كَذَأْبِ ثَنَاءِ اللّٰهِ تُؤْذِيْ وَ تَأْبُرُ

Na huzingatii njia ya kutumia upole na ulainifu, bali unauma kama Maulawii Thana'ullah.

اَ لَا اِنَّ حُسْنَ النَّاسِ فِیْ حُسْنِ خُلْقِهِمْ    وَ مَنْ یَّقْصِدِ التَّحْقِیْرَ خُبْثًا یُحَقَّرُ

Sikiliza, uzuri wa watu uko katika uzuri wa huluka zao, na anayedharau kwa ukorofi, huyo naye hudharauliwa.

أَ آخَیْتَ ذِئْبًا عَایِثًا اَوْ اَبَا الْوَفَا    أَ وَافَیْتَ مُدًّا اَوْ رَأَیْتَ امْرَتْسَرُ

Je ulifanya urafiki na mbwamwitu au Maulawii Thana'ullah? Je, Uliijia Mudd au Amritsar?

اَلَا اِنَّ اَهْلَ السَّبِّ یُدْرَی بِلَطْمَةٍ    وَ مُجْرِمُ لَطْمٍ بِالْهَرَاوٰی یُکَسَّرُ

Sikiliza, mtukanaji huonywa kwa kupigwa kofi; na mkosefu wa kupiga kofi hutandikwa bakora.

فَاِیَّاكَ وَ التَّوْهِیْنَ وَ السَّبَّ وَ الْقَلٰی    اِذَا مَا رَمَیْتَ الْحَجَرَ بِالْحَجَرِ تُنْذَرُ

Basi, jiepushe na dharau, matusi na uadui; ukitupia jiwe, utaonywa kwa kutupiwa jiwe.

وَ اَعْلَمُ اَنَّ اللَّعْنَ وَ السَّبَّ دَأْبُکُمْ    وَ مَنْ اَکْثَرَ التَّکْفِیْرَ یَوْمًا سَیُکْفَرُ

Nami najua kuwa kulaani na kutukana ni tabia yenu; na atakayekithiri kukufurisha, yeye naye atakufurishwa siku moja.

وَ اِنَّا وَ اِیَّاکُمْ اَمَامَ مَلِیْکِنَا    فَیَقْضِیْ قَضَایَانَا کَمَا هُوَ یَنْظُرُ

Sisi na nyinyi tuko mbele ya Mungu, basi Ataamua kesi yetu kama aonavyo.

فَاِنْ کُنْتُ کَذَّابًا کَمَا اَنْتَ تَزْعَمُ    فَتُعْلٰی وَ اِنِّیْ فِی الْاَنَامِ اُحَقَّرُ

Basi kama mimi ni mwongo kama udhanivyo, basi utanyanyuliwa na nitadharauliwa kati ya watu.

وَ اِنْ كُنْتُ مِنْ قَوْمٍ اَتَوْا مِنْ مَّلِيْكِهِمْ          فَتُجْزٰى جَزَاءَ الْمُفْسِدِيْنَ وَ تُبْتَرُ

Na kama mimi ni miongoni mwa waliotoka kwa Mfalme wao, basi utaadhibiwa wanavyoadhibiwa mafisadi.

وَ اَقْسَمْتُ بِاللّٰهِ الَّذِىْ جَلَّ شَاْنُهُ          سَيُكْرِمُنِىْ رَبِّىْ وَ شَاْنِىْ يُكَبَّرُ

Nami naapa kwa Mungu, ambaye utukufu ni Wake, kwamba Yeye atanipa heshima, na jaha yangu itazidishwa sana.

شَعَرْنَا مَاٰلَ الْمُفْسِدِيْنَ وَ مَنْ يَّعِشْ          اِلٰى بُرْهَةٍ مِنْ بَعْدِ ذٰلِكَ يَشْعُرُ

Tumeshajua mwisho wa mafisadi na yeyote atakayeishi kwa muda kidogo yeye pia atajua.

وَ فِى الْاَرْضِ اَحْنَاشٌ وَ سَبْعٌ وَ شَرُّهُمْ          رِجَالٌ اَهَانُوْنِىْ وَ سَبُّوْا وَ كَفَّرُوْا

Na katika ardhi kuna nyoka na wanyama mbuai pia, lakini mbaya zaidi ni wale watu wanaonidharau na kunitukana na kunikufurisha.

مَنَعْنَا مِنَ الْكِذْبِ الْكَثِيْرِ فَكَاثَرُوْا          وَ شَرُّ خِصَالِ الْمَرْءِ كِذْبٌ يُّكَرِّرُ

Tuliwakataza wasiongope sana, lakini wakakithiri kuongopa; na sifa mbaya kabisa ya mtu ni uongo anaoukariri-kariri.

كَتَبْتَ فَوَيْلٌ لِّلْاَنَامِلِ وَ الْقَلَمِ          وَ تَبَّتْ يَدٌ تُغْوِى الْاَنَامَ وَ تَهْذُرُ

Uliandika kitabu chako; ole wake kalamu hiyo na vidole hivyo, na umeangamia mkono unaowapoteza watu na kuandika upuuzi.

وَ كَيْفَ الْفَرَاغَةُ لِلرِّسَالَةِ حُصِّلَتْ    اَ لَمْ يَكُ طَنْبُوْرٌ وَّ مَا اَنْتَ تَزْمُرُ

Na ulipataje fursa ya kuandika kijitabu; je hukuwa na gambusi na zeze.

اُوَانِسُ رِجْزَ الْكِذْبِ فِيْهَا كَأَنَّهَا    كَنِيْفٌ وَ قَدْ عَايَنْتُ وَ الْعَيْنُ تَقْذُرُ

Nauona uchafu wa uongo katika kijitabu hicho kana kwamba ni msalani; nikakitazama na macho yakatiririka.

زَمَانٌ يَسُحُّ الشَّرَّ عَنْ كُلِّ فِيْقَةٍ    وَ زَلْزَلَةٌ اَرْدَى الْاُنَاسَ وَ صَرْصَرُ

Hizi ni zama zitiririshazo maji kutoka katika wingu la shari mara kwa mara, na ni tetemeko lililowahilikisha watu, na ni upepo mkali unaovuma kwa kasi.

فَفِيْ هٰذِهِ الْاَيَّامِ يُطْرَى ابْنُ مَرْيَمٍ    مَسِيْحٌ اَضَلَّ بِهِ النَّصَارٰى وَ خَسَّرُوْا

Basi, siku hizi Kristo anasifiwa ambaye kwa njia yake Wakristo waliwapoteza viumbe na kuwaangamiza.

كَذٰلِكَ فِي الْاِسْلَامِ عَاثَ تَشَيُّعٌ    اَبَادُوْا كَثِيْرًا كَاللُّصُوْصِ وَ دَمَّرُوْا

Kadhalika madhehebu ya Shia yameenea katika Islam; hao wamehilikisha wengi kama wezi.[39]

نَرٰى شِرْكَهُمْ مِثْلَ النَّصَارٰى مُخَوِّفًا    نَرَى الْجَاهِلِيْنَ تَشَيَّعُوْا وَ تَنَصَّرُوْا

Tunaona shirki yao inaogofia kama ile ya Wakristo, tunawaona majahili wanaingia katika Ushia na Ukristo pia.[40]

---

[39] Beti hizi ni kuhusu Mshia Sheikh Ali Ha'irii.

[40] Beti hizi ni kuhusu Mshia Sheikh Ali Ha'iri.

فَتُبْ وَ اتَّقِ الْقَهَّارَ رَبَّكَ يَا عَلِيْ    وَ اِنْ كُنْتَ قَدْ اَزْمَعْتَ حَرْبِيْ فَاَحْضُرُ

Basi, Ewe Ali Ha'irii, mche Mola wako na tubu. Na kama umekusudia kukabiliana nami basi nipo tu.[41]

عَكَفْتُمْ عَلٰى قَبْرِ الْحُسَيْنِ كَمُشْرِكٍ    فَلَا هُوَ نَجَّاكُمْ وَ لَا هُوَ يَنْصُرُ

Mlifanya itikafu kwenye kaburi la Husain kama washirikina, lakini hakuweza kuwakomboeni wala kusaidia.

اَلَا رُبَّ يَوْمٍ كَانَ شَاهِدَ عَجْزِكُمْ    وَ لَا سِيَّمَا يَوْمٌ اِذَا الصَّحْبُ خُيِّرُوْا

Sikilizeni, zipo siku nyingi zilizo mashahidi wa kushindwa kwenu; hususani siku ambapo Abu Bakr[ra] na Umar[ra] na Uthman[ra] walipokuwa Makhalifa na Hadhrat Ali[ra] akaahirishwa.

وَ يَوْمَ فَعَلْتُمْ مَّافَعَلْتُمْ بِغَدْرِكُمْ    بِاَخِّ الْحُسَيْنِ وَ وُلْدِهٖ اِذْ اُحْصِرُوْا

Na siku mlipofanya mliyofanya kumsaliti nduguye Husain, Muslim, na watoto wake walipofungwa.

فَظَلَّ الْاُسَارٰى يَلْعَنُوْنَ وَفَائَكُمْ    فَرَرْتُمْ وَ اَهْلُ الْبَيْتِ اُوْذُوْا وَ دُمِّرُوْا

Basi wale wafungwa, yaani *Ahli Bait*, wakaulaani uaminifu wenu; mkakimbia, na *Ahli Bait* wakateswa na kuuawa.

هُنَاكَ تَرَاءٰى عَجْزُ مَنْ تَحْسَبُوْنَهٗ    شَفِيْعَ النَّبِيِّ مُحَمَّدٍ فَتَفَكَّرُوْا

Ndipo uajazi na udhaifu wa mtu huyo, yaani Husain, ukadhihirika mliyemdhania atamfanyia maombezi hata Nabii Mtukufu[saw] siku ya Kiama.

---

[41] Beti hizi ni kuhusu Mshia Sheikh Ali Ha'iri.

زَعَمْتُمْ حُسَيْنًا اَنَّهُ سَيِّدُ الْوَرٰى    وَ كُلُّ نَبِيٍّ مِّنْهُ يَنْجُوْ وَ يُغْفَرُ

Mnafikiri Husain ndiye mkuu wa mahuluku wote, na kila nabii ataokolewa na kusamehewa kwa maombezi yake.

فَاِنْ كَانَ هٰذَا الشِّرْكُ فِي الدِّيْنِ جَائِزًا    فَبِاللَّغْوِ رُسُلُ اللهِ فِي النَّاسِ بُعْثِرُوْا

Basi, kama shirki hii ingejuzu katika dini, Mitume wote wangehesabiwa kutumwa bure tu.

وَ ذٰلِكَ بُهْتَانٌ وَّ تَوْهِيْنُ شَأْنِهِمْ    لَكَ الْوَيْلُ يَا غُوْلَ الْفَلَا كَيْفَ تَجْسُرُ

Na huku ni kuwasingizia na kuwakabehi Mitume wote[as]. Ole wako, ee ghuli wa misitu; mbona unajasiri hivyo!

طَلَبْتُمْ فَلَاحًا مِّنْ قَتِيْلٍ بِخَيْبَةٍ    فَخَيَّبَكُمْ رَبٌّ غَيُوْرٌ مُّتَبِّرٌ

Mlitaka kuokolewa na yule aliyekufa kwa kukata tamaa; basi, Mungu Mwangamizi Mwenye ghera Akawakatisha tamaa kupata kila muradi.

وَ وَاللهِ لَيْسَتْ فِيْهِ مِنِّىْ زِيَادَةٌ    وَ عِنْدِىْ شَهَادَاتٌ مِّنَ اللهِ فَانْظُرُوْا

Na Wallahi yeye hana yoyote zaidi yangu. Nami ninazo shuhuda za Mungu, basi mziangalie.

وَ اِنِّىْ قَتِيْلُ الْحِبِّ لٰكِنْ حُسَيْنُكُمْ    قَتِيْلُ الْعِدَا فَالْفَرْقُ اَجْلٰى وَ اَظْهَرُ

Na mimi nimeuawa na Mpenzi wangu Mungu, lakini Husain wenu aliuawa na maadui; basi tofauti ni dhahiri shahiri.

حَدَرْنَا سَفَائِنُكُمْ اِلٰى اَسْفَلِ الثَّرٰى    وَ اَوْثَانَكُمْ فِىْ كُلِّ وَقْتٍ نُكَسِّرُ

Tumeteremsha boti zenu chini kabisa, na tunavunjilia mbali kila saa sanamu zenu.

وَ وَاللهِ اِنَّ الدَّهۡرَ فِي كُلِّ وَقۡتِهٖ          نَصِيۡحٌ لَكُمۡ فِيۡ نُصۡحِهٖ لَا يُقَصِّرُ

Na Wallahi zama zinawanasihini kila wakati, na haziachi kasoro katika nasaha yake.

تَنَاهٰى لِسَانُ النَّاسِ عَنۡ دَاۡبِ فُحۡشِهِمۡ          وَ مِقۡوَلُكُمۡ يَجۡرِىۡ وَ لَا يَتَحَسَّرُ

Watu wote waliacha tabia ya kutukana, lakini ulimi wenu unaendelea kulaani wala hauchoki.

اَشَعۡتُمۡ طَرِيۡقَ اللَّعۡنِ فِيۡ اَهۡلِ سُنَّةٍ          فَاَجۡرَوۡا طَرِيۡقَتُكُمۡ فَاِنۡ شِئۡتُمۡ انۡظُرُوۡا

Mmeeneza njia za kulaani katika Masuni; basi na hao pia wakaanzisha njia hii yenu, angalieni mkitaka.

فَيَالَيۡتَ مِتُّمۡ قَبۡلَ تِلۡكَ الطَّرَائِقِ          وَ لَمۡ يَكُ دِيۡنُ اللهِ مِنۡكُمۡ يُخَسَّرُ

Laiti mngejifia kabla ya kuanzisha njia hizi zote, na dini ya Mungu isingeangamia kwa sababu yenu.

جَعَلۡتُمۡ حُسَيۡنًا اَفۡضَلَ الرُّسۡلِ كُلِّهِمۡ          وَ جُزۡتُمۡ حُدُوۡدَ الصِّدۡقِ وَ اللهُ يَنۡظُرُ

Mmemfanya Husain kuwa mbora kuliko manabii wote, nanyi mkavuka mipaka ya haki, na Mwenyezi Mungu Hutazama.

وَ عِنۡدَ النَّوَائِبِ وَ الۡاَذٰى تَذۡكُرُوۡنَهٗ          كَاَنَّ حُسَيۡنًا رَبُّكُمۡ يَا مُزَوِّرُ

Na wakati wa taabu na huzuni mnamkumbuka, kana kwamba Husain ndiye Mola wenu, ewe mwongo *mwenye bahati mbaya*!

وَ خَرَّتْ لَهُ اَحْبَارُكُمْ مِثْلَ سَاجِدٍ          فَمَا جُرْمُ قَوْمٍ اَشْرَكُوْا أَوْ تَنَصَّرُوْا

Na wanachuoni wenu wakaanguka mbele yake kama mwenye kusujudu. Basi, na washirikina au Wakristo wamefanya dhambi gani!

نَسِيْتُمْ جَلَالَ اللهِ وَ الْمَجْدَ وَ الْعُلٰى          وَ مَا وِرْدُكُمْ اِلَّا حُسَيْنٌ اَتُنْكِرُ

Mmesahau adhama na utukufu wa Mungu, na uradi wenu ni 'Husain' tu; je unakanusha?

فَهٰذَا عَلَى الْاِسْلَامِ اِحْدَى الْمَصَائِبِ          لَدٰى نَفَحَاتِ الْمِسْكِ قَذْرٌ مُّقَنْطَرُ

Basi, huu ni msiba mmojawapo wa Islam, ni rundo la kinyesi kando ya mnukio wa miski.

وَ اِنْ كَانَ هٰذَا الشِّرْكُ فِي الدِّيْنِ جَائِزًا          فَبِاللَّغْوِ رُسُلُ اللهِ فِي النَّاسِ بُعْثِرُوْا

Na ikiwa shirki inajuzu katika dini[42] basi watu walipelekewa bure Mitume wa Mungu.

---

[42] Tanbihi: Maana ya ubeti huu ni kwamba kama shirki ilijuzu na makafiri walianza kuwaua Waislamu kwa ajili tu ya kuwasaidia miungu wasiokuwa Mungu kama Husain, na baada ya hapo Waislamu wakaruhusiwa kupigana na washirikina hao, basi kulikuwa na haja gani ya kupigana nao; bali washirikina wakapaswa kuambiwa kuwa nyinyi m wakweli katika kushika shirki na shahada ya 'La Ilaha Illallahu' ni batili, hivyo tafadhalini acheni vita wala msituudhi. Sisi hatupigani nanyi na twakubali kuwa kuwaomba minghairi ya Mungu mahitaji ni sahihi wala hatulipingi jambo hili.

وَ اَیُّ صَلَاحٍ سَاقَ جُنْدَ نَبِیِّنَا      اِلٰی حَرْبِ حِزْبِ الْمُشْرِکِیْنَ فَدَمَّرُوْا

Na kwa manufaa gani jeshi la Nabii wetu[saw] likaenda kwa kupigana na washirikina, na kuwaangamiza.

وَ شَنُّوْا عَلَیْهِمْ کُلَّ شَنٍّ بِمَوْطِنٍ      فَصَارَ مِنَ الْقَتْلٰی بَرَازٌ مُعَصْفَرُ

Na kwa juhudi zao wakawaangamiza washirikiana hao uwanjani mwa vita mpaka medani ikawa nyekundu.

وَ کَمْ مِّنْ زِرَاعَاتٍ اُبِیْدَتْ وَ مِثْلُهَا      بُیُوْتٌ مَبِیْتَاةٌ وَّ طِرْفٌ مُّصَدِّرُ

Na mashamba mengi yakaharibiwa, na nyumba zikafutiliwa, na farasi waliokuwa wakishinda katika shindano la mbio wakauawa.

وَ اُحْرِقَ مَالُ الْمُشْرِکِیْنَ وَ حُصِّلَتْ      مَغَانِمُ شَتّٰی وَ الْمَتَاعُ الْمُوَقَّرُ

Na nyumba na mali za washirikina zikachomwa moto, na nyara nyingi na mali tele zikatekwa.

بِبَدْرٍ وَّ اُحُدٍ قَامَ نَوْعُ قِیَامَةٍ      وَ کَانَ الصَّحَابَةُ کَالْاَفَانِیْنِ کُسِّرُوْا

Katika vita ya Badr na Uhud shida kama ya Kiama ilitokea, na Masahaba[ra] walivunjwa kama matawi.

هَمَتْ مِثْلَ جَرْیَانِ الْعُیُوْنِ دِمَاءُهُمْ      تَسَوَّرَ دِعْصَ الرَّمْلِ مَا کَانَ یَقْطُرُ

Na damu zao zilitiririka kama chemchemi, na damu yao ilipanda juu ya rundo la mchanga.

وَ کَانَ بِجُرِّ الرَّمْلِ مَوْقِفُهُمْ فَهُمْ      عَلٰی رِسْلِهِمْ بَارَوْا عِدَاهُمْ وَ جَمَّرُوْا

Walikuwa katika sehemu yenye mchanga mtupu, lakini wakawakabili maadui zao kinyerenyere na wakasimama imara vitani.

وَ قَامُوْا لِبَذْلِ نُفُوْسِهِمْ مِنْ صِدْقِهِمْ    عَلٰى مَوْطِنٍ فِيْهِ الْمَنِيَّةُ يَزْئَرُ

Wakasimama kwa kutoa uhai wao kwa uaminifu wao mahali yaliponguruma mauti kama simba.

وَ صُبَّتْ عَلٰى رَأْسِ النَّبِيِّ مُصِيْبَةٌ    وَ دَقُّوْا عَلَيْهِ مِنَ السُّيُوْفِ الْمِغْفَرُ

Na taabu ikamsibu Mtukufu Nabii[saw], na maadui zake kwa kupiga panga wakaingiza helmeti yake kichwani mwake.

عَلٰى مِثْلِهَا لَمْ نَطَّلِعْ فِيْ مُكَلَّمٍ    وَ اِنْ كَانَ عِيْسٰى اَوْ مِنَ الرُّسْلِ اٰخَرُ

Hakuna mfano wa misiba hiyo katika nabii mwingine yeyote, awe Isa au nabii mwingine yeyote awaye.

فَفَكِّرْ أَ هٰذَا كُلُّهٗ كَانَ بَاطِلًا    وَ مَا كَانَ شِرْكُ النَّاسِ شَيْئًا يُغَيَّرُ

Basi, tafakari, je hayo yote yalikuwa batili, na shirki haikuwa ni kitu kinachoweza kubadilishwa?

اَلَا لَائِمِيْ عَارَ النِّسَاءِ اَبَا الْوَفَا    اِلَامَ كَفِتْيَانِ الْوَغٰى تَتَنَمَّرُ

Ewe aibu kwa wanawke, Thana’ullah unayenilaumu, mpaka lini utaonyesha mwenendo wa chui kama mabingwa wa vita.

أَرُدْتُّ الْهَوٰى مِنْ بَعْدِ سِتِّيْنَ حِجَّةً؟    وَ ذٰلِكَ رَأْيٌ لَا يَرَاهُ الْمُفَكِّرُ

Je, nilifuata matamanio baada ya umri wa miaka sitini? Hii ndiyo rai isiyokuwa ya mwenye lubu.

اَرَيْنَاكَ اٰيَاتٍ فَلَا عُذْرَ بَعْدَهَا     وَ اِنْ خِلْتَهَا تُخْفٰى عَلَى النَّاسِ تُظْهَرُ

Tunakuonyesheni ishara kadha na baada yake hautabaki udhuru. Na ukidhania hizo zitafichika, basi ujue hazitafichika hata kidogo.

اَرَدْتَّ بِمُدٍّ ذِلَّتِىْ فَرَأَيْتَهَا     وَ مَنْ لَّا يُوَقِّرْ صَادِقًا لَّا يُوَقَّرُ

Ulitaka dhila yangu huko Mudd, basi mwenyewe ukadhalilika. Na anayemvunjia heshima mkweli, mwenyewe atavunjiwa heshima.

وَ كَاُيِنْ[43] مِّنَ الْاٰيَاتِ قَدْ مَرَّ ذِكْرُهَا     رَأَيْتُمْ فَاَعْرَضْتُمْ وَ قُلْتُمْ تُزَوِّرُ

Na zipo ishara nyingi tulizoishazitaja. Uliziona ishara hizo, ukazikanusha na ukasema ‘unaongopa’.

فَعَنَّ لَنَا بَعْدَ التَّجَارِبِ حِيْلَةٌ     لِنَكْتُبَ اَشْعَارًا بِهَا الآىَ تَشْعُرُ

Basi, baada ya tajriba nyingi ikatudhihirikia njia moja ya kutunga beti hizi chache, ambazo kwazo upate kujua ishara hizo.

فَهٰذَا هُوَ التَّبْكِيْتُ مِنْ فَاطِرِ السَّمَا     وَ هٰذَا هُوَ الْاِفْحَامُ مِنِّىْ فَفَكِّرُوْا

Kwa njia hii Mungu Anataka kufumba mdomo wako; na huu ndio ukamilisho wa hoja kutoka kwangu; basi zingatieni.

اَثَارَتْ سَنَابِكُ طِرْفِنَا نَقْعَ فَوْجِكُمْ     فَهَلْ مِنْ كَمِيٍّ لِّلْوَغٰى يَتَبَخْتَرُ

Kwato za farasi wetu ziliangamiza kikosi chenu. Basi, je yupo mpanda farasi kati yenu ajitokezaye katika medani?

---

[43] يستعمل لفظ كاُيِنْ كما يستعمل كَاَيِّنْ فى لسان العرب۔ منه

اَ تُثْبِتُ عَظْمَةَ آيَتِيْ بِتَقَاعُسٍ     وَ قَدْ جِئْتَ مُدًّا سَاعِيًا لِّتُحَقِّرُ

Je, kwa kurudi nyuma sasa utathibitisha ishara yangu ilhali huko Mudd ukaja mbiombio kunihakirisha.

فَاِنْ تُعْرِضَنَّ الْاٰنَ يَاابْنَ تَصَلُّفٍ     فَهٰذَا عَلٰى بَطْنِ الْمُكَذِّبِ خَنْجَرُ

Kama sasa unakengeuka na kukabiliana, basi njia hii ni hanjari tumboni mwa mkadhibishaji.

وَ اِنْ كُنْتَ تَخْتَارُ الْهَزِيْمَةَ عَامِدًا     وَ تَهْوِيْ بِوَهْدِ الذُّلِّ عَجْزًا وَّ تَحْدُرُ

Na ukichagua kushindwa makusudi, na kuanguka shimoni mwa dhila kwa unyenyekevu,

فَفِيْهَا نَكَالُ الْعٰلَمِيْنَ وَ لَعْنَةٌ     وَ فِيْهَا فَضِيْحَتُكُمْ اَلَا تَتَذَكَّرُ

Basi humo mna adhabu na laana ya dini na dunia, na humo mna fedheha yako; je hufikiri?

وَ مَا لَكَ لَا تَسْطِيْعُ اِنْ كُنْتَ صَادِقًا     لِاَهْلِ صَلَاحٍ كُلُّ اَمْرٍ مُيَسَّرُ

Na ikiwa u mkweli, basi kwa nini huna nguvu ya kushindana? Na watu wema hurahisishiwa kila jambo.

وَ كُنْتَ اِذَا خُيِّرْتَ لِلْبَحْثِ وَالْوَغَا     سَطَوْتَ عَلَيْنَا شَاتِمًا لِتُوَقَّرُ

Na ulipochaguliwa kwa mjadala huko Mudd, ulitushambulia ili uheshimiwe hivyo.

لَعَمْرِيْ لَقَدْ شَجَّتْ قَفَاكَ رِسَالَتِيْ     وَ اِنْ مِتَّ لَايَأْتِيْكَ عَوْنٌ مُّعَزِّرُ

Na naapa kwamba kijitabu changu kiliponda kichwa chako, na sasa hata ukijifia hutapata msaada utakaokupa heshima.

وَ كَيْفَ وَ اَنْتُمْ قَدْ تَرَكْتُمْ مُعِيْنَكُمْ    وَ لَيْسَ لَكُمْ مَوْلٰى وَ مَنْ هُوَ يَنْصُرُ

Na msaada ungekufikiaje ilhli umeshaachana na Mungu, na sasa huna Mola wala Mwenye kukusaidia.

اَ فِيْكُمْ كَمِيٌّ ذُوْ نِضَالٍ شَمَرْدَلٌ    فَاِنْ كَانَ فَلْيَحْضُرْ وَ لَا يَتَأَخَّرُ

Je yupo mpandaji farasi kati yenu, mpiganaji, shujaa? Kama yupo, basi ahudhurie na asichelewe.

وَ جِئْنَاكَ يَا صَيْدَ الرَّدٰى بِهَدِيَّةٍ    وَ نُهْدِى اِلَيْكَ الْمُرْهِفَاتِ وَ نَعْقِرُ

Na Ee windo la maangamio, tumekuletea zawadi, nasi tunakupa zawadi ya panga kali, yaani kasida bora isiyojibika.

فَاَبْشِرْ وَ بَشِّرْ كُلَّ غُوْلٍ يَسُبُّنِىْ    سَيَأْتِيْكَ مِنِّىْ بِالتَّحَائِفِ سَرْوَرُ

Basi, ufurahi na mtolee habari njema kila ghuli aliyekuwa akinitukana. Muda si muda, Seyid Muhammad Sarwar atakujia na zawadi kutoka kwangu.

وَ اِنِّىْ اَنَا الْبَازِى الْمُطِلُّ عَلَى الْعِدَا    وَ اِنِّىْ مُعَانٌ مِّنْ مُّعِيْنٍ يُّكَبَّرُ

Na mimi ndiye tai ninayeshambulia maadui, nami nimesaidiwa na Mwenyezi Mungu.

اَثِرْ كُلَّ شَرْقِيِّ الْبِلَادِ وَ غَرْبِهَا    وَ كُلَّ اَدِيْبٍ كَانَ كَالْبَقِّ يَطْمِرُ

Basi, wachochee wa mashariki na wa magharibi dhidi yangu na mwite kila mwandishi aliyekuwa akirukaruka kama mbu.

وَ مَنۡ کَانَ یَحۡکِیۡ نَاقَۃً مُشۡمَعِلَّۃً　　　صَغَارٌ یَمُسُّ الۡقَوۡمَ فَاسۡعَوۡا وَ دَبِّرُوۡا

Na mwite mtu atembeaye haraka kama ngamia jike, kaumu imefedheheshwa sana; harakisheni na kufanya tadbiri.

وَ اِنِّیۡ لَعَمۡرِ اللّٰہِ لَسۡتُ بِجَائِرٍ　　　وَ اِنۡ کُنۡتَ تَأۡتِیۡ بِالصَّوَابِ فَأُدۡبِرُ

Nami, Wallahi, si dhalimu; kama jibu lako litakuwa sahihi, basi nitarudi nyuma.

وَ اِنۡ کُنۡتَ لَا تُصۡغِیۡ اِلَیۡنَا تَغَافُلًا　　　تَھُدُّ وَ تُلۡغِیۡ کُلَّمَا کُنۡتَ تَعۡمُرُ

Na usipojali kauli yetu hii, basi utalibomoa na kuliharibu jengo ulilolijenga.

اَلَسۡتَ تَرٰی یَرۡمِیۡ الۡقَنَا مَنۡ عِنۡدَکُمۡ　　　جَھُوۡلٌ وَ لَا یَدۡرِیۡ الۡعُلُوۡمَ وَ اَکۡفَرُ

Je, huoni kuwa anakurushia mikuki mtu ambaye kwa maoni yako ni jahili na kafiri.

فَاَیۡنَ ضَرَتۡ مِنۡکُمۡ عَلَامَۃُ صِدۡقِکُمۡ　　　وَ اَیۡنَ اخۡتَفٰی عِلۡمٌ بِہٖ کُنۡتَ تُکۡفِرُ

Basi, imepotea wapi alama ya ukweli wako, na imetokomea wapi elimu ambayo kwayo ulikuwa ukinikufurisha.

وَ اَیۡنَ التَّصَلُّفُ بِالۡفَضَائِلِ وَ النُّھٰی　　　وَ اَیۡنَ بِھٰذَا الۡوَقۡتِ قَوۡمٌ وَّ مَعۡشَرُ

Na yako wapi maringo yako ya fadhila na akili yako? Na wako wapi wakati huu watu wako na kundi lako?

وَ اَیۡنَ عَفَتۡ مِنۡکُمۡ طَلَاقَۃُ اَلۡسُنٍ　　　سِلَاطٍ عَلَیۡنَا مِثۡلَ سَیۡفٍ یُّشَھَّرُ

Na umepotea wapi umbuji na ufasaha uliokuwa dhidi yetu kama upanga uliochomolewa.

وَ فِیْ خَمْسَةٍ قَدْ تَمَّ نَظْمُ قَصِیْدَتِیْ          بَلِ الْوَقْتُ خَالِصَةً اَقَلُّ وَ اَقْصَرُ

Na kasida yangu ilikamilika katika siku tano, bali muda halisi ni chini ya huo, yaani siku tatu.

فَفَكِّرْ بِجُهْدِكَ خَمْسَ عَشْرَةَ لَیْلَةً          وَ نَادِ حُسَیْنًا اَوْ ظَفَرْ اَوْ اَصْغَرُ

Lakini jibidiishe kwa mausiku kumi na matano, na waite Muhammad Husain na Kadhi Dhafaruddin na Asghar Ali kukusaidia.

وَ هٰذَا مِنَ الاٰیٰتِ یَا اَكْبَرَ الْعِدَا          فَهَلْ اَنْتَ تَنْسِجُ مِثْلَهَا یَا مُحَسِّرُ

Na hii ni ishara ya Mungu, ewe adui mkubwa. Je utaweza kutunga kama hii?

عَلٰی مَوْطِنٍ یَّخْشَی الْجَبَانُ نُجَبِّرُ          فَاِنْ كُنْتَ فِیْ شَیْءٍ فَبَادِرْ وَ نَبْدِرُ

Pale wanapokimbia tumesimama imara; kama u kitu, basi njoo shindanoni, kisha tutaona.

اَ تَسْتُرُ بَغْیًا بَرْقَ اٰیٰتِ رَبِّنَا          سَیُظْهِرُ رَبِّیْ كُلَّمَا كُنْتَ تَسْتُرُ

Je unatka kuficha mwanga wa ishara ya Mola wetu, basi Mungu wangu atafichua yote unayoyaficha.

تُرِیْدُوْنَ ذِلَّتَنَا وَ نَحْنُ هَوَانَكُمْ          وَ لِلّٰهِ حُكْمٌ نَافِذٌ فَسَیَأْمُرُ

Mnataka dhila yetu, nasi yenu; na hukumu yenye nguvu ni ya Mungu, Yeye Atatoa uamuzi.

تَرَكْتُمْ كَلَامَ اللّٰهِ مِنْ غَیْرِ حُجَّةٍ          وَ اِنَّ كَلَامَ اللّٰهِ اَهْدٰی وَ اَظْهَرُ

Mmetengana na Neno la Mungu pasipo dalili, ilhali Neno la Mungu ni mwongozo hasa na wazi kabisa;

وَ يَسَّرَهُ الْمَوْلٰی لِيَدَّكَّرَ الْوَرٰی فَلَا شَكَّ اَنَّ الذِّكْرَ اَجْلٰی وَ اَيْسَرُ

Na Mungu Alilifanya kuwa rahisi kwa watu kulikumbuka; basi hakuna shaka kwamba Kurani ni wazi na rahisi sana.

وَ فِيْهِ تَجَلَّتْ بَيِّنٰتٌ مِّنَ الْهُدٰی وَ سَمَّاهُ فُرْقَانًا عَلِيْمٌ مُقَدِّرُ

Na ndani mwake mna miongozo wazi, na Mungu Akaiita Furkani.

وَ سَمَّاهُ تِبْيَانًا وَّ قَوْلًا مُّفَصَّلًا فَاَیَّ حَدِيْثٍ بَعْدَهُ نَتَخَيَّرُ

Na Akaiita تِبْيَان (ibainishayo) na kauli مُفَصَّل (kamilifu); basi ni hadithi gani tuichugue kinyume chake.

فَدَعْ ذِكْرَ بَحْثٍ فِيْهِ ظُلْمٌ وَّ فِرْيَةٌ وَ فَكِّرْ بِنُوْرِ الْقَلْبِ فِيْمَا نُكَرِّرُ

Basi achana na majadiliano yenye dhuluma na uongo ndani mwake, na uzingatie maneno yetu kwa nuru ya moyoni.

لَنَا الْفَضْلُ فِي الدُّنْيَا وَ اَنْفُكَ رَاغِمٌ وَ كُلُّ صَدُوْقٍ لَّا مَحَالَةَ يُظْهَرُ

Tumejaliwa utukufu duniani, nawe u ndani ya dhila; na kila mkweli hatimaye hujaliwa kushinda.

عَلَوْنَا بِسَيْفِ اللهِ خَصْمًا اَبَا الْوَفَا فَنُمْلِيْ ثَنَاءَ اللهِ شُكْرًا وَّ نَسْطُرُ

Tumemwua adui yetu Abul-Wafaa (Maulawii Thana'ullah) kwa upanga wa Mungu, basi twaandika sifa za Mungu kwa kutoa shukrani.

اَ يَزْعَمُ اَنِّيْ قَدْ تَقَوَّلْتُ عَامِدًا فَوَيْلٌ لَّهُ يُغْوِی الْاُنَاسَ وَ يَهْذُرُ

Je, anadhani, nilizua uongo makusudi; basi ole wake, anapotosha watu na kupayuka.

اَرٰی بَاطِلًا قَدْ ثَلَّمَ الْحَقُّ جُدْرَهُ     فَاَضْحَی الْهُدٰی مِثْلَ الضُّحٰی یُتَبَصَّرُ

Nauona ukweli umetoboa kuta za uongo; basi mwongozo ukawa wazi kama mwanga wa mchana.

وَ اِنِّیْ طَبَعْتُ الْیَوْمَ نَظْمَ قَصِیْدَتِیْ     وَ کَانَ اِلٰی نِصْفٍ تَمَشّٰی نُوْمْبَرُ

Na leo nilichapisha shairi la kasida yangu, na mwezi wa Novemba ulikuwa umepita karibu nusu,

کَذَالِکَ مِنْ شَعْبَانَ نِصْفٌ کَمِثْلِهِ     فَیَا رَبِّ بَارِکْهَا لِمَنْ یَّتَذَکَّرُ

Kadhalika nusu ya Shaabani pia; basi Ee Mola wangu, ibariki kwa wale watakao mwongozo.

رمَیْتُ لِاَغْتَالَنْ وَّ مَا کُنْتُ رَامِیًا     وَ لٰکِنْ رَّمَاهُ اللّٰهُ رَبِّیْ لِیُظْهِرُ

Nilitupa kama mshale kijitabu hiki ili kumwulia mbali adui; na kwa kweli sikutupa, bali ni Mungu Aliyetupa ili Anishindishe.

وَ هٰذَا لِعَهْدٍ قَدْ تَّقَرَّرَ بَیْنَنَا     بِمُدٍّ فَلَمْ نَنْکُثْ وَ لَمْ نَتَغَیَّرُ

Na tumetunga kasida hii kwa mujibu wa agano lililowekwa kijijini Mudd; nasi hatukuvunja agano wala hatukubadilika.

نَرٰی بَرَکَاتٍ نَزَّلُوْهَا مِنَ السَّمَا     لَنَا کَاللَّوَاقِحِ وَ الْکَلَامُ یُنَضَّرُ

Tunaona baraka ambazo zimeshuka kwetu kutoka mbinguni, kama ngamia wenye mimba, na kauli ikastawi.

وَ وَاللهِ اِنَّ قَصِيْدَتِيْ مِنْ مُّؤَيِّدِيْ        فَنُثْنِيْ عَلٰى رَبٍّ كَرِيْمٍ وَ نَشْكُرُ

Na, Wallahi, kasida yangu ndiyo kutoka kwa Mungu Msaidizi wangu, basi twamtukuza Mola Karimu na kumshukuru.

وَ يَا رَبِّ اِنْ اَرْسَلْتَنِيْ مِنْ عِنَايَةٍ        فَاَيِّدْ وَ كَمِّلْ كُلَّ مَا قُلْتُ وَ انْصُرُ

Na Ee Mola wangu, ikiwa umenituma kwa hisani yako, basi nisaidie na kamilisha yote niliyoyafikiria.

بِسۡمِ اللّٰہِ الرَّحۡمٰنِ الرَّحِیۡمِ [44] نَحۡمَدُہٗ وَ نُصَلِّیۡ عَلٰی رَسُوۡلِہِ الۡکَرِیۡمِ [45]

## Ubeti

قادر کے کاروبار نمودار ہو گئے کافر جو کہتے تھے وہ گرفتار ہو گئے
کافر جو کہتے تھے وہ نگونسار ہو گئے جتنے تھے سب کے سب ہی گرفتار ہو گئے

[Tafsiri ya Ubeti]

Kazi za Mweza zimeonekana; waliokufurisha wamekamatwa.

Waliokuwa wakikufurisha wameaibika, wote waliopo wamekamatwa.

## Tangazo la Rupia Elfu Kumi

Tangazo hili linachapishwa ili kudhihirisha ishara hii ya Mwenyezi Mungu ambayo itatimiza bishara moja kama ishara nyinginezo. Yaani, hii pia ni ishara iliyoahidiwa kudhihiri mpaka mwishoni mwa Desemba 1902. Na pamoja nalo lipo tangazo la rupia elfu kumi kama shahidi wa jambo hili kwamba kwa kuhakikisha ukweli wa madai yetu wapinzani wametanabahishwa kwa nguvu kiasi gani na kwa kutumia mali kiasi gani. Maulawii Thana'ullah wa Amritsar alisema kwa sauti ya juu kijijini Mudd kwamba hatuwezi kukiita kitabu *I'jazul Masihi* kuwa ni muujiza,

[44] Kwa jina la Mwenyezi Mungu, Mwingi wa rehema, Mwingi wa ukarimu.

[45] Twamhimidia Yeye na kumsalia Mtume wake Mkarimu.

nami naweza kuandika kitabu kama hicho. Na ni kweli pia kwamba kama wapinzani wanaweza kushindana na katika muda uliowekwa waweze kuandika kitabu kama hicho, basi hii si tu kwamba itakuwa ni muujiza, bali katika hali hii tutathibitika kuwa waongo kabisa. Lakini, marafiki zetu Maulawii Seyid Muhammad Sarwar na Maulawii Abdullah walipofika Qadian tarehe 2 Novemba 1902, basi baada ya siku chache nikapata wazo kwamba kama waambiwe kuleta, mfano wa *I'jazul Masihi*, watasema, kama hao wapinzani sikuzote wanavyotumia udhuru mbovu, kwamba tunavyofahamu kitabu cha *I'jazul Masihi* hakikutayarishwa katika siku sabini – jinsi kuhusu hotuba iliyotolewa katika *Jalsa Muhotso* Alivyosema Maulawii Abu Said Muhammad Husain kwamba hotuba hii ilitayarishwa zamani na iliandikwa baada ya kufikiria kwa muda fulani. Basi kama sasa pia wakisema kuwa *I'jazul Masihi*, si katika siku sabini, bali kimeandikwa katika miezi sabini, basi jambo hili litakuwa lenye mashaka kwa watu. Na nilikuwa na fikira hii kwa siku chache kwamba nifanye nini. Hatimaye, jioni ya Novemba 6, 1902 nilitiliwa moyoni mwangu kwamba nitunge kasida moja kuhusu mjadala wa Mudd, kwa sababu muda wa kutunga kasida ni wa yakini kabisa. Kwani hakuna anayeweza kukataa kwamba huko Mudd majadiliano yakafanyika 29 na 30 Oktoba 1902. Kisha tarehe 2 Novemba marafiki zetu wakafika Qadian na

tarehe 7 Novemba 1902 nikaenda katika mahakama ya Munshi Nasiruddin, Hakimu wa Mahakama ya Batala kwa kutoa ushahidi. Labda nikatunga ubeti mmoja au mbili njiani. Lakini 8 Novemba 1902 nikaanzia kutunga kasida kwa umakini kamili na nikamaliza kasida na insha ya Kiurdu katika siku tano. Hivyo, ikawa haina shaka kwamba kasida ilitungwa katika muda gani, kwa sababu matukio ya mjadala huo uliofanyika tarehe 29 na 30 Oktoba 1902 yameelezwa katika kasida hii na insha ya Kiurdu. Hivyo, ikiwa kasida hii na insha ya Kiurdu haikutayarishwa katika kipindi hiki kifupi, bali ilitayarishwa kabla, basi yapaswa kunikubali kuwa mjuzi wa mambo ya ghaibu niliyetoa habari ya matukio yote kabla ya kutokea hayo. Ilmuradi, hii ni ishara moja kubwa na ni njia rahisi sana ya kutoa uamuzi. Na ikumbukwe kwamba, kama nilivyoeleza hivi punde, muda wote huo haukutumika kuandika kasida tu, bali pia kuandika makala ya Kiurdu yaliyoambatanishwa na kasida hii, na hizo zote mbili pamoja ni ishara kutoka kwa Mwenyezi Mungu. Na kwa ajili ya mashindano na kupata zawadi ya rupia elfu kumi, sharti la lazima ni kwamba mtu atakayetunga kasida kwa kushindana, aandike pia jibu la makala ya Kiurdu kwa kuvunjilia mbali hoja zangu, ibara yake isipungue kuliko kiasi cha ibara yetu. Na kama yeyote kati yao akiacha mojawapo katika hizo mbili atakuwa ni mvunjaji wa sharti hili. Siwakalifishi wapinzani

wangu kufanya kazi ngumu ambayo sikufanya mimi mwenyewe. Ni dhahiri kwamba ibara ya Kiurdu pia inahusiana na tukio hilo la majadiliano na ndani yake amejibiwa Maulawii Thana'ullah upinzani wake aliokuwa ameleta. Katika hali hii, ni nani awezaye kushuku kwamba maandishi ya Kiurdu yalikuwa yameandikwa mapema. Kwa hiyo, nina haki ya kudai kwamba jinsi ibara ya Kiurdu na kasida ilivyotayarishwa katika muda mfupi wa kimuujiza watu hao wanaofikiria maandishi hayo kuwa ni uzushi wa binadamu walete mfano wake katika muda huo huo. Nasema kwa kuapa kwa Mwenyezi Mungu kwamba muda nilioutumia kuandika insha ya Kiurdu na kasida, kama katika muda kiasi hicho hicho wakichapisha makala ya Kiurdu kiasi hicho ambamo lijibiwe kila jambo, na jambo lolote lisibakie, na kasida kiasi hicho yenye idadi hiyo ya beti zielezazo matukio hayo kwa lugha fasaha na balagha, basi nitawapa rupia elfu kumi taslimu. Hii ni ikrari yangu halali ya kisheria ambayo haitavunjwa na wanayoweza kutekelezesha hata kwa njia ya mahakama. Sasa kama Maulawii Thana'ullah na wapinzani wangu wengineo wakwepe na waendelee kuniita kafiri na dajali, basi hawatakuwa na haki, baada ya kushindwa na kunyamzishwa, kwamba wadhihirishe ujanja hivyo, bali hao watakuwa waongo machoni pa umma. Pia nawaruhusu kwamba wajumuike wote kuandika jibu la makala ya Kiurdu na kasida ielezayo

matukio ya mjadala; sitakinzana hata kidogo. Kama wakichapisha kasida na jibu la makala yaliyoambatanishwa nayo, katika muda uliowekwa, basi bila shaka nitathibitika kuwa mwongo. Lakini kama kasida yangu, wapasawa waandike tafsiri pia kwa Kiurdu chini ya kila ubeti, na waichukulie kama sharti miongoni mwa masharti. Kwa shindano hili yataamuliwa mabishano yote. Na Mungu Akipenda, asubuhi ya 16 Novemba 2 nitamtumia Maulawii Thana'ullah kijitabu hiki *I'jaz Ahmadi* ambacho atakichukua Maulawii Seyid Muhammad Sarwar kumpelekea yeye. Na tarehe hiyo hiyo nitakituma kijitabu hiki kwa njia ya rejista kwa mabwana wote waliotajwa katika kasida hii. Mwishowe nimeridhika pia kuwapa wapinzani hao wote kwa kuandika na kuchapisha jibu liliotajwa hapo juu, muhula wa siku kumi na tano, kwani hata wakizidi kubisha, hata hivyo kasida yangu itawafikia mpaka tarehe 18 au 19 Novemba 1902. Kwa vyovyote italazimika kukubali kwamba kuanzia Novemba mosi 1902 hadi katikati ya Novemba ni siku kumi na tano, lakini hata hivyo, kwa kuwahurumia hali yao, kwa kukamilisha hoja nimewaongezea siku tano nyingine na siku za kupostia hazipo humo. Basi, kwa kuepuka mzozo twaweka siku tatu za kupostia, yaani tarehe 17, 18, 19 Novemba 1902. Hadi siku hizi, kwa vyovyote, kasida hii itawafikia sehemu mbalimbali. Sasa muda wao utaanzia 20

Novemba. Kwa hiyo muda huu utaishia tarehe 10 Desemba 1902. Kama katika muda wa siku ishirini utakaoishia jioni ya 10 Desemba 1902, wakichapisha jibu la kasida hii na makala ya Kiurdu, basi mfahamu kuwa nimeangamia na silsila yangu imebatilika. Hapo wanajumuiya wangu wote wanapaswa kuniacha na kujitenga nami. Lakini hata sasa pia wapinzani wakikwepa makusudi, si tu kwamba watanyimwa zawadi ya rupia elfu kumi, bali laana kumi zitakuwa hadhi yao ya tangu azali. Katika zawadi hii, Thana'ullah atapata elfu tano, na watano wengine watapata elfu moja moja ikiwa wakishinda.

Amani iwe juu ya wale wanaofuata mwongozo.

**Mnyenyekevu Mirza Ghulam Ahmad wa Qadian**.